

**RIPOTI YA MDHIBITI NA MKAGUZI MKUU WA
HESABU ZA SERIKALI KUHUSU TAARIFA ZA FEDHA
ZA SERIKALI KUU KWA MWAKA ULIOISHIA TAREHE
30 JUNI, 2012**



JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA
OFISI YA TAIFA YA UKAGUZI



Ofisi ya Taifa ya Ukaguzi, Barabara ya Samora, S.L.P. 9080, Dar es Salaam.
Simu ya Upepo: 'Ukaguzi' D'Salaam, Simu: 255(022)211515/8, Nukushi: 255(022)2117527, Barua
pepe: ocag@nao.go.tz, Tovuti: www.nao.go.tz

Unapojobu tafadhali taja:
Kumb. Na.FA.27/249/01//2011/2012

Tarehe: 28 Machi, 2013

**Kuwasilisha Taarifa ya Mwakaya Mdhibitina MkaguziMkuu wa Hesabu
za SerikaliuuyaTaarifaza Fedhaza SerikaliKuukwa mwakaulioishia
tarehe 30Juni, 2012**

Mh. Dkt. Jakaya M. Kikwete,
Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania,
S.L.P. 9120,
Ikulu,
Dar es Salaam.

**Yah: Kuwasilisha Ripoti ya Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za
Serikali kuhusu Taarifa za Fedha za Serikali Kuu kwa mwaka
ulioishia tarehe 30 Juni, 2012**

Kwa mujibu wa Ibara ya 143 (4) ya Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa
Tanzania (iliyorekebishwa 2005) na Kifungu cha 34 (1)(c) cha Sheria ya
Ukaguzi wa Umma Na.11 ya mwaka 2008, ninawasilisha kwako ripoti
iliyatajwa hapo juu.

Nawasilisha.

Ludovick S. L. Utouh
MDHIBITI NA MKAGUZI MKUU WA HESABU ZA SERIKALI.

ii

**Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali,
Ofisi ya Taifa ya Ukaguzi,
Jamhuri ya Muungano wa Tanzania.**

Ilianizishwa kwa mujibu wa Ibara ya 143 ya Katiba ya Jamhuri ya Muungano
Madaraka na wajibu wa Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali
yameelezwa kwenye Ibara ya 143 ya Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania
(iliyorekebishwa 2005) na kufafanuliwa zaidi katika Kifungu cha 10 (1) cha Sheria
ya Ukaguzi wa Umma Na.11 ya mwaka 2008.

Dira

Kuwa kituo cha ufanisi katika ukaguzi wa hesabu za Serikali na taasisi za umma.

Dhima

Kutoa huduma ya ukaguzi wa hesabu yenye tija ili kuimarisha uwajibikaji na
thamani ya fedha katika kukusanya na kutumia rasilimali za umma.

**Katika kutoa huduma zenyenye ubora, ofisi hii inaongozwa na vigezo vya msingi
vifuatavyo:**

- 1) **Uadilifu:** sisi ni asasi adilifu inayotoa huduma kwa namna isiyio na upendeleo.
- 2) **Ubora:** sisi ni wanataluma wanaotoa huduma zenyenye ubora kwa kuzingatia
viwango kubalifu vya ukaguzi
- 3) **Uaminifu:** tunahakikisha kuwa na kiwango cha juu cha uaminifu na kuzingatia
utawala wa sheria.
- 4) **Mtazamo wa watu:** tunatazama na kukazia zaidi katika matarajio ya wadau
wetu kwa kujenga utamaduni mzuri wa kuhudumia mteja na kuwa na
watumishi wataalamu na wenye motisha ya kazi.
- 5) **Uvumbuzi:** sisi ni asasi ambayo wakati wote inahamasisha utamaduni wa
kupokea na kuendeleza mawazo mapya kutoka ndani na nje ya asasi.
- 6) **Matumizi bora ya rasilimali:** sisi ni asasi inayothamini na kutumia rasilimali za
umma ilizokabidhiwa kwa umakini mkubwa.

DIBAJI

Kwa kipindi cha miaka mitano (kuanzia 2007/2008), jamii imeanza kuona maboresho katika mchakato wa uwajibikaji nchini. Sio tu kwamba maboresho haya yametokana na ripoti zangu za ukaguzi za kila mwaka, lakini pia ni kwa sababu ya utashi wa kisiasa uliowekwa na uongozi wa awamu ya nne ya serikali chini uongozi wa Mheshimiwa Dkt Jakaya Mrisho Kikwete na michango ya kimaendeleo inayotolewa na Bunge la Jamhuri wa Tanzania kuititia kamati zake za kudumu ambazo zimesimamia na kuhimiza uwajibikaji katika matumizi ya fedha za umma.

Ninapenda kutoa shukrani zangu kwa wale wote waliochangia kwa njia moja au nyingine kuniwezesha kutimiza majukumu yangu ya kikatiba na hatimaye kutoa ripoti hii kwa wakati.

Ripoti hii ya Ukaguzi inawasilishwa kwa Mheshimiwa Rais kwa mujibu wa Ibara ya 143 ya Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania na Kifungu 34(1)(c) cha Sheria Na.11 ya Ukaguzi wa Umma ya mwaka 2008.

Kwa mujibu wa Ibara 143 (2) (c) Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali anatakiwa angalau mara moja kila mwaka kufanya ukaguzi na kutoa taarifa juu ya ukaguzi wa Hesabu za Serikali ya Jamhuri ya Muungano, hesabu zinazosimamiwa na watumishi wote wa Serikali ya Jamhuri ya Muungano, hesabu za Mahakama zote za Jamhuri ya Muungano na hesabu zinazosimamiwa na Katibu wa Bunge.

Chini ya Ibara ya 143(4) ya Katiba ya Jamhuri wa Muungano wa Tanzania, Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali anatakiwa kuwasilisha kwa Rais kila ripoti anayotoa chini ya Ibara 143 (2). Baada ya kupokea ripoti hizo, Rais ataagiza wanaohusika waziwasilishwe ripoti hizo mbele ya Kikao cha kwanza cha Bunge ikiwezekana ndani ya siku saba baada ya kuanza kwa kikao.

Uhuru wa kiutendaji wa ofisi yangu kwa kiasi kikubwa umeimarika baada ya kuanza kutumia sheria ya Ukaguzi wa Umma Na 11 ya mwaka 2008. hata hivyo kulingana na viwango vya kimataifa maboresho zaidi yanahitajika hasa kwa upande wa kupanga mishahara na ajira za watumishi wa ofisi yangu ili kuniwezesha kutekeleza majukumu yangu ya kikatiba kwa ufanisi zaidi.

Kutungwa kwa Sheria ya Ukaguzi wa Umma Na. 11 ya mwaka 2008 kumeongeza mawanda ya ukaguzi wangu kwa kunipa madaraka ya kufanya

kaguzi nyingine zaidi ya ukaguzi wa kawaida wa taarifa za fedha. Kwa mujibu wa sheria hii natakiwa kufanya ukaguzi wa ufanisi, utambuzi na mazingira na kaguzi mbalimbali maalum kama zinavyojitokeza. Ni matumaini yangu kwamba, kwa kuanzishwa kwa sheria mpya ya Ukaguzi wa Umma, Ofisi yangu itaweza kuimarisha udhibiti wa fedha na kuisaidia Serikali kuimarisha uwajibikaji. Sheria hii pia itaniwezesha kuwa huru katika kulithibitishia Bunge masuala yanayohusu uwajibikaji, uwazi na matumizi bora ya rasilimali hasa kuona kwamba rasilimali hizo zimetumika vizuri kwa kuzingatia uchumi, ufanisi na kama ilivyotarajiwa na kupitishwa na Bunge.

Ni vyema kutambua kuwa wakati ofisi yangu inatoa taarifa kuhusu ukiukwaji wa sheria, taratibu na kanuni mbalimbali na udhaifu katika mifumo ya udhibiti wa ndani kwenye taasisi za Umma na hasa Serikali Kuu, lakini wajibu wa kuhakikisha kuwepo kwa mifumo thabiti ya udhibiti wa ndani ni jukumu la Maafisa Masuuli.

Bunge na watanzania kwa ujumla wanatarajia kuona kwamba Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali na Ofisi ya Taifa ya Ukaguzi watahakikisha utoaji wa taarifa za fedha na usimamizi wa rasilimali katika Serikali Kuu kuhusiana na ufanisi na ubora na usimamizi wa mipango iliyowekwa. Kwa njia ya ukaguzi, ofisi inachangia katika kutoa mapendekezo kuhusu uimarishaji na uboreshaji wa sekta ya Umma. Kwa msingi huu, Serikali Kuu na Ofisi yangu zina mchango mkubwa wa kutoa kwa Bunge katika kujenga imani kwa Umma katika usimamizi wa rasilimali za Umma.

Ingawa majukumu ya ofisi yangu na yale ya taasisi za umma yanatofautiana, hata hivyo matarajio ya usimamizi bora wa rasilimali yanafanana.

Ili kukidhi matarajio ya Wabunge na Umma wa Tanzania kwa mapana zaidi, Ofisi ya Taifa ya Ukaguzi imeendelea kufanya uchambuzi wa njia bora zaidi za kufanya ukaguzi na kuongeza wigo wa masuala yanayokaguliwa na hivyo kuimarisha utendaji wa uwajibikaji katika sekta ya Umma. Aidha, tunahakikisha ukaguzi wetu unalenga kuyapa kipaumbele maeneo muhimu ili kuchangia maendeleo katika sekta ya Umma. Kwa kuwa kazi ya ukaguzi ni chachu katika usimamizi wa fedha, tutaendelea kujadili masuala yanayoathiri utawala/uongozi katika sekta ya Umma, hasa katika utoaji wa taarifa za usimamizi wa fedha na masuala ya utawala bora. Kamati ya Bunge ya Hesabu za Serikali Kuu (PAC), moja kati ya kamati za Kudumu za Bunge, imefanya kazi kubwa ya kuboresha utendaji wa Maafisa Masuuli wa

Serikali Kuu ambao utendaji wao haukufikia matarajio ya Kamati hiyo. Pamoja na jitihada hizo, ninaamini kuwa Serikali Kuu ina jukumu muhimu katika kuboresha usimamizi wa fedha za Umma.

Napenda kutambua mchango wa wafanyakazi wa Ofisi yangu kwa utaalamu, juhudui kubwa walioonyesha katika kutimiza malengo tuliojipangia licha ya kufanya kazi katika mazingira magumu ambayo ni pamoja na kukosa fedha za kutosha, kukosa vitendea kazi, mishahara duni na upungufu wa watumishi, na wakati mwingine kufanya kazi maeneo ya vijijini ambayo sio rahisi kufikika.

Napenda pia kutambua kazi iliyofanywa na Mamlaka ya Udhibiti wa Manunuzi ya Umma, Kitengo cha Usimamizi wa Mali za Serikali na Msajili wa Hazina kwa kuandaa na kuwasilisha taarifa za kiutendaji za Taasisi zilizoko chini yao kwa kipindi cha mwaka wa fedha 2011/2012 na kuonyesha mambo mengi ambayo kwa kiasi kikubwa yalijitokeza kwenye ripoti yangu ya mwaka uliopita. Nipenda kuzitambua kazi zilizofanywa na Taasisi hizi ambazo nimeona ni vyema nikazijumuisha kwenye ripoti yangu.

Natarajia kuwa Bunge litaona taarifa hii kuwa ni muhimu katika kuiwajibisha Serikali kwa jukumu lake la usimamizi wa fedha za Umma na utoaji wa huduma kwa Watanzania. Hivyo, nitafurahi kupata maoni kutoka kwa watumiaji wa ripoti hii jinsi gani nitaweza kuboresha taarifa yangu kwa siku zijazo.

Ludovick S. L. Utouh

MDHIBITI NA MKAGUZI MKUU WA HESABU ZA SERIKALI

Mdhhibit na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali,
Ofisi ya Taifa ya Ukaguzi,
S.L.P. 9080,
Dar es Salaam.

Machi, 2013

SHUKRANI

Napenda kutoa shukrani kwa wote walioniwezesha kutekeleza majukumu yangu ya kikatiba. Kwa mara nyingine, napenda kutoa shukrani zangu kwa wafanyakazi wote wa Ofisi yangu kwa kuniwezesha kutoa ripoti hii kwa wakati. Ninawajibika kutoa shukrani zangu za pekee kwa familia yangu na familia za wafanyakazi wa Ofisi yangu kwa kutuvumilia kwa kutokuwa nao kwa muda mrefu wakati tukikamilisha majukumu haya ya kikatiba.

Vilevile, natoa shukrani zangu za dhati kwa wafadhili hasa Ofisi ya Taifa ya Ukaguzi ya Sweden, Serikali ya Sweden kupitia Shirika la Kimataifa la Misaada la Maendeleo la Sweden, Benki ya Dunia kupitia Mradi wa Kusimamia na Kuboresha Sekta ya Fedha za Umma (PFMRP), Benki ya Maendeleo ya Afrika (AfDB), Shirika la Misaada la Ujerumani (GIZ), Shirika la Misaada la Marekani (USAID), Serikali ya China na wote wenye mapenzi mema ambao wamechangia kwa kiasi kikubwa kuboresha Ofisi yangu. Michango wao umekuwa na manufaa makubwa katika kuendeleza na kukuza rasilimali watu, nyezo za kazi (magari), mifumo ya teknolojia ya mawasiliano na vitendea kazi. Hata hivyo, bado misaada zaidi inahitajika kwa ajili ya kuboresha kazi za ukaguzi katika sekta ya umma kwa kuzifanya kuwa za kisasa zaidi. Jambo hili lingeweza kwenda haraka endapo angepatikana mfadhili wa kugharamia ujenzi wa Kituo cha Mafunzo ya Ukaguzi kitakachojengwa Gezaulole katika Manispaa ya Temeke.

Aidha, natoa shukrani zangu kwa Hazina, Mlipaji Mkuu wa Serikali, Maafisa Masuuli, Mkurugenzi Mkuu wa Mamlaka ya Ununuzi wa Umma, Mhakiki Mali Mkuu na wadau wote kwa taarifa mbalimbali muhimu walizonipatia ili kukamilisha kazi hii. Pia namshukuru Mpiga Chapa Mkuu wa Serikali kwa kuniwezesha kutoa ripoti kwa wakati.

Kwa kumalizia, nawashukuru wafanyakazi wote wa Umma popote pale walipo Tanzania Bara, wawe ni wa Serikali Kuu au Halmashauri bila ya kuwasahau walipa kodi ambao ndio walengwa wa ripoti hii. Michango yao imekuwa msaada mkubwa katika ujenzi wa Taifa ambao hauwezi kupuuzwa hata kidogo.

Naomba Mungu awabariki wote kwa uwajibikaji katika matumizi ya rasilimali za umma nchini.

Vifupisho

A/C	Akaunti
ACGEN	Mhasibu Mkuu wa Serikali
Act	Sheria ya Fedha za Umma Na.6 ya 2001 kama ilivyorekebishwa mwaka 2004
CAG	Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali
CDTI	Taasisi ya Maendeleo ya Jamii na Mafunzo
CFS	Taarifa Jumuifu za Fedha
CPO	Ofisi Kuu ya Malipo
FDCS	Vyuo vya Maendeleo ya Wananchi
HIV	Upungufu wa Kinga Mwilini
IFMS	Mfumo Funganifu wa Usimamizi wa Fedha
INTOSAI	Taasisi ya Kimataifa inayojumuisha Asasi kuu za Ukaguzi wa Hesabu
JKT	Jeshi la Kujenga Taifa
LART	Mfuko wa Kusimamia Mikopo na Ufutiliaji wa Madeni
LGAs	Mamlaka za Serikali za Mitaa
MDAs	Wizara, Idara na Wakala
NAO	Ofisi ya Taifa ya Ukaguzi
PFA	Sheria ya Fedha za Umma Na. 6 ya 2001
PFMRP	Programu ya Marekebisho ya Usimamiaji Fedha za Umma
PFR	Kanuni za Fedha za Umma
PMG	Mlipaji Mkuu wa Serikali
PPA	Sheria ya Manunuzi wa Umma Na. 21 ya 2004
RAS	Sekretarieti za Tawala za Mikoa
RCCB	Daftari la Kukusanya Maduhuli
Reg.	Kanuni
Sect.	Kifungu
SUMA	Shirika la Uchumi na Maendeleo
TANSORT	Shirika la Kuchambua Almasi la Serikali ya Tanzania
TCAA	Mamlaka ya Usafiri wa Anga Tanzania
UNESCO	Shirika la Elimu, Sayansi na Utamaduni la Umoja wa Mataifa
URT	Jamhuri ya Muungano wa Tanzania
USD	Dola za Kimarekani
TRA	Mamlaka ya Mapato Tanzania
IFAC	Shirikisho la Kimataifa la Wahasibu
SNAO	Ofisi ya Taifa ya Ukaguzi ya Sweden
PAA	Sheria ya Ukaguzi wa Umma

YALIYOMO

Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali	i
Dira	i
Dhima	i
DIBAJI	ii
SHUKRANI	v
Vifupisho.....	vi
YALIYOMO.....	vii

MUHTASARI WA MAMBO MUHIMU KATIKA RIPOTI YA UKAGUZI WA	
TAARIFA ZA FEDHA ZA SERIKALI KUU KWA MWAKA 2011/2012....	xiii
1:Utangulizi	xiii
4:Dosari zilizobainika katika mchakato wa manunuza.....	xv

SURA YA 1	1
1.0 Utangulizi	1
1.1 Ukaguzi wa Taarifa za Hesabu za Umma	1
1.2 Majukumu na wajibu wa Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali kwa Wizara, Idara, Wakala na Sekretarieti za Mikoa	2
1.3 Muundo wa Kazi za Ukaguzi Ndani ya Ofisi ya Taifa ya .Ukaguzi	2
Ukaguzi wa Taasisi za Umoja wa Mataifa	3
1.4 Mawanda na viwango vya Ukaguzi vinavyotumika	4
1.4.1 Mawanda ya ukaguzi	4
1.4.2 Viwango vya Ukaguzi vinavyotumika.....	4
1.5 Sera ya Kiuhasibu	4
1.6 Wajibu wa Kisheria wa Wizara, Idara, Wakala na Sekretarieti za Mikoa	5
1.7 Mfumo wa Udhibiti wa Ndani	5

vii

1.8 Kutayarisha na kuwasilisha taarifa za fedha kwa ajili ya ukaguzi

SURA YA 2.....	7
MAPITIO YA UTEKELEZAJI WA MAPENDEKEZO YATOKANAYO NA HOJA ZA UKAGUZI KWA MIAKA ILIYOPITA.....	7
2.0 Utangulizi.....	7
i. Majibu kutoka kwa Mlipaji Mkuu wa Serikali (PMG)yaliyowasilishwa katika ripoti jumuifu ya Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali.	
	7
2.1 Ufuatiliaji wa majibu ya Mlipaji Mkuu wa Serikali yaliyowasilishwa kwa Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu	7
2.2 Baadhi ya shughuli za Serikali hazikujumuishwa katika . Hesabu Jumuifu za Taifa.....	29
2.3 Majibu ya taarifa za kila fungu kutoka kwa Afisa Masuuli yaliyowasilishwa kwa Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu ..za Serikali	29
2.4 Mamlaka ya Mapato Tanzania	30
2.5 Majibu ya hoja zitokanazo na ukaguzi wa Taarifa Jumuifu za Taifa	
	31
2.6 Utekelezaji wa maagizo yaliyotolewa na Kamati ya Bunge ya Hesabu za Serikali Kuu (PAC).....	33
SURA YA 3.....	52
MAKUSANYO YA MADUHULI NA MCHANGANUO WA FEDHA.....	
ZA MATUMIZI YA KAWAIDA NA MAENDELEO.....	52
3.0 Utangulizi.....	52
3.1 Ulinganisho wa fedha kutoka Mfuko Mkuu wa Serikali	52
3.2 Ulinganisho wa Fedha za Matumizi ya Kawaida na Maendeleo	53

3.3	Uwiano wa bajeti dhidi ya fedha zilizotolewa na Hazina kwa ajili ya maendeleo katika Wizara na Idara.....	55
3.4	Mamlaka ya Mapato Tanzania.....	56
3.5	Uwiano Kati ya Misamaha ya Kodi, Makusanyo na Pato la . Taifa	63
3.6	Matokeo ya utafiti wa uboreshaji wa mapato ya taifa.....	65
	SURA YA 4.....	83
	MATOKEO YA UKAGUZI WA AWALI WA MALIPO YA UZEENI.....	83
4.0	Utangulizi	83
4.1	Madhumuni ya ukaguzi wa awali	83
4.2	Mawanda ya ukaguzi wa awali	84
	SURA YA 5.....	91
	MAMBO MUHIMU YALIYOJITOKEZA KATIKA UKAGUZI WA WIZARA, IDARA, WAKALA NA SEKRETARIETI ZA MIKOA.....	91
5.1	Kushindwa kuweka kumbukumbu za masurufu	91
5.2	Mrahaba usiokusanywa Dola za Kimarekani	91
5.3	Ulipaji wa madeni ya miaka iliyopita kwa kutumia fedha zilizoidhinishwa kwa matumizi ya mwaka 2011/2012	92
5.4	Amana iliyokaa muda mrefu kwenye Shule za Sekondari	93
5.5	Malipo yaliyofanywa na Serikali kwenda Mfuko wa Pensheni . ya Utumishi wa Umma (PSPF) kulipia deni la pensheni	94
5.6	Masurufu yasiyorejeshwa kwa muda mrefu	96
5.7	Ulipaji wa deni la ATCL Dola za Kimarekani	96
5.8	Malipo yasiyokuwa na nyaraka za matibabu nje ya nchi	98
5.9	Mishahara iliyolipwa kwa maofisa waliostaafu kwa mujibu wa sheria 100	
5.10	Ada ya Utalii isiyokusanywa Dola za Kimarekani 158,000.....	101

5.11	Sehemu ya Bajeti ya Maendeleo iliyotolewa kwa Wizara ya Maji kufuatia Wajibu wa Tanzania kufikia Malengo	101
5.12	Ukaguzi wa Usimamizi wa Manunuzi	102
5.13	Usimamizi wa vifaa.....	106
	SURA YA 6.....	107
	UCHAMBUZI WA HESABU JUMUIFU NA DENI LA TAIFA	107
6.0	Utangulizi	107
6.1.	Tathimini ya Hesabu za Mwisho wa Mwaka	108
6.2	Taarifa ya misaada ya nje.....	110
6.3	Taarifa ya Madeni yasiyolipwa.....	111
6.4	Taarifa ya Mihadi ambayo haijalipwa.....	111
6.5	Taarifa ya malimbikizo ya Maduhuli	112
6.6	Taarifa ya upotevu	112
6.7	Ufuatiliaji wa mchakato wa malipo ya mirathi katikamahakama za mwanzo	113
6.8	Bakaa ya fedha taslimu za Serikali na zilizoko benki.....	116
6.9	Mwenendo wa Deni la Taifa.....	116
6.10	Dhamana za Serikali zilizopita muda wake	118
	SURA YA 7.....	121
	UWASILISHAJI NA UCHAMBUZI WA MATOKEO YA UKAGUZI.....	121
7.0	Utangulizi	121
7.1	Aina ya hati za ukaguzi	122
7.2	Hati inayoridhisha isiyokuwa na masuala ya msisitizo	126
7.3	Hati inayoridhisha yenye masuala ya msisitizo.....	126
7.4	Hati yenye shaka	126
7.5	Hati isiyoridhisha	126

7.6	Hati mbaya	126
7.7	Wizara /Idara na Sekretarieti za Mikoa zilizopewa hati inayoridhisha.	127
7.8	Wizara/Idara na Sekretarieti za Mikoa zilizopewa hatinayoridhisha yenye masuala ya msisitizo	127
7.9	Wizara, Idara, Wakala na Tawala za Mikoa zilizopata Hati yenye Shaka 155	
 SURA YA 8.....		164
MAJUMUISHO NA MAPENDEKEZO.....		164
8.0	Majumuisho.....	164
8.1	Mapendekezo.....	164
8.2	Matokeo ya ukaguzi wa awali wa mafao ya wastaifu	171
8.3	Usimamizi wa manunuvi ya umma	171
8.4	Mrahaba usiokusanywa Dola za Kimarekani	172
8.5	Amana za shule za sekondari zilizokaa muda mrefu.....	172
8.6	Masurufu yaliyokaa muda mrefu bila kurejeshwa.....	172
8.7	Malipo ambayo hayakupokewa na walipwaji	172
8.8	Ulipaji wa deni la ATCL Dola za kimarekani	172
8.9	Malipo ya matibabu nje ya nchi yasiyo na nyaraka	173
8.10	Malipo kwa watumishi ambao hawapo kwenye utumishi wa Umma 173	
8.11	Ada ya utalii isyokusanywa Dola za kimarekani	173
8.12	Masuala ambayo hayajashughulikiwa katika suluhisho . za benki. 173	
8.17	Maduhuli yasiyokusanywa	175
8.18	Taarifa ya Potevu.....	175

8.19	Mapato na matumizi ya taasisi zote za Serikali . kutojumuishwa katika Hesabu Jumuifu.	175
8.20	Dhamana zisizolipwa.	175
9.0	VIAMBATISHO	177
9.3	MATOKEO YA UKAGUZI WA AWALI WA MALIPO YA UZEENI.	186

MUHTASARI WA MAMBO MUHIMU KATIKA RIPOTI YA UKAGUZI WA TAARIFA ZA FEDHA ZA SERIKALI KUU KWA MWAKA 2011/2012

Taarifa ya Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali ihusuyo Taarifa za Fedha za Serikali Kuu imelenga maeneo yafuatayo:

- (1) Utangulizi
- (2) Mwelekeo wa hati za ukaguzi zilizotolewa
- (3) Udhafu uliogundulika katika mifumo ya udhibiti wa ndani
- (4) Mapungufu katika mchakato wa manunuzi
- (5) Masuala ya kodi
- (6) Masuala yahusuyo malipo ya wastaifu
- (7) Hitimisho na mapendekezo

1: Utangulizi

Sehemu hii inaeleza kwa muhtasari matokeo ya ukaguzi wa Taarifa za Fedha katika Serikali Kuu kwa mwaka wa fedha ulioishia tarehe 30 Juni, 2012. Mawanda ya ukaguzi katika Serikali Kuu yanajumuisha Wizara, Idara zinazojitegeremea, Wakala za Serikali na Sekretarieti za Mikoa.

2: Mwelekeo wa Hati za Ukaguzi zilizotolewa

Matokeo ya ukaguzi kwa miaka miwili mfululizo ulioishia tarehe 30 Juni, 2012 umeonyesha kuboreka kwa hati zilizotolewa kwa Serikali Kuu na Taasisi zake ikilinganishwa na mwaka uliopita kama inavyoonekana katika jedwali hapa chini:

Jedwali Na. 1: Mwelekeo wa Hati za Ukaguzi

Aina	Hati za kuridhisha			Hati zenyeshaka			Hati zisizoridhisha			Hati chafu			Jumla		
	FY 2009/ 2010	2010/ 2011	2011/ 2012	2009/ 2010	2010/ 2011	2011/ 2012	2009/ 2010	2010/ 2011	2011/ 2012	2009/ 2010	2010/ 2011	2011/ 2012	2009/ 2010	2010/ 2011	2011/ 2012
MDAs	43	50	87	13	10	6	1	0	0	-	-	0	57	60	93
RAS	12	19	21	7	2	0	1	0	0	1	-	0	21	21	21
Total	55	69	108	20	12	6	2	0	0	1	-	0	78	81	114
%age	71	85	94.7	26	15	5.3	2	0	0	1	0	0	100	100	100

Jedwali linaonyesha kwamba hati za kuridhisha zimeongezeka kutoka asilimia 85 mwaka 2010/2011 hadi asilimia 94.7 mwaka 2011/2012. Pia, hati zenye shaka zimepungua kutoka asilimia 15 mwaka 2010/2011 hadi asilimia 5.3 mwaka 2011/2012. Matokeo ya ukaguzi kwa mwaka huu yamebaini kutokuwepo kwa hati isiyoridhisha. Aidha, kama ilivyokuwa kwa mwaka 2010/2011, matokeo ya ukaguzi kwa mwaka huu yanaonyesha kutokuwepo kwa hati mbaya. Mwelekeo huu wa hati unaonyesha kuboreka kwa usimamizi wa fedha na rasilimali nyingine za Umma.

3: Dosari kuu zilizojitokeza wakati wa ukaguzi

Wakati wa ukaguzi wa mwaka huu tumeendelea kukutana na dosari mbalimbali ambazo maelezo ya kina yametolewa katika sura husika. Dosari hizo ni pamoja na kutofuatwa sheria mbalimbali, kutokuwepo kwa mifumo ya udhibiti ya ndani madhubuti, aidha kama mifumo ipo kutozingatiwa kwa mifumo hiyo. Masuala muhimu yanayohusiana na dosari hizo ambayo yako katika taarifa yangu ni haya yafuatayo:

- Kutofuatwa kikamilifu kwa Viwango vya Kimataifa vya Uhaisibu katika sekta ya Umma (IPSAS)
- Kutofuatwa kikamilifu kwa Sheria ya Manunuzi ya Umma ya mwaka 2004 na kanuni zake za 2005
- Kutotekeleza mapendekezo yangu ya ukaguzi niliyoyatoa katika miaka iliyopita.
- Wizara ya Nishati na Madini kutokutoa taarifa ya maduhuli yasiyokusanywa yanayofikia Shs. 1,645,582,899
- Malipo ya madeni ya Wizara ya Miundombinu kwa mwaka 2010/11 kulipwa kwa kutumia fedha zilizoidhinishwa kwa ajili ya ujenzi wa barabara kwa mwaka 2011/12 Shs. 252,975,000,000
- Maduhuli yatokanayo na mirahaba ambayo haikukusanywa inayofikia Dola za Kimarekani 12,634,354 sawa na Shs. 19,709,593,191
- Madeni ya Shirika la Ndege la Tanzania (ATCL) ya jumla ya Dola za Kimarekani 41,466,177.16 yalikuwa hayajalipwa hadi kufikia mwisho wa mwaka wa fedha 2011/12
- Malipoyamatibabu nje ya nchi ya jumla ya Sh.

448,144,343yalifanywabila nyarakaza kutoshakuthibitishauhalaliwake.

- Masurufu ya jumla ya Shs.706,701,016.36 yalikuwa hayajarejeshwa hadi kufikia mwisho wa mwaka wa fedha 2011/12.
- Malipo ya jumla ya Shs. 6,027,429,643 yalifanywa kutoka katika vifungu visivystahili na hivyo kuathiri majukumu yaliyokasimiwa fedha hizo
- Malipo ya uzeeni na mikataba kwa wastaa fu kufanywa mara mbili kinyume na sheria za pensheni.
- Deni la Taifa limeongezeka kwa Sh.2,064,860,281,962.80 (sawa na asilimia 17.6%) kutoka Sh. 14,441,617,939,770.20 mwaka 2010/2011 hadi Sh.16,975,962,626,745.20 mwaka 2011/2012. Sababu za ongezeko la deni hilo zimeelezwa katika sura ya sita.
- Kiasi chaSh.432,443,000,129 kilionyeshwakatika Hesabu Jumuifu za Taifakikiwa ni madeni yasiyolipwahadi kufikia tarehe 30 Juni, 2012. Kiasi hiki kinawakilishakupungua kwa asilimia25.12% ikilinganishwa nakiwangochamwakauliopitacha Sh. 577,537,084,848.

4: Dosari zilizobainika katika mchakato wa manunuizi

Kama ilivyokuwa kwa ukaguzi wa miaka iliyopita, dosari kuu zilizojitokeza mwaka huu zinafanana na za miaka iliyopita. Mifano michache ya dosari hizo inatolewa kwa muhtasati hapa chini na maelezo zaidi katika sura ya 5 ya taarifa hii.

Kutozingatiwa kwa utaratibu wa kuanzishwa vitengo vya manunuizi

Uzingativu katika uanzishwaji wa vitengo vya manunuizi na kuwepo kwa uwiano mzuri wa wataalam wenye sifa stahiki ilikuwa ni wastani wa 78% ikilinganishwa na 56% kwa mwaka 2010/11 kwa Wizara, Idara na Wakala za Serikali.

Utayarishaji usiokuwa sahihi wa mipango ya mwaka ya manunuzi

Taasisi nyingi za manunuzi zilizokaguliwa zilionekana kutofuata matakwa ya utayarishaji wa mipango ya mwaka ya manunuzi licha ya umuhimu wa mipango hiyo katika kuzisaidia taasisi husika: kuepuka manunuzi ya dharura; kunufaika na punguzo la bei na kupungua kwa gharama za manunuzi kutokana na kujumuisha manunuzi kwa pamoja; kutumia mikataba inayozingatia matakwa ya taasisi za manunuzi pale inapowezekana ili kuleta ufanisi, unafuu wa bei na uhuru katika zabuni za ujenzi, huduma au mali pale ambapo mahitaji ya vitu hivyo ni ya mara kwa mara au yanajirudia rudia katika kipindi fulani; kuepuka kugawanya manunuzi kwa kutumia njia sahihi ya manunuzi; na kupanga vyema vikao vya kamati za zabuni ili kupunguza gharama za manunuzi pale yanapofanyika kidogo kidogo.

Wastani wa kitaifa wa uzingativu wa utayarishaji na utekelezaji wa mipango ya mwaka ya manunuzi ilikuwa asilimia 58. Kiwango cha uzingativu kwa Wizara, Idara na Wakala za Serikali peke yake kilifiki 68% kwa mwaka 2011/12 (54% kwa mwaka 2010/2011).

Usimamizi dhaifu wa mikataba

Kama ilivyokuwa kwa ukaguzi wa miaka iliyopita, kasoro zifuatazo zilionekana wakati wa kutathmini masuala yahusuyo usimamizi wa mikataba: Baadhi ya mikataba haikuwa na nyaraka muhimu wakati mikataba mingine ilikuwa na nyaraka zisizohusiana na mikataba hiyo; Dhamana ya utekelezaji wa mikataba haikuwepo kama kinga endapo ingetokea kasoro katika utekelezaji; Uhakikisho wa ubora haukutolewa endapo mali zisizo na ubora zingenunuliwa; Fidia itokanayo na kuchelewa kutekeleza mikataba haikutozwa; Vikao katika maeneo mengi inakotekelezwa miradi havikufanyika; hapakuwa na mipango toshelevu ya kutoa uhakikisho wa mikakati ya ubora, kazi zilizokamilika hazikufanyiwa majaribio ili kuona kama zimefikia vigezo vilivyowekwa katika mikataba; Taarifa za utekelezaji wa miradi ya ujenzi hazikutayarishwa; Taarifa za usimamizi hazikutayarishwa; Ongezeko la muda wa utekelezaji miradi

pasipo kuwepo sababu za msingi na bila kufuata utaratibu; Hati za kuruhusu malipo kufanywa hazikuwa na viambatisho vinavyoonyesha vipimo na jinsi ukokotoaji ulivyofanyika kufikia kiasi cha fedha kinachotakia kulipwa; na Kamati za kupokea na kukagua mali hazikuteuliwa ili kubaini kiasi na ubora wa mali iliyopokelewa.

Matokeo ya ukaguzi yanaonyesha kiwango cha uzingativu cha 55% na 71% kwa udhibiti wa ubora na usimamizi wa mikataba. Kiwango cha wastani cha uzingativu kwa Wizara, Idara na Wakala kilikuwa 56% kwa udhibiti wa ubora na 72% kwa usimamizi wa mikataba (64% na 41% kwa mwaka 2010/11).

5: Masuala ya Kodi

Matokeo ya ukaguzi wa Mamlaka ya Mapato Tanzania yamejumuishwa katika Hesabu Jumuifu za Taifa katika Sura ya 3 ya taarifa hii. Mambo muhimu yaliyojitezea kuhusiana na ukusanyaji wa kodi ni kama ifuatavyo:

- Kumekuwepo na masuala ya taarifa za ukaguzi za miaka ya nyuma ambayo hayajashughulikiwa yenyе thamani ya kiasi cha Sh.545,273,124,808 na Dola za Kimarekani 105,036,380.
- Hesabu za Mamlaka ya Mapato Tanzania Bara zimeonyesha makusanyo ya kiasi cha Sh.6,703,229,704,887 ikilinganishwa na makadirio ya Sh.6,456,832,630,000 na kusababisha makusanyo ya ziada ya Sh. 246,397,074,887 sawa na asilimia nne (4%) ya makadirio.
- Mwelekeo wa misamaha ya kodi unaonyesha ongezeko la misamaha kwa kiasi cha Sh.789,883,259,827 sawa na 78% kutoka kiasi cha Sh.1,016,320,300,000 kilichoripotiwa mwaka 2010/2011 hadi Sh.1,806,203,559,827 kwa mwaka 2011/2012.
- Katika hali halisi, kama kiasi cha Sh. 1,806,203,559,827 ambacho ni sawa na asilimia 27 ya makusanyo yote kisingesamehewa, makusanyo ya ziada ya Sh. 246,397,074,887

yaliyopotiwa na TRA yangeongezeka hadi kufikia Sh. 2,052,600,634,714.

Kwa ujumla, misamaha kwa upande wa Tanzania Bara imeongezeka katika mwaka 2011/12 ikilinganishwa na miaka iliyopita ambapo athari zake ni upungufu wa mapato yatokanayo na kodi kama inavyoonekana hapa chini:

Jedwali Na. 2: Mwelekeo wa misamaha ya kodi

Maelezo	2011/2012	2010/2011
Makusanyo halisi	6,703,229,704,887	5,550,205,244,378
Misamaha	1,806,203,559,827	1,016,320,300,000
Misamaha ya kodi kama sehemu ya makusanyo	27%	18%
Pungufu/ (ziada ya makusanyo)	246,397,074,887	(298,888,455,622)
ziada endapo misamaha isingetolewa	2,052,600,634,714	717,431,844,378

Kwa upande wa Hesabu Jumuifu za Taifa, matokeo muhimu yalijumuisha masuala yafuatayo:

Jedwali Na. 3: Matokeo muhimu yatokanayo na Hesabu Jumuifu za Taifa

Maelezo	Kiasi (Sh.)
Matumizi ya Serikali kwa mwaka 2011/2012	12,061,571,308,295
Ongezeko la Deni la Taifa kwa 17.6%	2,064,860,281,962.80
Mihadi isiyolipwa	134,148,478,322
Madeni yasiyolipwa	432,443,000,129
Malimbikizo ya maduhuli yasiyokusanywa	98,774,320,855
Malimbikizo ya potevu za serikali	13,024,783,230

6: Masuala yahusuyo malipo ya mafao ya izeeni

Kwa vile udhibiti wangu unanitaka kufanya ukaguzi wa mafao ya wastaa fu, sura ya nne ya taarifa hii inaonyesha matokeo muhimu

ya ukaguzi wa awali niliyofanya katika kipindi husika. Ukaguzi ulibaini kwamba:

- Kiasi cha malipo kwa wastaa fu kingelipwa zaidi ya kile kinachostahili kwa Sh. 325,261,768.37 kama malipo hayo yasingehakikiwa.
- Wastaa fu wangepunjwa malipo ya kustaafu kwa kiasi cha Sh.258,915,380.69 kama madai yao hayangehakikiwa.

Matatizo makubwa yaliyojitokeza wakati wa ukaguzi wa mafao ya wastaa fu ni kama ifuatavyo:

- (i) Matatizo ya kiuendeshaji
- (ii) Kutoa tafsiri isiyokuwa sahihi ya sheria za pensheni, kanuni zake na sheria nyingine
- (iii) Matatizo ya kiutawala

Masuala muhimu yaliyojitokeza kutokana na ukaguzi huo ni haya yafuatayo:

- Malipo yenyeye shaka yahusuyo mishahara kwa ajira za mikataba na mafao ya uzeeni
- Kuzidi kwa muda unaotakiwa kukokotolea mafao ya uzeeni kwa maafisa wa jeshi na askari
- Kutotumia viwango sahihi katika ukokotoaji wa mafao ya wastaa fu.
- Kuchanganya masharti ya ajira za kudumu na za mikataba
- Kutozingatiwa kwa sheria za pensheni
- Ucheleweshaji wa kuwasilisha madai ya pensheni kwa ajili ya ukaguzi
- Kuwasilisha nyaraka zisizokamilika
- Utoaji maamuzi yenyeye utata (unaokinzana)

7: Mapendekezo

Mwisho, kwa mujibu wa madaraka niliyopewa chini ya Kifungu cha 10 cha Sheria ya Ukaguzi wa Umma Na.11 ya mwaka 2008, nimetoa mapendekezo kadhaa katika Sura ya 8 ya taarifa hii ambayo kama yatakelezwu yatasaidia kuimarisha usimamizi wa rasilimali za Umma katika nchi yetu. Mapendekezo hayo yanajumuisha:-

- Utekelezaji wa mapendekezo yangu ya miaka ya nyuma haujazingatiwa ipasavyo na serikali. Hivyo napendekeza utekelezaji wa mapendekezo hayo kwa wakati ili kuleta ufanisi na uwajibikaji.
- Nashauri Maafisa Masuuli wazingatie sheria pamoja na uandaaji wa taarifa mbalimbali ili kuweka uwazi na uwajibikaji ndani ya serikali.
- Serikali ijithabu kuepu kaungia katika mihadi huku ikijua fedha za kulipia hazipo.
- Kuimarishe mifumo ya udhibiti wa ndani na kuboresha nidhamu katika matumizi ya Serikali.
- Maafisa Masuuli waimarishe michakato ya manunuzi, ikiwa ni pamoja na kaungia na kusimamia mikataba yenye tija kwa kuzingatia sheria na kanuni za manunuzi ili kupata thamani ya fedha.
- Serikali iimarishe mfumo wa udhibiti wa ndani katika ukusanyaji wa mapato na kuhakikisha kuwa malimbikizo ya maduhuli yasiyokusanywa kwa miaka ya nyuma yanakusanywa
- Serikali ihakikishe kuwa mapato ya mrahaba ya kiasi cha Dola za Kimarekani 12,634,354.61 yaliyokusanywa pungufu kutokana na makampuni ya uchimbaji madini yanakusanywa na taarifa kutolewa.
- Maafisa Masuhuli wahakikishe kuwa masurufu ambayo muda wake wa kurejeshwa umepita yanakatwa kutoka katika mishahara ya waliopewa masurufu hayo.
- Maafisa Masuuli waepuke kuhamisha fedha kutoka katika vifungu vilivyokasimiwa pasipo kuomba na kupewa idhini ya kufanya hivyo na Hazina.
- Serikali iboreshe utaratibu za malipo ya mwisho ya wastaafu ili yalipwe haraka na kwa ufanisi.
- Serikali ifikirie namna ya kuachana na baadhi ya misamaha ya kodi na iboreshe utaratibu wa ndani wa kufuatilia na kuhakikisha kuwa misamaha ya kodi iliyokwishatolewa inatumwiwa kama ilivyokusudiwa na sio vinginevyo.

SURA YA 1

1.0 Utangulizi

Taarifa hii inatolewa kufuatia ukaguzi wa hesabu na kumbukumbu nyingine za Wizara, Idara, Wakala, Sekretarieti za Mikoa na Balozi kwa mujibu wa Ibara ya 143 (4) ya Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania ya mwaka 1977 (iliyorekebishwa 2005) na Kifungu cha 34(1) (c) cha Sheria ya Ukaguzi Na. 11 ya mwaka 2008 kwa mwaka ulioishia tarehe 30 Juni, 2012.

1.1 Ukaguzi wa Taarifa za Hesabu za Umma

Kutokana na Ibara ya 143 ya Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, ninapaswa kukagua kumbukumbu za taarifa zote za hesabu za fedha katika Ofisi zote za Umma, Mahakama na Mamlaka zote za Serikali ya Muungano wa Tanzania na kutoa taarifa kwa Mheshimiwa Rais ambaye atahakikisha zinawasilishwa mbele ya Bunge.

Katika kutimiza wajibu huu, kutokana na Kifungu Na. 10 cha Sheria Na 11 ya Ukaguzi wa Umma ya mwaka 2008, ninatakiwa kujiridhisha kwamba:-

- Tahadhari inachukuliwa ili kuhakikisha kwamba fedha za Umma zinakusanywa na kutunzwa kwa mujibu wa sheria na miongozo iliyowekwa.
- Fedha zote kutoka Mfuko Mkuu wa Serikali zimeidhinishwa na kutolewa kufuatana na Sheria ya Matumizi ya Bunge ya mwaka husika.
- fedha zote zimetolewa chini ya mamlaka sahihi na kuwa zimetumika kwa madhumuni yaliyokusudiwa na mamlaka hiyo na, kanuni zipo za kutosha kwa ajili ya kuwaongoza watunza vifaa namna ya kuweka vitabu sahihi. Aidha, nina wajibu, kwa mujibu wa kifungu hicho cha sheria

kumjulisha Rais na Bunge juu ya uwepo wa matumizi mabaya ya fedha na mali za Umma.

1.2 Majukumu na wajibu wa Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali kwa Wizara, Idara, Wakala na Sekretarieti za Mikoa

Wajibu wa kisheria wa Ofisi yangu katika kukagua hesabu za Wizara, Idara, Wakala na Sekretarieti za Mikoa umebainishwa chini ya Kifungu cha 10 (1) cha Sheria ya Ukaguzi wa Umma Na. 11 ya mwaka 2008. Kutokana na Sheria hiyo, ninawajibika kuchunguza, kukagua na kutoa taarifa juu ya hesabu za Wizara na Idara za Serikali na Maafisa Masuuli, na watu wote waliokabidhiwa jukumu la kukusanya, kupokea, kutunza, kutoa au kuuza, kuhamisha na kutoa stakabadhi, dhamana, vifaa au mali nyingine za Umma. Pia, jukumu langu linahusu Mashirika yote ya Umma na Taasisi nyingine, Mamlaka yoyote au Taasisi inayopokea fedha kutoka Mfuko Mkuu wa Serikali, au Taasisi yoyote ambayo imeruhusiwa kisheria kukaguliwa na Ofisi yangu.

1.3 Muundo wa Kazi za Ukaguzi Ndani ya Ofisi ya Taifa ya Ukaguzi

Taarifa hii inatoa kwa muhtasari matokeo ya mwisho ya zoezi la ukaguzi ambalo lilifanywa na Ofisi yangu nchini kote kwa kipindi cha mwaka unaoishia tarehe 30 Juni, 2012. Ili ofisi yangu iweze kushughulikia kwa ufanisi zaidi kazi hii kubwa ya kukagua Wizara zote, Wakala na Sekretarieti za Mikoa nchini, nimeweka ofisi katika kila Wizara na Mikoa ya Tanzania Bara kwa madhumuni ya usimamizi mzuri wa kazi.

Ofisi hizi za Mikoa na Wizara zinasimamiwa na Wakaguzi wa Hesabu Wakazi ambao tangu Mei, 2012 wanawajibika kwa Wasaidizi wa Mkaguzi Mkuu wa Hesabu.

Imeonekana kuwa ni vyema kugawa wakaguliwa wetu katika Kanda ambazo zinaongozwa na Wasaidizi wa Mkaguzi Mkuu wa Hesabu ili kurahisisha usimamizi wa kaguzi zinazofanywa chini

yao. Ili kuhakikisha ufanisi katika ukaguzi, wizara na taasisi zimegawanywa katika Kanda 11, na kila kanda inaongozwa na Msaидиzi wa Mkaguzi Mkuu wa Hesabu.

Ukaguzi wa Taasisi za Umoja wa Mataifa

Mwezi Disemba mwaka 2011, Mkutano Mkuu Maalumu wa Umoja wa Mataifa uliiteua Ofisi ya Taifa ya Ukaguzi ya Tanzania kujiunga na Bodi ya Ukaguzi wa Hesabu ya Umoja huo (United Nations Board of Auditors - UNBoA) kujaza nafasi itakayoachwa wazi wakati Afrika ya Kusini itakapomaliza muda wake tarehe 30 Juni , 2012.

Tanzania kama mwanachama wa UNBoA imeshaanza ukaguzi wa miradi na taasisi za Umoja wa Mataifa duniani kote tangu mwezi Julai mwaka 2012.Kaguzi za awali zimekamilika na taarifa zinazohusu shughuli na taasisi zifuatazo zimewasilishwa UNBoA kwa hatua za kiutawala: Operesheni za kulinda amani (Somalia, Liberia, DRC and Haiti), Shirika la Umoja wa Mataifa linaloshughulikia masuala ya Makazi (UN Habitat), Programu ya Umoja wa Mataifa inayoshughulikia Mazingira (UNEP), Ofisi ya Umoja wa Mataifa iliyoko Nairobi Nairobi (UNON), Programu ya Maendeleo ya Umoja wa Mataifa (UNDP), Mfuko wa Umoja wa Mataifa unaoshughulikia Idadi ya Watu (UNFPA) Shirika la Umoja wa Mataifa linaloshughulokia masuala ya Wanawake (UN Women), Shirika la Misaada kwa Wakimbizi kwa Wapalestina Ukanda wa Gaza (UNRWA), Mahakama ya Kimataifa ya Mauaji ya Rwanda (1994) (ICTR) na Mahakama ya Kimataifa ya uhalifu wa kivita ya Yugoslavia ya Zamani (ICTY).

Ningependa kuwapongeza watumishi wa ofisi yangu kwa kufanya kazi kwa masaa mengi ili kuhakikisha kuwa kaguzi hizi za Umoja wa Mataifa zinakamilika licha ya majukumu mengine ya ukaguzi wa hapa nchini yanayowakabili.

1.4 Mawanda na viwango vya Ukaguzi vinavyotumika

1.4.1 Mawanda ya ukaguzi

Mawanda ya ukaguzi kwa kifupi yanahusisha ukusanyaji wa maduhuli, uidhinishaji wa matumizi kwa kufuata sheria ya Bunge, utekelezaji wa miradi, utendaji wa Hazina na Mamlaka ya Mapato Tanzania.

Ukaguzi ulifanyika ili kujiridhisha kwamba kulikuwepo na uzingatiaji wa kanuni zilizopo, kuongeza ufanisi na kupunguza gharama za uendeshaji na kubainisha baadhi ya kasoro zilizojitokeza, kupitia ripoti mbalimbali.

Wakati wa ukaguzi, hoja zote zilizojitokeza ziliwasilishwa kwa menejimenti za Wizara, Mikoa na Miradi iliyokuwa inakaguliwa kwa ajili ya kutolea maelezo. Maafisa Masuuli wanapewa fursa ya kuzitolea ufanuzi hoja na mapendekezo ya ukaguzi kabla ya kuingizwa kwenye ripoti.

1.4.2 Viwango vya Ukaguzi vinavyotumika

Ofisi ya Taifa ya Ukaguzi ni mwanachama wa Shirika la Kimataifa la Taasisi Kuu za Ukaguzi (INTOSAI) na Shirika la Taasisi Kuu za Ukaguzi Kanda ya Afrika kwa nchi zinazoongea kингereza (AFROSAI-E). Hivyo basi inatumia viwango vya ukaguzi vinavyotolewa na Shirika la Kimataifa la Taasisi Kuu za Ukaguzi (ISSAI) na vile vinavyotolewa na Shirikisho la Kimataifa la Wahasibu (IFAC) ambalo Tanzania ni mwanachama kupitia Bodi ya Taifa ya Wahasibu na Wakaguzi wa Hesabu. Pia ninayo furaha kueleza kwamba Tanzania (kupitia kwa Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu) kwa sasa ndiye Mwenyekiti wa AFROSAI-E kuanzia Aprili 2011 kwa kipindi cha miaka mitatu. AFROSAI-E inajumuisha wanachama kutoka nchi 24 za Afrika.

1.5 Sera ya Kiuhasibu

Kwa mujibu wa Kanuni ya 53 ya Kanuni za Fedha za Umma za mwaka 2001 (zilizorekebishwa 2004), Serikali imewe ka taratibu za kihasibu ili kuhakikisha kwamba rasilimali zinazoidhinishwa na Bunge zinatumika kwa usahihi. Kwa mujibu wa Sheria ya Fedha za Umma Na.6 ya mwaka 2001

(iliyorekebishwa 2004), Maafisa Masuuli wanapaswa kuhakikisha kwamba mapato yote ya Umma yanaingizwa kwenye Mfuko Mkuu wa Serikali. Pia malipo kutoka kwenye Mfuko huo yataidhinishwa kwa Sheria ya Bunge ya Matumizi kwa mwaka husika.

Huu ni mwaka wa nne tangu serikali ianze kuandaa Taarifa za Fedha kwa kuzingatia Viwango vya Kimataifa vya kihasibu katika Sekta ya Umma kwa mising ya fedha taslimu [(IPSAS) - cash basis of accounting]. Chini ya msingi huu mapato ya Serikali hayatambuliwi mpaka zitakapopokelewa fedha taslimu. Hali kadhalika matumizi hutambulika pale tu malipo yanapofanyika.

Kifungu cha 25(i) hadi (j) cha Sheria ya Fedha za Umma ya mwaka 2001 (iliyorekebishwa 2004) inatoa ufanuzi wa wa hesabu na taarifa zinazotakiwa kuandaliwa na Maafisa Wahasibu na kuwasilishwa kwa Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali kwa ajili ya ukaguzi.

1.6 Wajibu wa Kisheria wa Wizara, Idara, Wakala na Sekretarieti za Mikoa

Maafisa Masuuli wa Wizara, Idara na Sekretareti za Mikoa wana majukumu ya kusimamia rasilimali za Umma kwenye maeneo yao ya kazi. Kazi na majukumu ya Maafisa Masuuli kama ilivyoainishwa chini ya kifungu Na 8 cha Sheria ya Fedha za Umma Na. 6 ya mwaka 2001 (iliyorekebishwa 2004) ni kuwajibika na kulinda mali za umma zilizoko chini ya maeneo yao. Katika kulinda rasilimali zilizoko chini yao, ni muhimu kwa Maafisa Masuuli kuhakikisha kwamba kunakuwepo na mifumo ya udhibiti wa ndani madhubuti na inayofuatwa muda wote kufanya kazi.

1.7 Mfumo wa Udhibiti wa Ndani

Udhibiti wa ndani unalenga jinsi rasilimali za Serikali zinavyoelekezwa, kusimamiwa na kupimwa. Kwa maana nyingi mfumo mzuri wa udhibiti wa ndani unayo nafasi kubwa katika kuzuia na kugundua ubadhirifu/matumizi mabaya na kulinda rasilimali za Umma zinazogusika na zisizogusika.

Uwekaji wa mfumo wa ndani madhubuti ni muhimu na niwajibu wa menejimenti ya taasisi husika.

1.8 Kutayarisha na kuwasilisha taarifa za fedha kwa ajili ya ukaguzi

Jukumu la kutayarisha na kuwasilisha hesabu za mwaka kwa Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali ni wajibu wa Maafisa Masuuli wa Serikali Kuu (Wizara, Idara, Wakala na Sekretarieti za Mikoa). Kifungu cha 25 cha Sheria ya Fedha za Umma ya mwaka 2001 (iliyorekebishwa mwaka 2004); inataja aina ya hesabu mbalimbali anazotakiwa kutengeneza Mhasibu Mkuu wa Serikali, Maafisa Masuuli na Maafisa wengine wa Serikali waliokasimiwa Mifuko Maalumu iliyoanzishwa kisheria. Pia, Kifungu cha 25(4) cha sheria hiyo hiyo kinataka taarifa za fedha ziandaliwe kulingana na mifumo ya kihasibu iliyokubalika kimataifa na ni lazima misingi ya kihasibu iliyotumika iwekwe bayana. Kwa mwaka wa pili katika historia, taarifa za fedha za Wizara, Idara, Sekretarieti za Mikoa zimeandaliwa kwa kuzingatia Viwango vya Kimataifa vya kutayarisha taarifa za fedha katika sekta ya Umma ambayo inalandana na matakwa ya kanuni Na. 53 ya Kanuni za Fedha za mwaka 2001 (zilizorekebishwa 2004). Aidha, utaratibu huo umeanza katika Balozi kwa mara ya kwanza mwaka huu wa fedha.

Kanuni ya 8 (5) ya Kanuni za Fedha za Umma za mwaka 2001 (zilizorekebishwa 2004) inataka kila Wizara, Idara na Sekretarieti za Mikoa kutengeneza na kutoa kwa Umma taarifa ya utekelezaji ya mwaka inayoeleza mikakati ya bajeti, aina na malengo ya kila mpango/programu, tathmini ya matokeo na mafanikio yakilinganishwa na malengo yaliyowekwa. Pia, Maafisa Masuuli wanatakiwa kutengeneza muhtasari wa matokeo ya matumizi ya fedha, kwa mwaka wa fedha unaohusika na kwa mfumo ulioidhinishwa na Mhasibu Mkuu wa Serikali, mipango ya mwaka ujao kama ilivyoidhinishwa na Bunge na mipango ya muda wa miaka miwili inayofuata. Baadhi ya Wizara, Idara na Sekretarieti za Mikoa hazikutimiza wajibu huu.

SURA YA 2

MAPITIO YA UTEKELEZAJI WA MAPENDEKEZO YATOKANAYO NA HOJA ZA UKAGUZI KWA MIAKA ILIYOPITA

2.0 Utangulizi

Sura hii inaonyesha matokeo ya tathmini iliyofanyika katika kipindi cha ukaguzi na ni jinsi gani Serikali imetekeleza mapendekezo yatokanayo na hoja za ukaguzi kwa miaka iliyopita yaliyotolewa na Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali kupitia ripoti jumuifu kwa Wizara, Idara zinazojitegemea na Sekretarieti za Mikoa.

Matokeo ya tathminiyalikuwa katika maeneo yafuatayo:

- i. Majibu kutoka kwa Mlipaji Mkuu wa Serikali (PMG) yaliyowasilishwa katika ripoti jumuifu ya Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali.
- ii. Majibu ya taarifa za kila fungu kutoka kwa Afisa Masuuli /Wakuu wa vitengo yaliyowasilishwa kwa Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali.
- iii. Majibu ya taarifa za Mamlaka ya Mapato Tanzania (TRA) yaliyowasilishwa kwenye ripoti jumuifu ya Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali
- iv. Majibu ya hoja zitokanazo na ukaguzi wa taarifa jumuifu za hesabu za Serikali.

2.1 Ufuatiliaji wa majibu ya Mlipaji Mkuu wa Serikali (PMG) yaliyowasilishwa kwa Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali kuhusu ripoti za Serikali Kuu kwa miaka ya nyuma.

- (a) Mapendekezo mengi yaliyotolewa katika ripoti ya Serikali Kuu kwa miaka ya nyuma(2008/09, 2009/10 na 2010/11).Hata hivyo kwa baadhi ya mapendekezo

yaliyotolewa hakukuwa na ushahidi wa wazi wa kuthibitisha hatua zilizochukuliwa kutohana na majibu yaliyotolewa na Serikali. Mapendekezo ambayo yalilenga kuboresha masuala ya miaka ya nyuma na hali ilivyo sasa wakati wa kuandika taarifa hii (Februari,2013) ni kama inavyoonyesha katika jedwali hapa chini:

Jedwali Na. 4:Maoni ya majibu yaliyoandalika na Serikali kwa mapendekezo ya kaguzi za miaka ya nyuma.

Na	Mapendekezo ya ukaguzi	Majibu ya Mlipaji Mkuu wa Serikali (PMG)	Maoni ya ukaguzi
1	Kutokufuatwa kikamilifu kwa Viwango vya Kimataifa vya Uhasibu Katika Sekta ya Umma (IPSAS)	<ul style="list-style-type: none"> • Kuhakikisha utekelezaji wa Viwango vya Kimataifa vya Uhasibu katika Sekta ya Umma (IPSAS) kwa ufanisi, Serikali imefanya mafunzo kwa wadau mbalimbali kama vile Kamati ya Hesabu za Serikali (PAC), Wahasibu Wakuu, Wahasibu, na waingizaji wa takwimu kutoka Wizara, Mikoa pamoja na wahasibu kutoka ofisi za Balozi. • Serikali ipo katika mchakato wa kuandaa muongozo wa uhasibu na sera za uhasibu ambazo zitatumika kama muongozo juu ya utekelezaji wa Viwango vya Kimataifa vya Uhasibu katika Sekta ya Umma (IPSAS) • Serikali ipo katika mchakato wa kuanzisha rejista ya mali za 	<ul style="list-style-type: none"> • Maendeleo ya utekelezaji wa kuhamia mfumo wa Viwango vya Kimataifa vya Uhasibu katika Sekta ya Umma utafanyiwa tathmini wakati wa ukaguzi wa mwaka ujao. • Serikali inatakiwa kuandaa na kuwasilisha rejista ya mali za kudumu kwa ajili ya uhakiki.

		kudumu katika Wizara, Sekretarieti za mikoa, Idara za Serikali na Wakala wa Serikali zipatazo 36 zimekwisha fanyiwa tathmini za mali za kudumu kwa ajili ya kutengeneza rejista kuu ya mali za kudumu za Serikali.	
2.	Kutofuatwa kikamilifu kwa Sheria ya Manunuzi ya Umma ya mwaka 2004 na kanuni zake za 2005	<ul style="list-style-type: none"> • Kuna hatua mbalimbali zimechukuliwa na Serikali kuhakikisha kuwa wadau wa manunuzi wanazingatia sheria za manunuzi na kanuni zake. Hatua hizo ni: 1.Kutungwa kwa sheria mpya ya manunuzi ya mwaka 2011. • Uundaji wa vitengo vya usimamizi wa manunuzi katika taasisi mbalimbali. • Kujenga uwezo kwa wafanyakazi wa vitengo vya manunuzi ili kuongeza ufahamu na uelewa kuhusu sheria na kanuni zinazohusika na manunuzi. • Kufanya tathmini ya mahitaji ya mafunzo kwa kutambua maeneo ambayo yanahitaji kuboreshwa. 	Serikali lazima ionyeshe ratiba ya utekelezaji, kwa mfano, ni wakati gani sheria mpya ya manunuzi ya mwaka 2011 itaanza kufanya kazi kwa ufanisi.
3	Mapitio ya mpango wa kubakiza maduhuli	Serikali itaendelea kuhakikisha kwamba mpango wa kubakiza maduhuli yaliyokusanywa, unazingatiwa na	Mlipaji Mkuu wa Serikali hakuonyesha katika jibu lake kama viwango vipya vya kubakiza maduhuli vimerekebishwa kama

		<p>kusimamiwa vizuri. Makusanyo ya ziada katika Balozi yatarejeshwa katika Mfuko Mkuu wa Serikali.</p> <p>Maafisa Masuuli wamekuwa wakikumbushwa kila mwisho wa mwaka wa fedha kuzingatia mpango wa kubakiza maduhuli kupitia Waraka wa Hazina.</p>	iliyoshauriwa.
4	Usimamiaji mbovu wa mali za Serikali	<p>Serikali imeona mapungufu katika suala la matengenezo ya mashine za kutolea viza.</p> <p>Kwa sasa Serikali inaandaa zabuni mpya ambayo pia itahusisha matengenezo ya mashine ya kutolea viza. Aidha, itajenga uwezo kwa watumiaji wa mashine za kutolea viza katika mwaka wa fedha 2012/2013.</p>	Serikali haijaweka wazi ni lini mashine za kutolea viza zitaanza kutumika kwa ufanisi ili kupata thamani ya fedha.
5	Kuboresha kanuni za utumishi za mwaka 1979 kwa wafanya kazi wa mambo ya nchi za nje.	Kanuni za utumishi za wafanyakazi wa mambo ya ya nchi za nje ya mwaka 1979 imefanyiwa mapitio katika ngazi ya menejimenti na kupelekwa katika Ofisi ya Rais, Menejimenti ya Utumishi wa Umma kwa ajili ya mapitio na kibali.	Majibu ya Serikali yamepokelewa. Matokeo ya kuboresha kanuni yatapitiwa katika kipindi cha ukaguzi ujao.
6	Umiliki wa ardhi na majengo ya ofisi za Balozi za Tanzania nchi za nje.	<p>Katika kuboresha utendaji katika Balozi, Serikali imeanza kununua ardhi na majengo kwa baadhi ya Balozi ili kupunguza gharama za uendeshaji. Hati miliki za ardhi na majengo yalijonunuliwa ni kama ifuatavyo:</p> <ol style="list-style-type: none"> 1. Kilimanjaro Court - 	Serikali katika majibu yake haijatamka wazi kama hati miliki ya ardhi na majengo yanayomilikiwa na Kamisheni ya Balozi ya Uingereza imetolewa au bado.

		<p>awali lilijulikana kama "Air Tanzania building" - LR. 2/472.</p> <p>2. Muthaigha Residential - LR 214/514.</p> <p>3. New Chancery - LR 209/13678.</p> <p>4. Tanzania Embassies/Mission - Maputo (Plot No 141B Registered under No 57,442 - G 59</p>	
7	Masuala ya Kodi: Hatua zilizo chukuliwa kutatua rufaa za kodi	Ili kuhakikisha kuwa masuala yote ya rufaa za kodi yanashughulikiwa ipasavyo na kukamilika menejimenti ya TRA imeandika barua kwa Mwanasheria Mkuu wa Serikali kutafuta namna ya kutatua kesi zilizopo.	Zaidi ya miezi 12 imepita bila kupata majibu ya barua iliyowasilishwa kwa Mwanasheria Mkuu wa Serikali. Kuna haja ya Serikali kufuutilia kwa Mwanasheria Mkuu ili kuhitimisha suala hili.
8	Malipo ya matengenezo ya magari bila kibali cha TEMESA Sh.176,722,089	Serikali inakiri makosa ya kutengeneza magari bila kibali cha TEMESA. Maafisa Masuuli wamekuwa wakikumbushwa kuzingatia kanuni ya 59 ya PPA, 2004. Hata hivyo, utafiti umebaini kwamba katika baadhi ya Mikoa ofisi za TEMESA hazina uwezo wa kutosha wa kushughulikia matengenezo ya magari na mitambo.	Bado inasisitizwa kwamba hata kama TEMESA haina uwezo wa kutosha wa kushughulikia matengenezo, idhini ya kutengeneza magari katika gereji nyingine lazima itolewe na TEMESA kama ilivyoelekezwa katika kanuni ya 59 ya PPA, 2004
9	Malipo ya Posho ya samani kwa maofisa wasiostahili Sh.650,714,800	Ni kweli kuwa Wizara, Idara na Mikoa hazikuzingatia waraka wa Utumishi Na. C/CA/134/213/01/G/69 wa tarehe 30 Januari, 2006 ambao umeweka mipaka ya kulipa posho ya samani kwa maofisa wanaostahili ambao wanaishi katika nyumba za Serikali kama yatakuwepo.	Marekebisho ya waraka wa malipo ya posho ya samani yawasilishwe kwa Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali kwa ajili ya mapitio na maoni kama yatakuwepo.

		<p>ilivyoshauriwa na Mdhiliti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali. Jambo hili lilijadiliwa kwa kina katika mukutano wa Makatibu wakuu uliofanyika tarehe 13 Oktoba, 2011 na iliamuliwa marekebisho ya Waraka na.C/CA/134/213/01/G/69 yafanyike.</p> <p>Ofisi ya Rais Menejimenti ya Utumishi wa Umma imeandaa mapendekezo na inatarajiwa kwamba endapo idhini itapatikana suala hili litakuwa limetatuliwa.</p>	
10	Malipo yaliyofanyika kutoka katika vifungu visivyoohusika Sh.5,296,243,598	Ni kweli matumizi yamefanyika katika vifungu visivyoohusika kwa mujibu wa taarifa za fedha. Wizara, Mikoa na Wakala wamekumbushwa kuzingatia sheria ya fedha na kanuni zake kwa kuomba kibali cha kuhamisha fedha kati ya kifungu hadi kifungu ili kuondokana na makosa ya kufanya matumizi katika vifungu visivyoohusika.	Mdhiliti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali apewe taarifa za mawasiliano yaliyofanywa na Hazina kati ya Wizara na Mikoa kwa ajili ya ufuatiliaji.
11	Kuimarisha mfumo wa ndani wa ukusanyaji mapato	Ili kuimarishtamfumo wa ndani, Mamlaka ya Mapato Tanzaniakwa kutumia hudumayamshauri walT kuititia upyamifumo walT. Hivi sasa TRAinateskelezaprogramu ya ASYCUDA++(ASY-Bank). Hii ilianza kutekelezwa katika CitiBank, Bank Mna jitihada zinaendelea kufanyika kwa benki	Majibu ya Serikali yamepokelewa. Utekelezaji wa ufanisi wa mfumo mpya wa udhibiti utahakikiwa katika ukaguzi ujao.

		<p>nyingine.</p> <p>Kama hatua yamuda mrefu, TRAipo katika mchakato wakubadilishamifumo yake mikubwaya ukusanyaji mapato yaani ITAXmfumokwaKodiya Ndanina mfumo wa ASYCUDA++kwaushuru wa forodhakama mfumo mpyanawa kisasaili kukabiliana namabadiliko ya kiteknolojia.</p> <p>Aidha,TRApiainatekeleza mfumo wa ufuatiliaji na upakiaji ili kudhibiti mapato yanayopotea.Utekelezaji wamfumo mpyaunatarajiwakukamilik aOktoba 31, 2013.</p>	
12	Makusanyo pungufu ya mapato	<p>Serikali inatambua utendaji usioridhisha katika ukusanyaji wa mapato kwa muda wa miaka mitatu mfululizo. Sababu za utendaji usio ridhisha ni pamoja na:</p> <ol style="list-style-type: none"> 1. M dororo wa uchumi duniani ambao uliathiri pia nchi za Jumuia ya Afrika Mashariki. 2. Hali ya hewa mbaya iliyosababisha ukame wa muda mrefu iliathiri ukuaji wa uchumi na kusababisha njaa na upungufu wa mapato. 3. Uhaba wa umeme uliathiri uzalishaji viwandani na shughuli za biashara. 	<p>Majibu ya Serikali yamepokelewa. Hata hivyo bado kuna nafasi kwa ajili ya kuongeza mapato ya kodi kupidia njia mbalimbali, ikiwa ni pamoja na yafuatayo:</p> <ul style="list-style-type: none"> • Upanuzi wa wigo wa kodi kwa kuingiza sekta isiyo rasmi ili kukusanya kodi stahiki. • Kudhibiti ukwepaji wa kodi kwa kufanya tathimini ya kina kodi na usajili wa walipa kodi. • Mapitio ya viwango vya kodi vya sasa na msururu mrefu wa kodi ili kuhamasisha walipa kodi.

		<p>4. Athari juu ya mikataba iliyosainiwa kwa muungano wa kiuchumi, hasa SADC na EAC zimemesababisha bidhaa kutoka nchi hizi za muungano ziongezeke lakini zilitozwa ongezeko la thamani tu</p> <p>5. Changamoto ya ukaguzi wa mapato, hasa wakati wa kushughulika na makampuni ya kimataifa na sekta maalumu kama Mawasiliano na Madini. Licha ya mambo yaliyotajwa hapo juu, Serikali imechukua juhud ya kuhamasisha na kuimarisha sheria ya kodi na mikakati mingine ili kuboresha ukusanyaji wa mapato.</p>	<ul style="list-style-type: none"> Kudhibiti uhaba wa umeme kwa kuhakikisha upatikanaji wa umeme wa kuaminika na nafuu.
13	Hatua za kuboresha malengo ya ukusanyaji wa mapato kila mwaka	Serikali imechukua juhud ya kuhamasisha ulipaji kodi kwa hiari kwa njia ya elimu kwa walipa kodi, kuimarisha ukaguzi wa kodi za kampuni za kimataifa na sekta maalumu, kwa msaada kutoka taasisi ya usimamizi wa kodi ya Norway. TRA ina mchakato wa kuanzisha kitengo cha kodi cha kimataifa. Taasisi ya usimamizi wa kodi ya Norway itatoa mafunzo kwa wakaguzi wa kodi katika ukaguzi wa sekta ya madini na mafuta. Hatua nyingine ni pamoja na usimamizi na ufuatiliaji wa	Msisitizo unatolewa kuwa Serikali inapaswa kubuni mikakati kwa ajili ya kupambana na ukwepaji kodi, kupanua wigo wa kodi, kuingiza sekta isiyo rasmi ili kukusanya kodi stahiki na kuondokana na urasimu katika mfumo wa kodi uliopo sasa ili kuhamasisha ulipaji wa kodi kwa hiari.

		walipa kodi.	
14	Malipo yaliyofanywa bila nyaraka sahihi na pasipo maelezo ya kuthibitisha uhalali wa malipo husika	Maafisa Masuuli wameagizwa kuimarisha udhibiti wa mfumo wa ndani wa kuhifadhi nyaraka na kuzihakiki kabla ya kuwasilisha kwa wakaguzi.	Uhakiki wa utekelezaji wa suala hilo utafanyika wakati wa ukaguzi wa mwaka ujao. Hata hivyo ushauri unatolewa kwamba malipo yasiyo na viambatanisho yasiruhusiwe.
15	Bidhaa zilizonunuliwa na kulipwa kupokelewa bila	Serikali imekiri kuwepo kwa mapungufu na imeagiza Maafisa Masuuli wote ambao wamelipia bidhaa bila mapokezi wahakikishe kuwa vifaa vilivyoagizwa na kulipiwa vinapokelewa na kuingizwa kwenye daftari la vifaa. Vifaa vilivyoipiwa bila kupokelewa, baadhi vimekwisha pokelewa na vingine vinaendelea kupokelewa kwa awamu na vingine vitapokelewa baada ya kuongeza muda wa kulipa deni (letter of credit). Serikali imetoa wito kwa Maafisa Masuuli wote kufuutilia taarifa ya mapokezi ya vifaa kwa ajili ya udhibiti.	Ushahidi kuthibitisha upokeaji wa bidhaa uwasilishwe kwa ukaguzi ikiwa ni pamoja na kuhakikisha kwamba kumbukumbu za utunzaji wa vifaa unaimarishwa.
16	Malipo ya mishahara kwa watumishi ambao hawako kwenye utumishi wa umma	Serikali inatambua kuwepo kwa suala hilo na hatua zifuatazo zimechukuliwa: 1. Kuchambuanaku hakiki wafa nyakazi wotekatika Mamlakaza Serikali za mitaa, taasisi za elimu ya juu, Wakala na Mashirika ya Umma. 2. Hazinakwa kushirikiana na Ofisi ya Waziri Mkuu-PSM imefunga programu ya	Uhakiki wa utekelezaji wa suala hilo utafanyika wakati wa ukaguzi wa mwaka ujao. Hata hivyo, kuna haja ya kufanya ukaguziwa uchunguzijuu ya mishaharakwenye Wizara, Serikali za Mitaa, na Mikoaili kufichuaidadi halisi yawafanyakazi hewa, watu waliohusika na kiasi kulicholipwaili kuchukuliwahatua za marekebisho

	<p>Lawsonversion9katikaHalm ashaurizote, Mikoa, Wizara,Idara zinazojitegemea,Wakalana Taasisi za Serikaliambayoinawezesha Maafisa Masuulikufanya marekebishoya mishaharamuhimukamakuf utawafanyakaziambao hawapo kwenye utumishi wa ummanamabadililikoyamsha harakutokana nakupanda cheo, makato ya mishahara namahesabuya malimbikizoyawafanyakazi wao.</p> <p>3.Hazina ilifanya uhakiki wa wafanyakazi waliopo kazini</p> <p>4. Kati yaDisemba 2011naMachi 2012, jumla ya watumishi 9,215kutokaSerikali za Mitaa,692kutokaWakal a za Serikali na42kutoka Serikali Kuukwa mtiririko huowaligunduliwa kamawafanyakazi hewanakufutwa kutoka orodha ya mishahara,ukaguziwa aina hiyo utaendelezwa katika siku zijazo.</p> <p>5. Waraka wa Hazina Na.2 wa mwaka 2010 ulitolewa kwa mara nyingine kwa ajili ya kuwaongoza Maafisa Masuuli juu ya udhibiti wa mishahara.</p>	
--	---	--

Masuala yanayohusiana namafao ya wastaifu			
17	Madai mara mbili ya malipo ya uzeeni (pensheni na mafao ya mikataba) kinyume na sheria za pensheni	<p>Serikaliitatoa Waraka kwa taasisizinazoshughulika namaandalizi yamafaonawadau wengineikiwa ni pamoja naHuduma ya Walimu(TSD), Usalamawa Taifa (TISS), Jeshi la wananchi wa Tanzania(JWTZ), Sekretarieti zaTawala za Mikoa (RAS) naWizarakuhakikisha utekelezaji wamapendekezoya ukaguzi.</p> <p>Hazinakwa kushirikiana naOfisi ya RaisMenejimentiya Utumishi wa Ummaitatoamwongozo juu yamasualayamafao ya wastaifu.</p> <p>Katika mwaka wa2011/2012Serikaliilende sha mafunzojuu ya maandalizi yamafao yawadaumuhimu ambaonikatika Ofisi za Hazina Ndogo na Mahakama za Mwanzo. Mafunzoyalifanyikanchini koteikiwa ni pamoja naZanzibar.Piakatika mwaka wa fedha2012/2013Serikaliime pangakutoa mafunzo kwawadau zaidi, lengo</p>	<p>Majibu ya Serikali yamepokelewa. Hata hivyo, Waraka wa Hazina uwasilishwe kwa ajili ya uhakiki.</p>

		likiwa nikupunguzaudhaifuliopo	
18	Mapokezi ya fedha kwenye akaunti ya Amana kutoka NMB kwa ajili ya wastaafuhewa	<p>Wastaafuwotewanalipwape nshenizao kupitiaakaunti zaobinafsiza benki.Fedhailiyorejeshwa na benki zilikuwa za wastaafukutoka katika akaunti isiyotumika kwa muda mrefu (Idadi ambayohaikuwa katikaoperesheni kwakipindi fulanikwa mujibu wakanuniya benki). Hii hutokea kwa sababuwastaafuwanalipwa penshenikatikamuda wamiezisitaambayo ina maana kwambabaadhi ya wastaafuhuchukua fedha kila baada ya miezi sita.Hii haina maana kwambawastaafuhawapo,la kinihawakuwezakwendaben kimara kwa marakulingana na kanuni za benki.Hatua zilizochukuliwana Serikalinikama zifuatazo;</p> <ol style="list-style-type: none"> 1. PSPFinathibitishakumbuku mbu zawastaafu'mara mbili kwa mwaka, JanuarinaJulai. 2. Akaunti ya wastaafuinahakikiwa mara mojakilamwaka. 3. Tangu mwezi Januari,2012'wastaafu wanlipwabaada yakila miezi mitatuili kupunguzakiasi chafedha kutoka Serikalinikukaabilaa kutumikakatikamabenki. 	<p>Matokeo ya hatuazilizochukuliwa naserikaliyatafanyiwa tathminikatikaukaguziwa mwaka ujao. Aidha, ripoti ya uchanganuzi wa akaunti ya wastaafuinapaswakwasilish wa ukaguzi kwakwa ajili ya mapitio.</p>

		<p>4. Kiasi chote kisichochukuliwa kinarejeshwa Hazinana kuhifadhiwa katikaakaunti ya muda ya Amana ikisubirikuuhakikiwa.</p> <p>5. Serikali kupitiaWakalawake(PPF)im epangakufanya ukaguziwa wastaafunakufuta wastaafu wotewasiokuwepo.</p> <p>6. Zoezi la uchanganuzi ambalo bado linaendelea lina lengo la kuwa na kumbukumbu za wastaafu zitakazohifadhiwa kieletroniki kwa urahisi wa rejea.</p>	
19	Kutokuwa na stahili ya kulipwa pensheni	Serikali iliendelea kuhakiki Akaunti za Wastaafuambapo ukaguziuliofanyika mwezi waJuni/Julai, 2010/2011. Jumlaya akaunti124 za Wastaafuzilisitishwakwa ajili ya ukaguzizaidi.	Taarifa zote zauhakikiziwasilishweukagu zi kwa ajili ya mapitio.Pia, kuna haja ya kufanya ukaguziwauchunguzi ili kubainiukubwa wa tatizo.
20	Taarifa ya deni la Taifa	Uamuzi wa kukopa ndani au nje ya nchi unafikiwa baada ya kulinganisha gharama na faida itakayopatikana. Serikali hukopa nje ili kugharamia miradi ya maendeleo. Sehemu kubwa ya mikopo mikubwa ni ile yenye masharti nafuu ambapo asilimia 35 au zaidi ya aina hii ya mikopo huwa ni msaada kwa anayetoa na riba yake ni ya chini ya asilimia 1, na muda wa kuanza kulipa hurefushwa	Serikali haijaweka bayana ni kwa namna gani deni la Taifa litapunguzwa. Itakuwa vema kuonyesha waziwazi mikakati itakayotumika ili kuhakikisha kuwa deni la Taifa linalipwa.

		<p>hadi kufikia miaka 10, muda wa kuiva kwa mikopo hufikia hadi miaka 50 ijapokuwa kuna kuwepo viashiria hasi vyatukumbana na mabadiliko ya kiwango cha kubadili fedha (Foreign Exchange Risk). Mikopo ya ndani haikumbwi na athari za mabadiliko ya viwango vyakubadilishana fedha, ila inapatikana kwa kiwango cha juu cha riba, masharti yasiyo nafuu, huanza kulipwa baada ya muda mfupi na upatikanaji wa kiasi kikubwa cha mkopo unadhibitiwa chini ya Sera ya “Policy Support Investment” (PSI). Kwa sasa Serikali inaruhusiwa kukopa ndani ya nchi hadi asilimia 1 ya Pato la Ndani la Taifa (GDP). Udhibiti huu unafanyika ili kutodhoofisha uwekezaji mitaji wa ndani. Soko la ndani ya nchi halina uwezo wa kutosha kutoa fedha za kugharamia shughuli za Serikali, hii ndiyo sababu uamuzi wa kukopa zaidi nje unafikiwa na Serikali. Hata hivyo, mwezi Machi, 2012 Serikali ilifanya tathmini ya uhimilivu wa deni la Taifa ili kuona kama nchi bado inao uweze wa kuendelea kulipa madeni yake; matokeo ya tathmini yanaonyesha kuwa Serikali bado inao uwezo wa kulipa madeni kwa kuzingatia rasilimali ilizonazo.</p>	
--	--	--	--

21	UsimamiziwaDhamana za Serikali	Serikali inaafiki mapendeleko ya ukaguzi juu ya kutokuwa na viwango vya dhamana kinyume na sheria ya Mikopo ya Dhamana, na Ruzuku ya Sheria ya mwaka (1974) kama ilivyorekebishwa mwaka 2004. Dhamana nyingi zilitolewa kwenye Wizara, Idara na Wakala ili kupata fedha kutoka mifuko ya Hifadhi ya Jamii kwa ajili ya utekelezaji wa miradi mbalimbali ya maendeleo. Miogoni mwa taasisi nyingine ni pamoja na ujenzi wa Chuo Kikuu cha Dodoma, Chuo Kikuu cha Nelson Mandela kilichopo Arusha na ujenzi wa nyumba za kuishi za askari wa Jeshi la Polisi. Serikali imeamua kuahirisha kwa kipindi cha mwaka mmoja utoaji wa Dhamana kwa Wizara, Idara na Wakala na Mashirika ya Umma ili kuiwezesha kuitopia athari juu ya undelevu wa madeni. Ni katika kipindi hiki kwamba Serikali kuitopia Mikopo ya Dhamana na Ruzuku ya Sheria (1974) iliyorekebishwa mwaka 2004 ya kuanzisha masharti mbalimbali kufanyiwa marekebisho kama inafaa.	Majibu ya Serikali yamepokelewa. Uhakiki wa suala hili utafanyika katika ukaguzi ujao.
22	Fedha zilizotolewa kuagiza bidhaa nje ya nchi ambazo hazijarudishwa Serikalini.	Hazinaimekuwa ikifanya kazikwa karibu namkusanyaji madeniM/MSolopalInvestmentCo Ltd, ambaye taarifa	Majibu ya Serikali yamepokelewa; Matokeo ya mashauriano kati ya Serikali na Mwanasheria Mkuu wa Serikali juu ya

		<p>yake ya mwishokwakipindikilichoish ia Disemba 31, 2011taarifa hiyo ilionyesha kuwepo kwa changamoto zilizokwamisha ukusanyaji wa deni lote na mapendekezo ya hatua za kuchukua. Hazinakwa kushauriana na vyombo vingine vyaseriali pamoja na Mwanasheria Mkuu wa Serikali kuangalia ni namna gani mapendekezo yaliyotolewa na mkusanyaji wa madeni yatakavyotekelawa.</p>	<p>hatua zitakazochukuliwa dhidi ya wafanyabiashara waliokiuka masharti ya mikopo yatafanyiwa tathmini wakati wa ukaguzi wa mwaka ujao.</p>
23	Madeni na Mihadi	<p>i. Mihadi</p> <p>Kiasi hiki kilitengwa kwa ajili ya kulipa mikataba ambayo bado ilikuwa haijakamilika mwisho wamwaka wa fedha. Fedha hizozilihamishiwa kwenyeakauntiya Amanabaada ya kupatakibali kutoka mamlaka husika. Fedha hizo zitalipwa baada ya mikataba kukamilika. Tatizo hili halitatokea wakati ujao kwa kuwa Serikali iko katika mchakato wa kuhamia katika mfumo wa “IPSASaccrual”</p> <p>ii. Madeni</p> <p>Serikaliinakabiliwa na changamotoza makusanyo ya mapato zinazosababishwa namasualambalimbali kama vilemdororo wa uchumi</p>	<p>Majibu ya Serikali yamepokelewa.</p> <p>Hata hivyo imebainika kwamba upo ucheleweshaji wa kutoa fedha kutoka Hazina kwenda kwa Maafisa Masuuli na hazitolewi zote kwa mujibu wa bajeti iliyopitishwa na Bunge. Ni matumaini yangu kwamba hatuamuhimuzitachukuliwaku hakikisha fedhazinatolewa kwa wakati.</p>

		<p>duniani, uhaba wa umeme uliosababisha kutolingana kati ya mapato na matumizi katika mwaka uliomalizika.</p> <p>Madenihaya yanasantabishwa na mahitaji yasiyokwepeka kwa mfano manunuziya Madawa, chakul akwa ajili ya shulenamagerezapamoja na ukweli kwamba Serikali inafanya kazikwa utaratibu wafedha taslimu.</p>	
24	Mali zisizoingizwa katika daftari la mali	<p>Ni kweli kwamba Wizara, Idara na Mikoa hazi jaingiza kumbukumbu za mali katika daftari la kudumu la mali. Aidha mali nyingine zimeingizwa bila kuonyesha taarifa muhimu kama vile thamani na mahali mali hizo zilipo.</p> <p>Serikali imeona mapungufu haya na imeagiza Maafisa Masuuli kufuata sheria ya fedha ya mwaka 2001 pamoja na kanuni zake.</p>	<p>Majibu ya Serikali yatahakikiwa katika ukaguzi wa mwaka ujao. Rejesta ya mali za kudumu iliyo kamilika budi iwasilihwe ukaguzi kwa ajili ya mapitio kwa maandalizi ya ukaguzi ujao.</p>
25	Misamaha ya kodi	<p>Serikali inalionia ongezeko la mwenendo wa misamaha ya kodi inayotolewa kila mwaka. Wakati inatambua ukweli huu, Serikali iliunda timu ya wataalam kutoka Wizara ya Fedha na Mamlaka ya Mapato Tanzania (TRA) ili kufanya upembuzi yakinfu wa mifumo ya kodi ya nchi mbalimbali zilizopiga hatua katika kurahisisha masuala</p>	<p>Majibu ya Serikali yamepokelewa; hata hivyo, hakuna ratiba inayoonyesha ni lini upembuzi huo wa mifumo ya kodi utafanywa na lini Sera mpya ya misamaha ya kodi itakuwa tayari.</p>

	<p>ya kodi, mageuzi katika uwazi kwa masuala yahusuyo kodi na misamaha ya kodi. inatarajiwa kuwa, matokeo ya upembuzi huo yatasaidia kutayarisha Sera ya misamaha ya kodi kwa nchi yetu ambayo uenda ikasaidia kupunguza kiasi cha misamaha kinachotolewa. Serikali inatoa misamaha ya kodi kwa mujibu wa sheria za kodi; ni lazima Serikali itoe misamaha ya kodi kwa sababu zifuatazo:</p> <ul style="list-style-type: none"> • Kutoa misamaha kwa wawekezaji ili kuweka mazingira mazuri ya kukua kwa uchumi • Miradi inayofadhiliwa na wadau wa Maendeleo ina masharti yanayoambatana na makubaliano wanayofikia na Serikali kwamba, kodi kama vile: ushuru wa kuagiza mali, VAT na ushuru wa bidhaa zinazozalishwa ndani itasamehewa • Kutoa unafuu kwa watumishi wa Serikali wanaponunua magari • Kuziwezesha Taasisi zisizo za Kiserikali (NGOs) kuchangia kikamilifu katika huduma za jamii ikiwa ni kusaidia juhudini za Serikali za kupunguza umaskini. Vile vile, Serikali kupitia TRA inaendelea na mikakati 	
--	--	--

		yake ya kupanua wigo wa kodi kwa lengo la kuongeza mapato.	
26	Kutoandika kwa usahihi mikopo iliyotolewa naSerikalikamadhamana na	<p>Serikaliinakubalimapendek ezoya wakaguzi wa hesabukuhusukutoandika kwa usahihi mikopoiliyotolewa moja kwa mojakamadhamana, kwa makampuni ya maua. Serikali ilitoleamikop kwaMakampunisita(6) yaMauanamoja(1) la ufungaji wa ng'ombe kupitiaMfuko wa Maendeleo wa Dhamana(DFGF). DFGFilianzishwana Serikali mwaka2003 kwa lengokuula kuendeleza nakuimarishaviwandaya ukulima wa mauakatikanchi. Hatua zimechukuliwana Serikaliza kuokoamikopoisyorejeshwa ambapoumiliki wake umeishakamaifuatavyo:-</p> <ol style="list-style-type: none"> 1. Hivi karibuniSerikaliimelipwaSh. 5,132,167,000.00(Mkopo halisil Sh.3,835,000,000.00nariba ya Sh.1,297,167,000.00)na HortanziaLtd(Mmoja wawanufaika wa mikopo iliyotolewa na DFGF) kwa njia ya mnada. 2.Hatuanyingineiliyochukuli wana Serikali nikubadilishasehemuyaSha mbala FleurD "Afrique Limited(ArushaBloomsLtd) na kuzalisha viwanja kwa ajili ya maendeleo ya mji. Idhiniilitolewa na 	<p>Majibu ya Serikali yamepokelewa na kupitiwa.Nyaraka za kuthibitishahatua ambazozimechukuliwazina paswa kuwasilishwa kw Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesebu za Serikali ajili ya mapitiozaidi.Pia,kuna haja ya kuwa na utaratibuwakuhakikisha kwambamikopo iliyotolewa inarejeshwa..</p>

		Halmashauri ya Wilaya ya Arushakuendelea kuuza viwanjanainatarajiwa kwambaifikapo Septemba,2012shambalitak uwa limeuzwanadeni halisi la Sh.10,100,000,000na riba zitakuwazimerejeshwa. 3. Serikali kupitiaBenki Kuu yaTanzania itafanya kazi kwa karibu zaidi naBenki ya Rasilimali ya Tanzania kuchunguza utendaji wataasisi zotena kupendekeza hatuamadhubuti ili kupata ufumbuzi ili kupata ufumbuzi wa tatizo hili kwa ajili ya kutimiza lengo la Serikali la kusaidia miradi ya maendeleo inayojishughulisha na utengenezaji/uzalishaji wa bidhaa kwa ajili ya kuuza nje	
27	Kutojihusisha kikamilifu kwa Serikali katika makubaliano ya kutayarisha mikatabakujenga Chuo Kikuu cha Dodoma (UDOM) na vingine kama hivyo	Mkataba wa ujenzi wa Chuo Kikuu cha Dodoma na Chuo Kikuu cha Nelson Mandela isipokuwa Hosteli ya Mabibo ulitekelezwa kwa utaratibu wa kusanifu, kujenga, kumiliki na kuhamisha. Katika mikataba hii kuna majukumu/wajibu maalum kwa mifuko ya pensheni, Serikali (Wizara ya Fedha kama mkopaji) na Wizara ya Sayansi na Tekinolojia (mpangaji).	Mapendekezo ya Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikaliwa kufanyaukaguzi wa thamani yafedhajuu yaujenzi wa miradi yote mitatuna kupatagharama halisizilizotumika,stahilina uhalali wamadaiyaliyotolewa na taasisi ya mifuko ya Jamii kwa Serikali hayajatekelezwa.
28	Udhaifu katika mfumo wa kusimamia ubia kati ya sekta ya	(i) Miradi iliyopo Serikali imeanza kurekebisha baadhi ya	Majibu ya Serikali yamepokelewa na kupitiwa. Hata hivyo

	umma na binafsi (PPP)	<p>matatizo yaliyotokana na shughuli za ubia kati ya sekta ya umma na binafsi (PPP) Hatua zilizochukuliwa ni pamoja na kuahirisha mikataba ya Makampuni ambayo yameshindwa kufuata sheria na masharti. ya mikataba. Makampuni hayo ni pamoja na RITES (TRL Ltd), Shirika la ndege la Afrika Kusini, ATCL, Tan Power Resources inayosimamia Mgodi wa Makaa wa Mawe wa Kiwira na City Water.</p> <p>Katika mwaka ujao wa fedha, Serikali inakusudia kufanya mapitio juu ya miradi iliyopo ili kupima na kujua ukubwa wa athari zilizopo katika mfumo wa kusimamia ubia kati ya sekta ya umma na binafsi. Mapitio hayo yatasaidia kurekebisha baadhi ya atharizitakazobainishwa.</p> <p>(ii) Miradi ya baadaye</p> <p>Sheria ya ubia kati ya sekta ya umma na binafsi na kanuni zake inataka kuwe na tafiti yakinifu kwa ajili ya utekelezaji wa miradi ya baadae. Kuandaa mikataba ya manunuzi dhidi kwa mipango iliyopo ya kusimamia sekta ya umma na binafsi na kutathmini uwezo wa kuwa na rasilimali ambazo zitawezesha kutekeleza miradi hiyo.</p>	<p>matokeo ya hatua zinazotarajiwa kuchukuliwa na Serikali katika kusimamia ubia kati ya sekta ya umma na binafsi kwa ajili ya kuimarisha ufanisi yatafanyiwa mapitio na kutolewa maoni wakati wa ukaguzi ujao.</p>
--	----------------------------------	--	---

	<p>Wakati wa mchakato wa uchambuzi yakinifu, wa miradi tathimini ya gharama-faida huangaliwa.</p> <p>(iii) Usimamizi wa madeni sanjari na uhasibu kwa mali na madeni ya PPP. Benki Kuu ya Tanzania hutoa Dhamana kwa ajili ya miradi ambayo itaongeza faida kiuchumi, kutokana na kuzaa nje na kuongeza ajira kwa Watanzania. Fedha za mpango zinatengwa na hutumiwa kudhamini miradi katika uwiano wa 50%, 75% na 80% kulingana na makubaliano ya mkataba. Mikataba ya miradi ya PPP ni ya muda mrefu ambayo inaweza kusababisha kuzaa madeni sanjari. Serikali kabla ya kuingia mikataba ya PPP, hufikiria viashiria hatarishi vinavyoweza kutokea kutokana na madeni yasiyotarajiwu kuititia njia mbalimbali kama vile haki ya mgawanyo wa hasara na madeni yanayotokea bila kutegemea hatari kati ya vyama, pamoja na ufuatiliaji na tathmini ya miradi na mgao wa fedha katika bajeti kwa ajili ya kuhudumia madeni sanjari. Miradi ya PPP ilianzishwa na kutekelezwa na Wizara, Idara na Halmashauri baada ya kuidhinishwa na Bunge.</p>	
--	--	--

2.2 Baadhi ya shughuli za Serikali hazikujumuishwa katika Hesabu Jumuifu za Taifa

Katika kuitia taarifa za fedha iligundulika kuwa Taarifa za Hesabu Jumuifu za Taifa hazikujumuisha mapato, matumizi na fedha taslim za Serikali za Mitaa kutokana na kutumia mifumo tofauti ya kiuhasibu ya utoaji taarifa. Aidha, hesabu za mashirika ya umma hazikujumuishwa katika Hesabu Jumuifu za Taifa kinyume na Aya 1.6.5 ya IPSAS.

2.3 Majibu ya taarifa za kila fungu kutoka kwa Afisa Masuuli yaliyowasilishwa kwa Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali

Ofisi za Wizara, Idara na Sekretarieti za Mikoa zimekuwa na maendeleo mazuri katika utekelezaji wa masuala ya kaguzi za nyuma. Hata hivyo, katika mwaka huu wa ukaguzi, Wizara, Idara na Sekretarieti za Mikoa60 zilikuwa hazijashughulikia masuala ya miaka ya nyuma yenye jumla ya, Sh.2,006,667,848,562.49, USD 2,117,226.99,JPY 16,965,125,082.95 na Euro 850,000. Kati ya kiasi hicho, deni la Taifa na Huduma za Ujumla inaongoza kwa kiasi kikubwa cha Sh.842,698,586,988.07 ikifuatiwa na Wizara ya Miundombinu yenye kiasi cha Sh.674,330,186,269.00 na Wizara ya Ulinzi na Jeshi la Kujenga Taifa ikiwa ya tatu yenye kiasi cha Sh.85,140,905,881.00 na Euro 850,000. (**Kiambatisho Na.I.**).

Lengo la kuwasilisha matokeo ya ukaguzi pamoja na mapendekezo kwa mkaguliwa ni kumsaidia mkaguliwa kurekebisha kasoro zilizojitokeza katika usimamizi wa fedha na udhibiti wa mali katika Wizara, Idara,Wakala na Sekretarieti za Mikoa. Kutojibwa kwa hoja na mapendekezo ya ukaguzi, kutokufanyiwa kazi kama inavyoonekana katika Wizara, Idara,Wakala na Sekretarieti za Mikoa ni kosa kubwa kwa Maafisa Wahasibu wa taasisi hizo na uongozi wa Wizara, Idara,Wakala na Sekretarieti za Mikoa husika.

Kutoshughulikiwa kwa hoja na mapendekezo ya ukaguzi kunasababisha kasoro zilizojitokeza wakati wa ukaguzi kujirudia katika miaka inayofuata. Pia, hii inaonyesha kutowajibika

kikamilifu kwa Maafisa Wahasibu na uongozi wa taasisi husika.

Katika mwaka wa fedha wa 2011/2012 Wizara, Idara na Sekretarieti za Mikoa ambazo ziliikuwa hazijashughulikia masuala ya miaka ya nyuma zimeongezeka kutoka 58 mpaka 60 zenye jumla ya Sh.2,006,667,848,562.49, USD 2,117,226.99, JPY 16,965,125,082.95 na Euro 850,000 ukiltinganisha na Sh.543,364,747,075.99 katika mwaka 2010/2011.

Mchanganuo huu unaonyesha kwamba Menejimenti za Wizara, Idara na Sekretarieti za Mikoa hazikufanya jitihada za kutosha kushughulikia mapendekezo ya ukaguzi. Orodha ya masuala ya miaka ya nyuma yasiyojibwa yako kwenye Kiambatisho Na. I katika ripoti hii.

2.4Mamlaka ya Mapato Tanzania

Hadi kufikia wakati wa kutoa taarifa yangu kwa Mamlaka ya Mapato Tanzania (Disemba 31, 2012); Mamlaka ya MapatoTanzania ilikuwa namasuala mbalimbali ya ukaguzi yaliyopotiwa katika taarifa zilizopita yaliyofikia kiasi cha Sh.545,273,124,808 na Dola za Kimarekani 105,036,380 kama yalivyoainishwa hapa chini ambayo hayakuwa yameshughulikiwa kikamilifu.

Jedwali 5:Masuala ya Mamlaka ya Mapato yaliyosalia

Idara	Kiasi(Sh.)	Kiasi (Dola za Kimarekani)
(i) Maduhuli		
Ushuru wa Forodha	25,019,207,641	-
Idara ya Kodi za Ndani	16,955,384,161	-
Idara ya Walipa Kodi Wakubwa	503,166,532,902	105,036,380
Jumla	545,141,124,704	105,036,380
(ii) Matumizi	132,000,104	-
Jumla	545,273,124,808	105,036,380

Baadhi ya masuala yaliyoainishwa kwenye jedwali hayakujibowi kikamilifu tangu mwaka 2001/2002 na baadhi yake yanashubiri maamuzi ya Mahakama.

2.5 Majibu ya hoja zitokanazo na ukaguzi wa Taarifa Jumuifu za Taifa

Jedwali 6: Mapendekezo ya nyuma ya ukaguzi wa Taarifa Jumuifu za Taifa

Namba	Maelezo
1.0	Usimamizi wa madeni yanayotarajiwa kutokana na ubia kati ya Sekta ya Umma na Sekta Binafsi katika kutekeleza miradi (PPP)
1.1	Udhaifu katika mfumo wa kusimamia ubia kati ya sekta ya umma na binafsi Mapitio ya makubaliano yaliyofanywa kati ya Serikali na sekta binafsi kwa baadhi ya wawekezaji binafsi imeonekana kuwa na mafanikio kidogo yenye mapungufu makubwa. Mazungumzo hayo ni kati ya Serikali na SONGAS Ltd, IPTL Ltd, ARTUMAS, TRL Ltd, ATCL Ltd, Kiwira Coal Mines (TANPOWER Ltd), City Water na TICTS.
	Serikali ilitakiwa kufanya uchambuzi wa kina wa gharama na manufaa pamoja na thamani ya fedha, baadhi ya rasilmali au vitega uchumi vimeonekana kutokuwa endelevu kiuchumi. Hakuna kilichotekeliza kama nilivyopendekaza.
	Serikali ilitakiwa kuangalia uwezekano wa kupitia mikataba iliyopo ili kuangalia kama kuna mapungufu ambayo yanaweza kurekebishwa na kuhakikisha kwamba Serikali inanufaika na shughuli hizo na kuzuia uwezekano wa athari zinazoweza kutokea kutokana na makubaliano hayo. Hakuna kilichotekeliza kama nilivyopendekaza.
	Serikali ilitakiwa kumpatia Mshauri kazi ya kukagua

	<p>utendaji wa uongozi makampuni yote. Hakuna kilichotekelawa kama nilivyopendekaza.</p>	katika kuendesha
	<p>Serikali ilitakiwa kupata ushari wa kisheria katika mchakato wa kuzingatia uvunjaji wa mikataba yote na makampuni binafsi ambayo yameshindwa kuzingatia sheria na masharti ya mikataba. Hakuna kilichotekelawa kama nilivyopendekaza.</p>	
1.2	<p>Usimamizi wa madeni yamkini kutokana na ubia kati ya Serikali na sekta binafsi mali na amana zake Ingawa nilipendekeza kwa Serikali kupitia Wizara ya Fedha kuzuia kutoa mikopo na kudhamini sekta binafsi au wawekezaji wasio na uwezo kifedha kwani kwa kufanya hivyo, mzigo wote hubebwa na Serikali. Sababu ya kutofuata kifungu Na.13 na 14 Sheria ya Mikopo, Udhamini na Misaada ya mwaka 1974 (iliyorekibishwa mwaka 2004) hazijatolewa.</p> <p>Kwa kuwa Benki Kuu ya Tanzania ni wakala wa Serikali, haina budi kusimamia na kuendesha mfuko maalumu kwa kufuata sheria ya Mikopo, Udhamini na Misaada Na.30 ya mwaka 1974 (iliyorekibishwa mwaka 2004).</p>	
	<p>Pamoja na hayo, mapendekezo yangu kwa Serikali kurekebisha Sheria ya Mikopo, Udhamini na Misaada ya mwaka 1974 (iliyorekibishwa mwaka 2004) yanayoongelea rehani kwa mikopo na dhamana inayotolewa na mashirika ya umma bado hayajazingatiwa</p>	
	<p>Mara nyingi makubaliano ya ubia kati ya Serikali na sekta binafsi (PPP) yameonekana kutokuwa na mpangilio mzuri wa uwendeshaji kwani ni dhahiri kwamba mwisho wa ubia husababisha Serikali kuwa na madeni makubwa ambayo haikuyatarajia.</p>	
1.3	Kutojihusisha kikamilifu kwa Serikali katika	

	<p>makubaliano ya kutayarisha mikataba na ujenzi kama vile Chuo kikuu cha Dodoma (UDOM), Hostel ya Mabibo, nyumba za Polisi na vingine kama hivyo.</p> <p>Ingawa nilitoa mapendekezo yangu kwa Wizara ya Fedha kumpatia mshauri kazi ya ukaguzi wa thamani ya fedha katika miradi hiyo mitatu ili kugundua gharama halisi zilizotumika, stahili na uhalali wa madeni kutoka Mifuko ya hifadhi ya jamii, hakuna kilichoteklezwa na Wizara.</p>
--	---

2.6 Utekelezaji wa maagizo yaliyotolewa na Kamati ya Bunge ya Hesabu za Serikali Kuu (PAC)

Sehemu hiiinashughulikiahali ya utekelezaji wa mapendekezo ya Kamati ya Bunge ya Hesabu za Serikali Kuu (PAC)kwa mujibukifungu cha 40(3) cha Sheria ya Ukaguzi waUmma, 2008. Sheria inamtaka Mlipaji Mkuu wa Serikali (PMG), kuandaamajibu nampango wa kujibu taarifa ya Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali (CAG)pamoja na majibu ya mapendekezoya Kamatiya Bunge. Mwenyekiti wa kamati ya PACaliwasilisharipotiya Kamatiya mwaka wa fedha ulioishiaJuni 30, 2010. Ripoti hiiiliwasilishwaBungenimwezi Aprili,2012. Majibu ya Serikali yaliyoandaliwa hayakuonyesha utekelezaji wa mapendekezo PAC kama ifuatavyo:

2.6.1 Ukosefuwa udhibiti wa ndanijuu yamakusanyo ya mapatokatikaWizara ya Habari, Utamaduni Vijanana Michezo

Kamati ya PACiliona kwambaShirikisho la Soka Tanzania(TFF)inadaiwa na Wizara ya Habari, Utamaduni, Vijanana Michezokiasi kikubwa cha mgawo wa makusanyo yalango, tokaviwanjambalimbali vyat michezo vyat TFF. PACilipendekeza kwambaWizara ya Habari, Utamaduni Vijana, na Michezoinapaswa kuwekezakwenyewazo la kuanzishaChuwachezajiwenye vipaji ambaa watapewa mafunzokabla yakuuzwanje ya nchi kwa kwa lengo la

kuongezamapato ya serikali nakuongezauwekezajikatika michezo nautalii.

2.6.2 Matumizimabaya ya fedha za Serikali
Mbali na kutozingatia masharti ya Sheria ya Ununuzi waUmma, katika mwaka wa fedha 2009/2010, CAG alihoji kuwepo matumizi yenye hati pungufu ya jumla ya Sh. 362,026,933,382.25. Hata hivyo, Kamati ilibainisha kuwa hoja za ukagazi hatimaye zilifungwa baada ya hati zilizokosekana kuwasilishwa kwa wakagazi na kuhakikiwa. Kamati alibainisha kwamba katika matukio mengi, nyaraka zilizokosekana wakati wa ukagazi hatimaye hupatikana kwa muda mfupi kabla Maafisa Masuuli kufika mbele ya Kamati.

Kamatiilipendekezakwamba, mafunzoyatolewe kwawasimamizi na watunza kumbukumbu nakwambamfumo wa kielektroniki unapaswakufungwaambao utahakikisha utunzaji sahihi wa kumbukumbu za Serikali na ulio endelevu.

2.6.3 Kutayarisha Hesabu Kufuata Viwango vya Kimataifa vya Uandishi wa vitabu vya Sekta ya Umma (IPSAS)
Taarifa za fedha zaSerikali Kuuzinatayarishwa kwa kufuata Viwango vya Kimataifa vya Uandishi wa vitabu vya Sekta ya Umma.

PACilibaini kuwakwa kutumia mfumo wa IPSASnimiongoni mwa sababu zilizosababisha Hesabu Jumuifu za Serikalikupata hati isiyoridhisha kwa mwaka2007/2008 na2008/2009nahati yenye mashakakatika kipindi cha mwaka2009/2010.Afisa Masuuli Mwajibika alielezaKamatikwambahesabu za SerikaliKuu zitaendeleakupata hati isiyoridhishakutokana na kutokuwepo daftari la mali za kudumu hadi hapo litakapoandaliwa.

Kamati ilipendekeza kwa serikalikuanza mchakatowa kuandaarejistaambayo itawezesha kuandaa taarifa za fedhakwa kufuatalPSAS (accrualbasis of accounting).

Ingawa AfisaMhasibualijibu kuwa hatuaya kuandaa daftari la

mali za kudumuimeanzalakini hakutaja muda wa kukamilisha kazi hiyo.

2.6.4 Utekelezaji wa mapendekezo ya ukaguzi kuhusu Mfumo Funganifu wa Usimamizi wa Fedha (IFMS)

Katika mwaka 2009/2010, Ofisi ya Taifa ya Ukaguzi iliipa Kampuni ya ukaguzi ya KPMG kazi ya kuufanya tathmini Mfumo Funganifu wa Usimamizi wa Fedha (IFMS) ili kujua ufanisi wake katika kuchakata taarifa za fedha katika Serikali Kuu na Serikali za Mitaa. KPMG ilifanya tathmini ya kazi ambazo Mfumo unafanya, utekelezaji wa mfumo wenyewe na mifumo ya udhibiti inayouzunguka Mfumo wa IFMS na kazi zaidi ilifanyika ili kubaini kama Serikali inapata thamani ya fedha kutokana na kuwekeza katika Mfumo Funganifu wa IFMS.

Kutokana na taarifa ya utekelezaji iliyowasilishwa kwangu na Hazina, juhudini kubwa zimefanywa katika kutekeleza mapendekezo yaliyotokana na tathmini ya ufanyaji kazi wa Mfumo.

Hata hivyo, Serikali iongeze juhudini zaidi ili kukamilisha utekelezaji wa mapendekezo yaliyabakia. Mpango wa Wizara wa kukamilisha mapendekezo yaliyobakia ni kama inavyoonekana hapa chini:

S/N	Ukurasa	Hoja ya Ukaguzi	Jibu la Wizara	Mpango wa utekelezaji	Hali ya utekelezaji hadi kufikia tarehe 04 Machi, 2013	Maoni
2	49	Usimamizi dhaifu wa mkataba	Shughuli zote zinaongozwa na mikataba sahihi ambayo imeandaliiwa kama LPO au mikataba halisi. Wizara inakiri kuwepo	Ofisi ya Mhasibu Mkuu wa serikali iliandaa mafunzo yahusuyo usimamizi wa mikataba kwa wadau wakuu	<ul style="list-style-type: none"> • Watumishi kutoka Kitengo cha Manunuizi pamoja na wahasibu tayari wameshapewa mafunzo • Mikataba ya 	Utekeli ezaji unaendelea

S/N	Ukurasa	Hoja ya Ukaguzi	Jibu la Wizara	Mpango wa utekelezaji	Hali ya utekelezaji hadi kufikia tarehe 04 Machi, 2013	Maoni
			<p>udhaifu katika utunzaji wa nyaraka hasa zile zinazohusiana na kazi zilizokwisham alizika katika kipindi cha nyuma.</p> <p>Kwa kipindi cha nyuma, Wizara haikuwa na Kamati ya Zabuni; hata hivyo, uwekaji sahihi kumbukumbu halikuwa jambo rahisi kutokana na kupita muda mrefu (tangu mwaka 2000 hadi ththmini ya IFMS ilipofanyika)</p>	<p>wanaohusika na usimamizi wa mikataba katika ngazi ya idara; hii inaenda sambamba na juhudi za kuboresha usimamizi wa mikataba kwa huduma zinazotolewa katika Idara ya Mhasibu Mkuu wa serikali.</p> <p>Majukumu makuu katika Idara ya Mhasibu Mkuu wa serikali yatafanyika kwa kufuata vipengele vyta mikataba iliyoingiwa.</p> <p>Mikataba itatunzwa vyema na kusimamiwa vizuri.</p>	<p>sasa inatunzwa na kusimamiwa vizuri</p>	

S/N	Ukurasa	Hoja ya Ukaguzi	Jibu la Wizara	Mpango wa utekelezaji	Hali ya utekelezaji hadi kufikia tarehe 04 Machi, 2013	Maoni
5	55	Utunzaji dhaifu wa taarifa	Wizara inakiri kuwepo udhaifu katika utunzaji wa nyaraka hasa zile zinazohusiana na kazi zilizokwisham alizika katika kipindi cha nyuma.	Kuanzisha sera ya utunzaji bora wa kumbukumbu kutawezesha nyaraka zinazotumika kuweza kufanyiwa marekebisho pale itakapolazim u kufanya hivyo. Sera hii itakuwa imekamilika ifikapo Disemba 2013. Pamoja na yote hayo, Idara ya Mhasibu Mkuu wa serikali itaangalia uwezekano wa kutumia programu ya kompyuta iliyopo katika Idara	<ul style="list-style-type: none"> • Wizara inaangalia namna bora ya kushughuliki a tatizo hili. Hii inajumuisha kuangalia uwezekano wa kutumia programu ya kompyuta kama ‘Saperion document management’ ambayo inatumika hivi sasa katika kitengo cha pensheni cha Idara ya Mhasibu Mkuu wa serikali 	Utekel ezaji unaendelea

S/N	Ukurasa	Hoja ya Ukaguzi	Jibu la Wizara	Mpango wa utekelezaji	Hali ya utekelezaji hadi kufikia tarehe 04 Machi, 2013	Maoni
				kwa ajili ya utunzaji wa nyaraka.		
7	58	Mafunzo kwa Watumiaji	Huu ni mwendelezo wa shughuli. Mafunzo haya hotolewa kwa njia mbili; Inapotokea watumishi wa SDU kutembelea mikoani kutoa mafunzo kwa watumiaji ni wajibu wao. Tumeona utaratibu wa mafunzo ulioandalialiwa. Hata hivyo, bado tunaona kuna tatizo la kukosekana ujuzi wa kutosha kwa baadhi ya watumiaji kutokana na watu kuacha kazi mara kwa mara na kuhama kutoka ofisi moja kwenda nyingine.	Watumiaji wa mtandao wa IFMS watapewa mafunzo kila inapohitajika. V ivyo hivyo, timu ya wataalamu pia itaendelea kupata mafunzo ili kuboresha zaidi ujuzi wao.	<ul style="list-style-type: none"> Mwezi Julai na Agosti 2010 watumiaji 110 wa mtandao huu walipata mafunzo ya jinsi ya kutumia mtandao wa IFMS ili kufanya malipo ya moja kwa moja kielektroniki yaani TISS. Kundi jingine la watumiaji 145 lilipewa mafunzo ya jinsi ya kufanya malipo moja kwa moja kupitia mtandao wa TISS mwezi Mei 2011. <p>Kundi la watumiaji kutoka Hazina Ndogo na Ofisi za Maafisa Tawala wa Mikoa walifunzwa</p>	Utekelezaji unaende lea

S/N	Ukurasa	Hoja ya Ukaguzi	Jibu la Wizara	Mpango wa utekelezaji	Hali ya utekelezaji hadi kufikia tarehe 04 Machi, 2013	Maoni
					<p>jinsi ya kutumia mtandao ili kufanya malipo kwa njia ya kielektroniki yaani TISS mwezi Disemba 2011.</p> <ul style="list-style-type: none"> • Mwezi Machi na Aprili 2010 watumiaji 111 kutoka Wizara na Idara za Serikali na watunzaji wa mali za Serikali walifundishwa jinsi ya kutumia Epicor kuweka kumbukumbu za mali za Serikali. • Mwezi Aprili na Mei 2012 kikundi cha watu 318 ambao ni watumiaji wa mwisho wa mtandao walipata mafunzo kuhusu marekebisho yaliyofanywa kwenye toleo 	

S/N	Ukurasa	Hoja ya Ukaguzi	Jibu la Wizara	Mpango wa utekelezaji	Hali ya utekelezaji hadi kufikia tarehe 04 Machi, 2013	Maoni
					<p>jipya la mtandao yaani Epicor 9:05</p> <ul style="list-style-type: none"> • Mwezi Novemba 2012 watumiaji kutoka ofisi za Balozi zetu walipewa mafunzo ya jinsi ya kuendesha mashine zinazotumika kutolea Visa katika Balozi za Tanzania nchi za nje. 	
8	59	Kutotumika kwa moduli katika Mfumo Funganifu wa Usimamizi wa Fedha (IFMS)	<p>Programu ya EPICOR inayotumiwa na Mfumo Funganifu wa Usimamizi wa Fedha (IFMS) inajumuisha moduli saba muhimu.</p> <p>Kati ya moduli hizo saba, moduli 5 zifuatazo zinatumia kikamilifu:</p> <p>Meneja wa Mfumo , Akaunti ya Wadai, Akaunti ya Wadaiwa,Menejimenti ya Fedha,leja kuu na</p> <p>Menejimenti ya nyenzo.</p>	<p>Kutekeleza utumiaji wa Epicor toleo la 9: 05 na wa moduli zote zilizolipiwa kutumika kikamilifu.</p> <p>Moduli hizi zinajumuisha Meneja wa Mfumo Akaunti ya Wadai, Akaunti ya Wadaiwa, Menejimenti ya Fedha,leja kuu na</p> <p>Menejimenti ya nyenzo.</p>	<ul style="list-style-type: none"> • Pamoja na Utekelezaji wa Epicor toleo la 9:05 moduli zote zilizolipiwa zinatumika. Aidha, moduli ya Usimamizi wa mali ipo tayari kutumika. • Wizara 20 zimeweza kutumia moduli ya Usimamizi wa mali katika hatua za 	Inaendelea kufanyi wa kazi

S/N	Ukurasa	Hoja ya Ukaguzi	Jibu la Wizara	Mpango wa utekelezaji	Hali ya utekelezaji hadi kufikia tarehe 04 Machi, 2013	Maoni
			<p>na leja kuu .Moja kati ya hizo inayoshughulikia manunuzi haitumiki kikamilifu na moduli iliyobakia iitwayo Usimamizi wa mali imekaribia kuanza kutumika.</p> <p>Mafunzo ya jinsi ya kutumika moduli ya Usimamizi wa mali yanaendelea.</p>		<p>mwanzo za Epicor (Epicor 7.3.5).</p>	
9	60	Rasilimali za Mfumo Funganifu wa Usimamizi wa Fedha (I FMS) zilizolipiwa lakini hazitumiki kikamilifu	<p>Wakati wa ukaguzi, mfumo wa utunzaji wa taarifa katika kompyuta ulikuwa umeharibika kwa sababu ya tatizo la umeme na ulihitaji kubadilishwa.</p> <p>Kwa sasa, mfumo huo wa utunzaji wa taarifa katika kompyuta umebadilishwa; uunganishwaji wa mifumo unaendelea na</p>	<p>Utayalishaji wa mkakati wa kukabiliana na majanga ulikamilika tangu Januari 2011</p>	<ul style="list-style-type: none"> Idara ya Mhasibu Mkuu imechagua mkakati wa DRS, ambapo mfumo wa utunzaji wa kumbukumbu katika ofisi za TAMISEMI Dodoma umewekwa katika ofisi ya Mhasibu Mkuu wa Serikali Dar es Salaamna kinyume chake vile vile. Mpangilio huu ni wa manufaa kwa vyombo vyote viwili kwa kuwa 	Inaendelea kufanyi wa kazi

S/N	Ukurasa	Hoja ya Ukaguzi	Jibu la Wizara	Mpango wa utekelezaji	Hali ya utekelezaji hadi kufikia tarehe 04 Machi, 2013	Maoni
			DRS itaanza kazi kikamilifu hivi karibuni.		pande zote mbili zimeunganish wa na changamoto imebaki katika kifaa cha utunzaji wa kumbukumbu katika kompyuta.	
10	62	Kutokuwepo kwa utaalamu wa kutosha wa ndani juu ya Epicor	Tuligundua hilo na tutaboresha huduma katika makubaliano yajayo ili kuyafanya kazi mapendekezo ya Mkaguzi. Kwa kuanzia, tumeong eza idadi ya wafanyakazi wenye utaalamu ili kuruhusu mgawanyo wa kazi kulingana na mahitaji wa Mhasibu Mkuu wa Serikali. Utegemezi kwa Muuzaji umepungua kwa sasa kwa sababu shughuli hizo sasa tunafanya wenyewe.	Tumekwishaan daa makundi ndani ya SDU yatakayopata mafunzo kulingana na taaluma zao. Zoezi la mafunzo ni endelevu	<ul style="list-style-type: none"> • Tumekwishaan daa makundi ndani ya SDU yatakayopata mafunzo kulingana na taaluma zao • Timu iliyoanzishwa ilihudhuria mafunzo ya uchambuzi wa mfumo na ubunifu ambayo yalilifanyika nchini Swaziland mwezi Oktoba 2010. • Kundi jingine lilihudhuria mafunzo ya ubora wa mfumo nchini Uganda mwezi Disemba 2010. • Kundi la wafanyakazi 6 	Inaendelea kufanyi wa kazi

S/N	Ukurasa	Hoja ya Ukaguzi	Jibu la Wizara	Mpango wa utekelezaji	Hali ya utekelezaji hadi kufikia tarehe 04 Machi, 2013	Maoni
					<p>wengine kutoka SDU - Ufundii Walihudhuria mafunzo ya wiki mbili kuhusu mambo ya mtandao na mafunzo ya usimamizi wa mfumo wa utunzaji wa kumbukumbu katika kompyuta yaliyofanyika India mwezi Julai 2011.</p> <ul style="list-style-type: none"> • Mtumishi mmoja kutoka SDU alipata mafunzo ya utaalamu wa manunuzi na usimamizi wa mikataba • Wanachama 33 kutoka timu ya SDU walipatiwa mafunzo ya Epicor 9: 05 mwezi Aprili 2012. • Kwa kiasi kikubwa, mafunzo yamepunguza 	

S/N	Ukurasa	Hoja ya Ukaguzi	Jibu la Wizara	Mpango wa utekelezaji	Hali ya utekelezaji hadi kufikia tarehe 04 Machi, 2013	Maoni
					utegemezi wa uendeshaji kwa muuzaji na yameboresha huduma ya IFMS kwa watumiaji wa mwisho.	
11	96	Moduli ya kupokelea vifaa itumiwe na watanza stoo.	Hoja ya ukaguzi imepokelewa, watanza stoo wataunganishwa na Mfumo Funganifu wa Usimamizi wa Fedha (IFMS)	Mafunzo kwa watanza stoo kuhusu jinsi ya kuingiza LPO katika mtandao wa IFMS yatafanyika katika Wizara na Idara zote za Serikali. Wizara na Idara zitapanga watumishi watakaopanga kazi hizo. Wizara na Idara zitasaidia kuunganisha stoo zote na mtandao wa Epicor.	<ul style="list-style-type: none"> Mawasiliano yamefanyika kwa wizara zote kwamba wawezeshe kupatikana vifaa ili bohari ziunganishwe na Mfumo Funganifu wa Usimamizi wa Fedha (IFMS) Mafunzo kwa watanza stoo yatatayarishwa na SDU wataendesha mafunzo hayo. 	Utekelezaji unaende lea
12	97	Ukaguzi wa usimamizi wa ubora	Tutatafiti ili kuongeza kipengele cha ukaguzi wa ubora	Hii itatekelezwa katika mwaka ujao wa fedha katika mwezi Disemba 2013.	<ul style="list-style-type: none"> Tunafikiri kwamba utaratibu unaotumika sasa katika idara ni mzuri katika mazingira yetu na uendelee kutumika 	

S/N	Ukurasa	Hoja ya Ukaguzi	Jibu la Wizara	Mpango wa utekelezaji	Hali ya utekelezaji hadi kufikia tarehe 04 Machi, 2013	Maoni
					kama ulivyo.	
13	98	Ukokotoaji wa kodi ya ongezeko la thamani usio sahihi	Tunakubaliana na matokeo ya wakaguzi na tutafanya uchambuzi zaidi kuona jinsi ya kututua tatizo hilo.	Ukokotoaji wa Kodi ya Ongezeko la Thamani utakuwa ukifanyika kupitia mfumo wa Kompyuta wakati wa uboreshaji wa mtandao kutoka Epicor 7.3.5 kwenda Epicor 9.05.	<ul style="list-style-type: none"> Kwa kuwa uboreshaji wa Epicor unaendelea, ukokotoaji wa Kodi ya Ongezeko la Thamani nao utajumuishwa wakati wa uboreshaji 	Utekelezaji unaende lea
14	99	Usuluhihi kati ya taarifa zilizoko kwenye rejista ilioandikwa kwa mkono na taarifa zilizo ingizwa kwenye mfumo wa kompyuta ulibaini kuwa zilikuwa zikitofautiana.	Tumeyaona makosa hayo na tutayafanyia kazi ikiwa ni pamoja na kuanda rejista itakayokuwa inatumika kwenye ofisi za Serikali Kuu na waraka utatolewa ili kuhakikisha utekelezaji wake.	Taarifa zilizoko kwenyerejista ilioandikwa kwa mkono zitatakiwa kuwa sawa na taarifa zitakazo ingizwa kwenye mfumo wa kompyuta. Pia elimu itatolewa kuhusu uandaaji mzuri wa rejista hiyo kwenye ofisi za Serikali Kuu ili kuondoa mapungufu yaliyojiteza.	SDU wametoa mafunzo kwa watumiaji jinsi ya kuandaa rejista hiyo ili tuweze kuondoa mapungufu yaliyojiteza.	Uboreshaji unaende lea
16	115	Hakuna idhini iliyotolewa kufanya usuluhihi wa benki pasipo kutumia mfumo wa	Tumeyaona maoni yaliyotolewa na tutayafanyia kazi ili kuboresha	Mchakato wa kuboresha utendaji kazi kukamilika	Tatizo la usuluhihi usiotumia mfumo wa kompyuta ulizingatiwa tulipokuwa	Utekelezaji unaende lea

S/N	Ukurasa	Hoja ya Ukaguzi	Jibu la Wizara	Mpango wa utekelezaji	Hali ya utekelezaji hadi kufikia tarehe 04 Machi, 2013	Maoni
		kompyuta	maeneo yanayo husu usuluhisho wa benki na kubaini udhibiti wake.	Disemba, 2012	tunafanya mabadiliko ya toleo jipya Na. 9.05 la mtandao wa Epicor	
17	118	Kumbukumbu za rejea zisizo sahihi.	Tumekubalianana maoni yaliyotolewa. Mbali ya kufanyika kwa utafiti wa maboresho katika utendaji kazi tutafanya mafunzo stahili pamoja na kununua vifaa vyatufanya mchanganuo kama IDEA	Utafiti wa maboresho katika utendaji kazi utafanyika Disemba, 2012	Kufuatia uanzishaji wa TISS suala la programu ya kompyuta ya IDEA inakuwa haina maana tena. Mafunzo kuhusu usuluhisho yameshafanyika. Mafunzo hayo yatakuwa endelevu.	IUtekelezaji unaende lea

S/N	Ukurasa	Hoja ya Ukaguzi	Jibu la Wizara	Mpango wa utekelezaji	Hali ya utekelezaji hadi kufikia tarehe 04 Machi, 2013	Maoni
18	119	Mfumo kuchukua taarifa za malipo zisizo sahihi	Pamoja na kupitia taratibu za utendaji kazi wa mfumo, pia tutazihusisha benki ili kuhakikisha kwamba Serikali na benki tunaingiza taarifa zinazofanana wakati wa kufanya malipo.	Zoezi la kupitia taratibu za utendaji kazi wa mfumo lilifanyika Juni, 2011	<ul style="list-style-type: none"> Kufuatia uamuzi wa Benki Kuu kutaka malipo yote yafanyike kwa njia ya kielektroniki yaani TISS, utumiaji wa mfumo wa kompyuta wa IDEA hautahitajika tena kwa kuwa baadhi ya matatizo mengine yaliyotolewa taarifa yametatuliwa na TISS. Mafunzo ya kufanya suluhishoza benki yamekwisha fanyika. Mafunzo haya yatakuwa yakifanywa mara kwa mara 	Inaendel ea kufanyi wa kazi
19	120	Taarifa za malipo zenye namba za kumbukumbu zinazofanana ambazo hazikusuluhishwa	Tunakubaliana na mapendekezo ya mkaguzi, mapitio yatafanyika ili kupata ufumbuzi wa tatizo hilo.	Uchambuzi thabiti wa tatizo hili unafanyika ili kupata ufumbuzi wa tatito hili kufikia	Ufumbuzi wa tatizo hili umepatikana kutokana na kubadilishwa kwa mfumo wa sasa na kuwa Epicor 9.5	Inaendel ea kufanyi wa kazi

S/N	Ukurasa	Hoja ya Ukaguzi	Jibu la Wizara	Mpango wa utekelezaji	Hali ya utekelezaji hadi kufikia tarehe 04 Machi, 2013	Maoni
				Disemba, 2012		
20	121	Kuanzishwa kwa utaratibu wa kufanya malipo benki kwa njia ya kielectroniki(EFT)	Tunakubaliana na mapendeleko ya mkaguzi. Tutafanya usuluhishi wa benki kwa kushirikisha mabenki ili kutatua suala la kumbukumbu za malipo.	Uchambuzi thabiti wa EFT ulifanyika Disemba, 2012 Utekelezaji wa EFT utatoa ufumbuzi wa tatizo hili.	<ul style="list-style-type: none"> • Kwa Wizara zilizopo DaresSalaam, malipo yanafanya kupita EFT(TISS). Hili limewezesha usuluhishi wa kila siku wa malipo na makusanyo kufanyika • Kwa vituo ambayyo viko mikoani, utaratibu huu wa EFT utatekelezwa ndani ya mwaka wa fedha 2013/14 	Inaendelea kufanyi wa kazi
23	134	Kukosekana kwa ufahamu wa usalama wa mifumo ya kompyuta	Tunakubaliana na mapendeleko ya mkaguzi. Sera ya usalama wa mifumo ikikamilika tutaanza kutoa mafunzo kuhusu uelewa wa usalama wa mifumo ya kompyuta	Mafunzo kuhusu uelewa wa usalama wa habari na Mifumo ya Kompyuta utatolewa ndani ya mwaka wa fedha ujao (2013/14)	Mwongozo wa Usalama wa habari na mifumo ya kompyuta wa Wizara umekamilika hivi karibuni. Uelewa wa wafanyakazi juu ya Usalama Habari na Mifumo ya Kompyuta utatolewa	Inaendelea kufanyi wa kazi

S/N	Ukurasa	Hoja ya Ukaguzi	Jibu la Wizara	Mpango wa utekelezaji	Hali ya utekelezaji hadi kufikia tarehe 04 Machi, 2013	Maoni
24	136	Kukosekana kwa kanuni na mafunzo juu ya kukabiliana na dharura	Tunakubaliana na mapendekezo ya wakaguzi na uongozi utaandaa na kuendesha mafunzo kwa watumishi kuhusu namna ya kukabiliana na dharura.	Mwongozo uliothibitishwa kuhusu usalama kwa masuala ya TEHAMA utaelezea utaratibu wa namna ya kukabiliana na dharura.	Mwongozo wa Wizara juu ya masuala ya usalama wa TEHAMA umeshakamilika na taratibu za mafunzo ziko mbioni kutolewa.	Utekelezaji unaende lea
26	143	Ukosefu wa mafunzo kwa mtaalam wa Teknolojia ya Mawasiliano	Tumeshapanga wataalam wa Teknolojia ya habari kwenye vitengo vitatu tofauti na kutokana na mgawanyo huu, wataalam hawa wataanza kupata mafunzo kulingana na mahitaji ya fani zao. Mfano, kitengo cha masuala mtandao, maendeleo na utendaji. Uanishwaji wa mahitaji ya mafunzo sambamba na utekelezaji utafanyika baada ya kuwapata washauri kutoka nje.	Mafunzo ya watumishi wa SDU kwa kozi za muda mfupi yatafanyika mwaka 2013. Utaratibu huu wa mafunzo utakuwa ni wa kudumu.	<ul style="list-style-type: none"> Kundi la wataalam wanaohusika na maendeleo walihudhuria mafunzo juu ya uandaaji na uchamodzi wa mifumo yaliyofanyika Swaziland, Oktoba 2010. Kundi jingine lilihudhuria kozi ya Uhakiki wa Ubora wa Mifumo, Uganda. Wataalam 6 kutoka SDU walihudhuria kozi ya wiki mbili juu ya masuala ya mtandao na Seva yaliyofanyika Julai 2011 	Utekelezaji unaende lea

S/N	Ukurasa	Hoja ya Ukaguzi	Jibu la Wizara	Mpango wa utekelezaji	Hali ya utekelezaji hadi kufikia tarehe 04 Machi, 2013	Maoni
					<p>India.</p> <ul style="list-style-type: none"> • Wataalam 33 walipatiwa mafunzo juu ya matumizi ya mfumo wa kihasibu wa Epicor toleo la 9.05 Aprili 2012 kabla ya mfumo huo mpya kuanza kutumika. • Wataalam wengine watatu walipata mafunzo ya uandishi wa lugha za kimfumo kwa kutumia mpango wa lugha wa 'C Sharp' Machi 2013. 	
29	150	Kukosekana kwa utaratibu wa kukabiliana na majanga.	Mwongozo wa namna ya Kukabiliana na Majanga (DRP) upo katika hatua ya rasimu kama ilivyoelezwa hapo awali.	Mwongozo wa namna ya Kukabiliana na Majanga (DRP) utaandalowiwa kwa kuzingatia yaliyomo kwenye Mwongozo wa usalama wa masuala ya TEHAMA na kuwasilishwa	<ul style="list-style-type: none"> • Kufuatia kukamilika kwa Muongozo wa usalama wa masuala ya TEHAMA, uandaaji wa Muongozo wa namna ya Kukabiliana na Majanga (DRP) utaweza kuandaliwa 	Utekelezaji unaende lea

S/N	Ukurasa	Hoja ya Ukaguzi	Jibu la Wizara	Mpango wa utekelezaji	Hali ya utekelezaji hadi kufikia tarehe 04 Machi, 2013	Maoni
				kwa wadau wote.	sasa.	
32	154	Kutokuwepo kwa njia mbadala za mawasiliano.	Uongozi unakubaliana na mapendeleko ya wakaguzi na tumeanza kuchukua hatua mbalimbali kuboresha njia za mawasiliano ikiwemo kuwepo kwa njia mbadala.	Lengo ni kuwa na mawasiliano kupitia kampuni ya simu ya TTCL na kwa kutumia mkongo wa Taifa kwa mikoa yote na VSAT kama kituo cha utunzaji wa kumbukukumbu	<ul style="list-style-type: none"> • Mpaka sasa ni ni mkoa wa Dodoma tu uliouunganishwa kwa majaribio; mae neo mengine yatafuata kama ilivyoainishwa kwenye Hadimu za Rejea 	Utekelezaji unaende lea

SURA YA 3

MAKUSANYO YA MADUHULI NA MCHANGANUO WA FEDHA ZA MATUMIZI YA KAWAIDA NA MAENDELEO

3.0 Utangulizi

Sehemu hii inatoa mchanganuo wa kina wa fedha zilizotolewa kwa Wizara, Idara na Sekretarieti za Mikoa kwa mwaka 2010/2011 na 2011/2012. Kiasi kikubwa cha fedha zinazotolewa kwa Wizara, Idara na Sekretarieti za Mikoa kinatoka Mfuko Mkuu wa Serikali kuitia Hazina.

3.1 Ulinganisho wa fedha kutoka Mfuko Mkuu wa Serikali na matumizi halisi ya Kawaida katika Wizara, Idara na Sekretarieti za Mikoa


Kumbukumbu zinaonyesha kwamba, jumla ya fedha zilizotolewa na Hazina kwa ajili ya matumizi ya kawaida katika mwaka wa fedha 2010/2011 zilikuwa Sh. 7,587,424,923,903 wakati matumizi halisi yalikuwa Sh. 7,581,154,383,395. Kwa upande mwingine, fedha zilizotolewa na Hazina kwenda Wizara, Idara na Sekretarieti za Mikoa katika mwaka wa fedha 2011/2012 zilikuwa Sh. 8,687,230,788,550 wakati matumizi halisi yalikuwa ni Sh. 8,685,275,162,094 (**Kiambatisho II**)

Muhtasari wa mchanganuo huu ni kama ifuatavyo:

Jedwali 7: Ulinganisho wa fedha zilizotolewa na matumizi halisi

	2010/2011	2011/2012
Fedha zilizotolewa (Sh)	7,587,424,923,903	8,687,230,788,550
Matumizi halisi (Sh)	7,581,154,383,395	8,685,275,162,094
Tofauti (Sh)	6,270,540,508	1,955,626,456

Pia taarifa hiyo hapo juu imeonyeshwa katika chati mhimili hapa chini:



3.2 Ulinganisho wa Fedha za Matumizi ya Kawaida na Maendeleo zilizotolewa na Hazina kwa ajili ya Wizara na Idara za Serikali kwa kipindi cha 2010/2011 na 2011/2012

Kumbukumbu zinaonyesha kwamba jumla ya fedha zilizotolewa kutoka Mfuko Mkuu wa Serikali kwa mwaka 2010/2011 kwa ajili ya matumizi ya kawaida ni Sh 7,587,424,923,903 na matumizi ya maendeleo yalikuwa Sh. 2,223,684,150,465 na kufanya jumla ya fedha zilizotolewa kwa ajili ya matumizi ya kawaida na matumizi ya maendeleo kuwa sh. 9,811,109,074,368. Halikadhalika, mchnganuo unaonyesha kuwa kiasi kilichotolewa kwa ajili ya matumizi ya maendeleo ni asilimia 23 na matumizi ya kawaida yalikuwa asilimia 77.


Kwa upande mwingine, fedha zilizotolewa kwa ajili ya matumizi ya kawaida kwa mwaka 2011/2012 ni Sh 8,687,230,788,550 na matumizi ya maendeleo zilikuwa Sh 3,384,431,758,346 na kufanya jumla ya fedha zote zilizotolewa kufikia Sh 12,071,662,546,896. Mchanganuo huu pia unaonyesha kuwa asilimia 72 ya fedha zote zilitolewa kwa ajili ya matumizi ya kawaida na asilimia 28 kwa matumizi ya maendeleo.

Mchanganuo huo umewekwa katika jedwali lifuatalo:

Jedwali 8: Ulinganisho wa fedha za matumizi ya kawaida na maendeleo

Fungu	2010/2011	%	2011/2012	%
Fedha za matumizi ya kawaida (Sh)	7,587,424,923,903	77	8,687,230,788,550	72
Fedha za matumizi ya maendeleo (Sh)	2,223,684,150,465	23	3,384,431,758,346	28
Jumla	9,811,109,074,368	100	12,071,662,546,896	100

Pia taarifa hiyo hapo juu imeonyeshwa kwenye chati mhimili kama ifuatayo:



3.3 Uwiano wa bajeti dhidi ya fedha zilizotolewana Hazinakwa ajili ya maendeleo katika Wizara na Idara

Bajeti iliyoidhinishwa kwa ajili ya miradi ya maendeleo katika Wizara na Idara kwa mwaka 2010/2011 ilikuwa Sh. 3,750,684,569,000 ambapo kiasi cha Sh. 2,223,684,150,465 kilitolewa na Hazina ikiwa ni pungufu kwa Sh.1,527,000,418,535 sawa na asilimia 41.

Aidha, bajeti iliyoidhinishwa kwa ajili ya matumizi ya maendeleo kwa Wizara na Idara katika mwaka 2011/2012 ilikuwa Sh 4,311,009,394,737 ambapo fedha zilizotolewa na Hazina ziliwa Sh 3,384,431,758,346 ikiwa ni pungufu kwa Sh. 926,577,636,391 sawa na asilimia 21 ya fedha zilizoidhinishwa.


Muhtasari wa bajeti na fedha zilizotolewa kwa Wizara na Idara kwa kipindi cha miaka miwili ni kama ifuatavyo:

Jedwali 9: Ulinganisho wa bajeti dhidi ya fedha zilizotolewa na Hazina

Mwaka	Bajeti iliyoidhinishwa (Sh.)	Fedha halisi zilizotolewa (Sh.)	Tofauti (Sh.)	%
2010/2011	3,750,684,569,000	2,223,684,150,465	1,527,000,418,535	41
2011/2012	4,311,009,394,737	3,384,431,758,346	926,577,636,391	21

Kutokana na jedwali hapo juu, shuguli za maendeleo za jumla ya Sh 926,577,636,391 au asilimia 21 ya fedha zilizoidhinishwa hazikutekelezwa katika mwaka wa fedha 2011/2012 ikilinganishwa na Sh. 1,527,000,418,535 au asilimia 41 ambazo hazikutolewa katika mwaka 2010/2011.

Taarifa kwenye jedwali hilo hapo juu pia imeonyeshwa kwenye chati mhimili kama ifuatavyo:



Kutokana na uchambuzi na chati mhimili hapo juu, ni dhahiri kuwa kuna tatizo kubwa katika utoaji wa fedha za shughuli za maendeleo. Hata hivyo kwa mwaka huu wa fedha kumekuwa na ongezeko la utoaji wa fedha za maendeleo ambapo asilimia 21 ya fedha zote hazikutolewa ukilinganisha na asilimia 41 za mwaka jana.

3.4 Mamlaka ya Mapato Tanzania

Mamlaka ya Mapato Tanzania imeanzishwa kwa mujibu wa Sheria Na.11 ya mwaka 1995 kama ilivyorekebishwa na Sheria Na.8 ya mwaka 1996 ikiwa na majukumu ya kusimamia ukusanyaji wa kodi za Serikali kuu pamoja na ukusanyaji wa mapato mbalimbali ya Serikali. Mamlaka inatengeneza aina

mbili za Taarifa za Hesabu ambazo ni zile za Mapato na Taarifa ya Hesabu za Matumizi.

3.4.1 Ukusanyaji wa Mapato

Hesabu za Mapato zinaonyesha kuwa kiasi cha Sh6,703,229,704,887 kilikusanywa kwa Tanzania Bara ikilinganishwa na makisio ya Sh6,456,832,630,000ikiwa ni makusanyo ya ziada ya Sh 246,397,074,887sawa na asilimia 4% ya Makisio ya Mapato ya Mwaka.

Kwa upande wa Zanzibar,makusanyoyalikuwaSh . 91,652,054,954ikilinganishwa na Makisio ya Sh 100,581,100,000 na kufanya makusanyo pungufu kwa Sh 8,929,045,046sawa na asilimia 9% ya makisio ya Mapato ya mwaka.

Mchanganuo wa makusanyo ya mapato yaliyokusanywa na Mamlaka ya Mapato Tanzania kwa idara ni kama ifuatavyo:-

Jedwali 10 (a): Tanzania Bara

Idara (a)	Lengo (a) Sh.	Makusanyo halisi (b) Sh.	Ziada/pungufu ya makusanyo (c) = (b-a) Sh.	£ (c/a)
Idara ya Kodi za Ndani	1,123,693,100,000	1,256,579,867,689	132,886,767,689	12
Idara ya Walipa kodi Wakubwa	2,556,980,930,000	2,799,745,044,459	242,764,114,459	9.5
Ushuru wa Forodha	2,742,213,500,000	2,609,406,122,613	-132,807,377,387	(5)
Jumla ndogo	6,422,887,530,000	6,665,731,034,761	242,843,504,761	4
Ongeza: Vocha za Hazina	33,945,100,000	37,498,670,126	3,553,570,126	10
Jumla Kuu	6,456,832,630,000	6,703,229,704,887	246,397,074,887	4

Jedwali 10(b): Zanzibar

Idara	Lengo (a) Sh.	Makuanyo halisi (b) Sh.	Ziada/Pungufu ya Makusanyo (c) = (b-a) Sh.	% (c/a)
Idara ya Kodi za ndani	49,442,300,000	32,553,852,450	(16,888,447,550)	(34)
Ushuru wa Forodha	51,138,800,000	59,098,202,504	7,959,402,504	16
Jumla	100,581,100,000	91,652,054,954	8,929,045,046	(9)


Mwelekeo wa makusanyo ya mapato kwa pande mbili za Serikali - yaani Tanzania Bara na Zanzibar kwa miaka mitatu mfululizo ni kama ifuatavyo:-

Jedwali 11(a): Mwelekeo wa Makusanyo ya Mapato - Tanzania Bara

Mwaka	Lengo (a) Sh.	Makusanyo halisi (b)Sh.	Tofauti (c) = (b-a) Sh.	% (c/a)
2009/2010	5,028,922,100,000	4,637,686,999,618	(391,235,100,382)	(7.78)
2010/2011	5,849,093,700,000	5,550,205,244,378	(298,888,455,622)	(5.11)
2011/2012	6,456,832,630,000	6,703,229,704,888	246,397,074,888	4

Mwelekeo huo wa makusanyo unaweza kuonyeshwa katika chati mhimili kama ifuatavyo:

MWELEKEO WA MAKUSANYO KWA MIAKA MITATU




Jedwali 11(b): Mwelekeo wa Makusanyo ya Mapato - Zanzibar

Mwaka	Lengo (a) Sh.	Makusanyo Halisi (b) Sh.	Tofauti (c) = (b-a) Sh.	% (c/a)
2009/2010	63,234,200,000	59,998,034,392	(3,236,165,608)	(5.12)
2010/2011	69,240,800,000	76,357,574,602	7,116,774,602	10.28
2011/2012	100,581,100,000	91,652,054,954	(8,929,045,046)	(9)

Mwelekeo huo wa makusanyo kwa upande wa Zanzibar unaweza kuonyeshwa katika chati mhimili kama ifuatavyo:

MWELEKEO WA MAKUSANYO KWA MIAKA MITATU



Ukusanyaji wa mapato kwa kipindi cha miaka mitatu kwa upande wa Tanzania bara umeonyesha kuwa kuna ongezeko la makisio ya makusanyo sambamba na ongezeko la makusanyo. Makusanyo katika mwaka huu wa fedha yameongezeka na kuvuka malengo kwa asilimia 4 ikilinashwa na makusanyo pungufu ya asilimia 8 kwa mwaka 2009/2010 na asilimia 5 kwa mwaka 2010/2011.

Kwa upande mwingine makadirio na makusanyo ya kodi kwa Zanzibar yameendelea kuongezeka mwaka hadi mwaka. Hata hivyo kwa mwaka huu wa fedha kumekuwa na ongezeko kubwa la makisio ikilinganishwa na miaka iliyopita na kusababisha makusanyo pungufu kwa asilimia 9

Misamaha ya Kodi Sh.1,806,203,559,828.

Taarifa za Mapato kwa mwaka unaoishia tarehe 30, Juni 2012 zimeonyesha kuwa kiasi cha Sh. 1,806,203,559,828 kilikuwa ni misamaha ya kodi iliyotolewa kwa Taasisi mbali mbali na watu binafsi kama inavyoonekana hapa chini:

Jedwali 12: Muhtasari wa misamaha ya kodi kwa Taasisi mbalimbali

Taasisi	Idara ya Forodha (Sh)	Idara ya Kodi za ndani (Sh)	Jumla (Sh) 2011/2012	Jumla (Sh) 2010/2011
Taasisi za Serikali	9,603,414,035	-	9,603,414,035	35,867,200,000
Mashirika ya Umma	15,699,616,106	-	15,699,616,106	8,131,200,000
Taasisi za Kidini	438,967,358	-	438,967,358	1,569,300,000
Taasisi zisizo za Kiserikali	7,542,700,000	-	7,542,700,000	25,462,600,000
Balozi za nje	10,194,000,000		10,194,000,000	
Misamaha ya kodi kwenye maduka ya jeshi	2,454,600,000		2,454,600,000	
Miradi ya Wafadhilli	225,039,689,862	-	225,039,689,862	115,758,100,000
Makampu ni na watu binafsi	304,045,656,449	-	304,045,656,449	182,706,100,000
Sekta ya Madini	140,637,400,000	-	140,637,400,000	109,885,900,000
Kituo cha Uwekezaji Tanzania	280,961,890,898		280,961,890,898	239,667,300,000
Misamaha ya kodi za Ongezekola Thamani		801,859,518,440	801,859,518,440	279,845,200,000
Misamaha ya Kodi katika Maduka yasitozwa kodi	-	7,726,106,679	7,726,106,679	17,427,400,000
Jumla	996,617,934,708	809,585,625,119	1,806,203,559,827	1,016,320,300,000

Mwenendo wa misamaha unaonyesha ongezeko la Sh.789,883,259,827 sawa na asilimia 78 kutoka Sh.1,016,320,300,000 zilizosamehewa kwa kipindi cha mwaka wa fedha 2010/2011 hadi Sh1,806,203,559,827 mwaka 2011/2012.

Endapo kiasi hiki cha Sh 1,806,203,559,827 ambacho ni sawa na asilimia 27 ya makusanyo yote kingekusanya, makusanyo yote


yangekuwa Sh.8,509,433,264,717 badala ya Sh.6,703,229,704,888. Misamaha ya kodi iliyotolewa kwa mwaka huu ni sawa na asilimia 13 ya bajeti yote ya mwaka 2011/2012 ya Sh.13,525,895,350,000.

Kwa ujumla, misamaha ya kodi kwa Tanzania Bara imeongezeka kwa mwaka wa fedha unaoishia tarehe 30 June 2012 ikilinganishwa na mwaka uliopita na kuathiri ufanisi katika makusanyo kama ifuatavyo:

Jedwali 13: Mwelekeo wa misamaha ya kodi

Maelezo	2011/2012 (Sh)	2010/2011 (Sh)
Makusanyo Halisi	6,703,229,704,887	5,550,205,244,378
Misamaha	1,806,203,559,827	1,016,320,300,000
Asilimia ya Misamaha kwa makusanyo Halisi	27%	18%
Pungufu la Makusanyo	246,397,074,887	(298,888,455,622)
Ziada kama misamaha isingetolewa	2,052,600,634,714	717,431,844,378

Mwelekeo huo wa makusanyo kwa upande wa Zanzibar unaweza kuonyeshwa katika chati mhimili kama ifuatavyo:



3.5 Uwiano Kati ya Misamaha ya Kodi, Makusanyo na Pato la Taifa

Mwelekeo unaonyesha kuwa wakati makusanyo yamekuwa yakiongezeka kwa kipindi cha miaka mitano kutoka shilingi million 3,378,793.7 mwaka 2007/2008 hadi shilingi million 6,703,230 zilizokusanya mwaka 2011/2012, misamaha ya kodi imeongezeka kutoka asilimia 3.5 kwa mwaka 2007/2008 hadi asilimia 4.3 ya pato la taifa kwa mwaka 2011/2012.

Kiwango cha misamaha ya kodi kimekuwa kwenye wastani wa asilimia 3.5 ya pato la taifa kati ya mwaka 2007/2008 na 2007/2008 kabla kushuka hadi asilimia 2.1 ya pato la taifa mwaka 2009/2010 na kupanda tena hadi asilimia 2.9 mwaka 2010/2011 na asilimia 4.3 mwaka 2011/2012.

Jedwali 14: Uwiano wa mapato baada ya misamaha ya kodi dhidi ya pato la Taifa

Maelezo	2007/08	2008/09	2009/10	2010/2011	2011/2012
Pato la taifa	22,782,917.1	26,868,213.4	31,316,223.9	35,026,679	41,125,313
Makusanyo	3,378,793.7	4,051,963.8	4,437,933.4	5,315,148	6,703,230
Asilimia ya makusanyo dhidi ya pato la taifa	14.8%	15.1%	14.2%	15.2%	16.3
Jumla ya misamaha ya kodi	795,856.5	731,267.7	653,652.5	1,016,320.3	1,806,203.6
Asilimia ya misamaha ya kodi dhidi ya pato la taifa	3.5%	2.7%	2.1%	2.9%	4.3%
Asilimia ya misamaha ya kodi dhidi ya makusanyo	23.6%	18.0%	14.7%	19%	27%

Chanzo: Taarifa za fedha za Mamlaka ya Mapato kwa mwaka 2011/2012 Tathmini ya viashiria hasi vyta misamaha ya kodi Kwa mwaka 2006/2007 - 2009/2010

Jedwali hapo juu linaonyesha kuwa misamaha ya kodi iko juu na bado inendelea kuongezeka hasa ikichukuliwa kuwa serikali inahitaji kuongeza mapato. Pamoja na jitihada zinazochukuliwa kupunguza misamaha ya kodi, imeonekana kuwa hakuna viwango na miongozo iliyowekwa kuonyesha kikomo cha misamaha ya kodi ambacho hakitakiwi kuzidi.

Ili kuongeza makusanyo ya kodi na kuboresha usimamizi wa misamaha ya kodi, Serikali inatakiwa kuweka ukomo wa misamaha ya kodi na kuhakisha kuwa misamaha haitolewi zaidi ya kikomo kilichowekwa.

Ninatambua kuwa misamaha ya kodi ni nyenzo muhimu katika kukuza uwekezaji na uchumi wa nchi kwa ujumla, hata hivyo ni lazima ijulikane kuwa hii haina maana ya kutokusimamia

misamaha hii kwa lengo la kubaini miradi inayohitaji misamaha na ambayo haihitaji.

- 3.6 Matokeo ya utafiti wa uboreshaji wa mapato ya taifa**
Kifungu cha 12 cha Sheria ya Ukaguzi wa Umma ya mwaka 2008 inanitaka kuishauri serikali kwa malengo yafuatayo:
- (a) Kuzuia au kupunguza matumiza yasiyo na tija
 - (b) Kuongeza makusanyo ya serikali, na
 - (c) Kuzuia upotevu wa fedha za serikali aidha kwa uzembe, wizi, kukosa uaminifu, udanganyifu au rushwa

Aidha kifungu cha 33 cha sheria hiyo kinaniruhusu kumruhusu mtu ye yote inayestahiki kufanya kazi ya ukaguzi kuifanya kwa niaba yangu.

Kutokana na mamlaka niliyopewa kisheri, niliipa kazi kampuni ya Ernst & Young (Mshauri), kufanya utafiti na kushauri njia bora ya kusimamia misamaha ya kodi na kubaini vyanzo zaidi vya kodi . Mkazo pia uliwekwa kwenye mapato yasiyo ya kodi yanayokusanywa na Wizara mbalimbali; kodi za sekta isiyo rasmi; mchango wa mapato yakanayo na wakala wa serikali na makusanyo ya mapato kutoka sekta ya mawasiliano ya simu.

Kwa mujibu wa kifungu cha 12 cha Sheria ya Ukaguzi wa Umma Namba 11 ya 2008 na kwa kuzingatia matokeo ya ripoti ya mshauri, mapendekezo yangu kwa serikali juu ya jinsi ya kusimamia na kuzuia misamaha isiyo ya lazima na kuongeza vyanzo vya mapato kwa lengo la kuboresha mapato ya serikali ni kama ilivyoonyeshwa kwa muhtasari katika sura ya 8

Maeneo yanayoathiri ukusanyaji wa mapato na ambayo yanahitaji uboresha ni kama ifuatavyo:

3.6.1 Misamaha ya kodi

Misamaha ya kodi inatolewa kwa walengwa tofauti kwa sababu mbalimbali,kama vile kijamii, kiuchumi, kisiasa au makubaliano ya kimataifa(nchi na nchi au ya kimataifa). Katika baadhi ya matukio,misamaha ya kodi au makubaliano ya kodi yanatolewa

kama sehemu ya likizo ya kulipa kodi ili kuchochaea maendeleo ya kiuchumi kwa mfano misamaha ya kodi inayotolewa kwa makampuni ya madini na motisha katika kodi inayotolewa kwa wawekezaji walioandikishwa na Kituo cha Uwekezaji Tanzania(TIC)

Kuna njia kuu mbili ambazo misamaha ya kodi inatolewa kama ilivyoainishwa hapa chini:

(i) Misamaha ya kodi inayotolewa chini ya sheria za kodi ambazo ni:

- Sheria ya Usimamizi wa Ushuru wa Forodha ya Afrika Mashariki (Kifungu cha 5)
- Sheria ya Kodi ya Ongezeko la Thamani (Jedwali la 2 & 3)
- Sheria ya kodi ya Mapato (Kifungu cha 10 na jedwali la 2)
- Sheria ya Ushuru wa Barabara na Mafuta (kifungu cha 8)
- Sheria ya Usimamizi wa Ushuru wa bidhaa za ndani (Kifungu cha 128 (2)

(ii) Misamaha ya kodi inayotolewa kwa utaratibu wa notisi ya serikali (Government Notices (GN))

Notisi ya Serikali inatambua misamaha ya kodi ambayo haipo kisheria mfano iliyoko kwenye mikataba ya miradi inayofadhiliwa na wafadhili,miradi ya Millennium Challenge Corporation (MCC),fedha zilizotengwa kwa ajili ya majanga ya asili na kadhalika.

Mpango ulifanyika kupunguza misamaha ya kodi mwaka 2009 ambapo serikali ilifuta zaidi ya ilani za serikali 500, ikiwa ni pamoja na zile za tangu mwaka 1961.Pamoja na hayo,Serikali kupitia Katibu Mkuu Ofisi ya Rais imetoa mwongozo kwa wizara na idara zote za serikali zisiingie mkataba wenye vifungu vyya kusamehe kodi.

(a) Utaratibu wa Kituo cha Uwekezaji Tanzania(TIC) wa kutoa vyeti vyya motisha

Kituo cha Uwekezaji Tanzania kinatoa motisha kwa wawekezaji wakati wa kuanzisha biashara Tanzania.Kama mwezeshaji wa

wawekezaji, TIC inawasiliana na wizara na idara mbalimbali za serikali ili kufanikisha hilo.

Vyeti vinavyotolewa kwa wawekezaji vinasimamiwa kwa karibu na TIC kupitia mpango unaojulikana kama "After Care Services" ambayo mwangalizi anasimamia Maendeleo ya miradi ili kujiridhisha kwamba motisha inayotolewa haitumiwi vibaya. Ikidhibitika kwamba motisha inatumiwa vibaya, TIC inachukua hatua muhimu ikiwa ni pamoja na kufuta vyeti vilivyotolewa. Hata hivyo wakati wa ukaguzi hakuna udhibitisho ulioonekana kwamba kuna vyeti vilivyofutwa kwa wawekezaji waliotumia vibaya motisha hiyo ya misamaha ya kodi.

(b) Utaratibu wa kodi katika sekta ya madini ulianzishwa mwaka 1997 kufuatia sera ya serikali iliyotoa sababu ya kuwa na utaratibu maalumu wa kutoza kodi katika eneo hilo la madini. Marekebisho haya ya sera yaliwezesewa na kuanzishwa kwa sheria ya fedha ya mwaka 1977. Marekebisho haya yaliingizwa katika sheria husika za kodi mfano Sehemu III ya jedwali la pili la Sheria ya Kodi ya mwaka 1973 inayohusu misamaha inayotolewa katika mitaji iliyowekezwa nchini.

Sheria ya madini ya mwaka 1998 na Sheria ya Kodi ya mwaka 2004 zinasimamia utaratibu wa kutoza kodi katika eneo la madini. Pia kuna misamaha katika Sheria ya Ongezeko la Thamani ya mwaka 1997. Kodi mbalimbali ikijumuisha kodi za mafuta zinazojulikana kama tozo ya mafuta pia zinasamehewa katika Mikataba ya Uchimbaji Madini kati ya Serikali na mwekezaji inayosainiwa kwa kila leseni nayotolewa.

Utaratibu wa kutoza kodi katika sekta ya madini kulingana na Sheria ya Madini ya mwaka 1998 unajumuisha yafuatayo:

- i. Mrahaba wa 5% kwenye almasi na 4% kwenye madini mengineyo.
- ii. 30% kama kodi ya mapato ya kibiashara

- iii. 100% ya matumizi yote ya maendeleo yanayotegemewa au yaliyo kwisha fanyika.
- iv. 3% kama zuijio la kodi za huduma za kiufundi
- v. 3% kama zuijio la kodi za usimamizi hadi 2% ya gharama za uendeshaji na 20% kama zuijio la kodi zaidi ya 2% ya gharama za uendeshaji.
- vi. hakuna zuijio la kodi katika riba zinazotozwa katika mikopo ya fedha za kigeni kutoka kwa watu wasiokuwa katika mkataba unaozihusisha pande mbili zilizo saini mkataba huo.
- vii. Kufidiwa hasara kusiko kuwa na kikomo
- viii. Matumizi ya maendeleo ambayo hayajafutwa kuongezwa kwa 15% kila mwaka
- ix. Hakuna kikomo katika kufadhili gharama za uwekezaji kwa mkopo
- x. Punguzo la kodi kwa mwaka husika kwa ajili ya malipo yaliyofanyika au yanayo tegemewa kufanyika kwa ajili ya kuhifadhi mazingira
- xi. Kikomo cha msamaha wa tozo ya mafuta wa Dolla za Kimarekani 200,000
- xii. Misamaha ya kodi ya forodha toka kipindi kabla ya uzalishaji kuanza na ndani ya kipindi cha mwaka wa kwanza wa uzalishaji na kiwango cha mwisho cha tozo cha 5% kwa kipindi kinachoendelea.
- xiii. Misamaha ya kulipa kodi ya ongezeko la thamani kwa vitu vinavyoingizwa nchini na vinavyo nunuliwa nchini.

(c) Taratibu za kusaini Mikataba ya Uchimbaji Madini

Utaratibu unaotumika katika kuingia mikataba ya uchimbaji wa madini umewekwa wazi katika Sheria ya Madini ya mwaka 2010. Sehemu ya 23 ya Sheria hiyo inaelezea kuhusu kuanzishwa kwa bodi itakayo julikana kama Bodi ya Ushauri ya Sekta ya Madini. Bodi hii inamshauri Waziri anayesimamia madini kuhusu masuala ambayo yako chini ya Sheria ya Madini ya mwaka 2010 ambayo yanatakiwa kufikishwa kwenye Bodi. Masuala haya yanahusisha:

- i. Kuomba na kupewa leseni ya uchimbaji katika eneo ambalo maombi yake yanafanywa kwa utaratibu wa zabuni.
- ii. Kuomba na kupewa haki ya kumiliki leseni ya uchimbaji
- iii. Kuomba na kupewa leseni maalumu ya uchimbaji wa madini
- iv. Mwenye leseni kufanya marekebisho ya leseni maalumu ya uchimbaji wa madini

Hata hivyo haikuwezekana kubainisha taratibu ambazo zinafuatwa na Wizara katika kutekeleza matakwa ya sheria hii kwa vile mikataba hii ya Uchimbaji ni ya watu binafsi na ni siri kwa watu wengine wasiokuwa sehemu ya mikataba hiyo. Kutokana na usiri huo, sikupewa haki ya kuipitia mikataba hiyo na hivyo kuzuia wigo wa ukaguzi wangu.

**(d) Utaratibu wa kusaini Makubaliano ya Uzalishaji wa Ubia
[Production Sharing Agreement (PSA)]**

Utafiti na maendeleo ya mafuta na gesi unasimamiwa na Sheria ya Mafuta (Utafiti na Uzalishaji) ya mwaka 1980 Cap 328 ya 2002.

Makampuni ya utafiti na maendeleo ya mafuta na gesi yalikuwa na makubaliano ya uzalishaji wa ubia pamoja na Shirika la Maendeleo ya Petroli Tanzania (TPDC).

Ibara ya 14 ya Makubaliano ya Uzalishaji wa Ubia inahusisha maeneo ya Kodi ya Mapato ambayo yanatakiwa kushughulikiwa kwa kuzingatia Sheria ya Kodi ya Mapato ya mwaka 2004.

Kodi zingine zinazo husishwa na sheria za kodi za utafiti wa mafuta na gesi zinastahili misamaha ya ushuru wa forodha na kodi za ndani kwa kulingana na Taarifa ya Serikali (Government Notice) Na. 10 ya tarehe 9 Januari 1998. Msamaha wa kodi ni kwa ajili ya mashine, vifaa, malighafi, na magari.

Hata hivyo, sikupatiwa taarifa zinazohusu misamaha ya kodi ya sekta ya mafuta na gesi. Ikizingatiwa kwamba kwa vile katika kipindi hiki utafiti wa mafuta na gesi unazidi kuongezeka nchini, ni muhimu taarifa sahihi za misamaha ya kodi katika sekta ya madini na gesi ziwekwe bayana.

(e) Changamoto zinazozuia kupunguza kutoa misamaha ya kodi.

- (i) Sheria ya Madini inampa uwezo Waziri husika wa madini kusaini Mikataba ya Uchimbaji Madini (MDA) inayotoa vivutio kwa wawekezaji. Hii inatoa misamaha kinyume na miongozo iliyotolewa na Katibu Mkuu Kiongozi. Aidha muungozo Na. 2010 wa Katibu Mkuu Kiongozi umeelezea utaratibu wa utoaji misamaha ya kodi. Hakukuwa na ushahidi kwamba Wizara ya Nishatina Madini ilifuata maelakezo ya mwongozo huo wakati wa wanasantini makubaliano na MDAs ya kutoa misamaha ya kodi.
- (ii) Kuna changamoto kupunguza vivutio walivyopewa wawekezaji wenye hati za TIC kwa mfano Mlimani City, Kagera Sugar na Mtibwa Sugar. Wawekezaji hawa wana mikataba na serikali katika baadhi ya miradi yenye makubaliano yenye misamaha. Changamoto zingine ni :
- Mikataba inaingiwa kupitia National Investment Steering Committee iliyoanzishwa na TIC
 - Sheria ya Kituo cha Uwekezaji (TIC Act) hailezi ukomo wa misamaha.
 - Hakuna sera au muongozo wa kutoa misamaha ambao unaeleza usimamizi wa misamaha.

Kadhalika, hakuna utaratibu wa kusimamia misamaha iliyotolewa. Sio rahisi kwa mamlaka zilizopo kuhakiki misamaha kama ilitumika kama ilivyo kusudiwa; kwa mfano hakuna udhibiti kuwa msamaha uliotolewa wa kuagiza mashine kwa ajili ya uwekezaji lakini mashine hizo baadae zikauzwa sokoni.

(f) Misamaha ya kodi katika sheria ya Kodi ya Mapato (ITA), 2004

Sheria ya Kodi ya Mapato namba 11 ya mwaka 2004 inaonyesha misamaha ya kodi katika kifungu cha 10. Kifungu hiki kinamwezesha Waziri wa Fedha kutoa msamaha wa kodi kupitia notisi ya serikali inayochapishwa katika gazeti la serikali.

Aidha, Jedwali la Pili katika Sheria ya Kodi ya Mapato linaonyesha orodha ya waliosamehewa kodi, makundi ya mapato na kadhalika. Kifungu hiki pia kinampa nguvu Waziri wa Fedha kurekebisha au kubadilisha Jedwali la Pili kwa kutoa notisi itakayochapishwa katika gazeti la serikali. Hivi sasa misamaha ya kodi iliyoonyeshwa katika Jedwali la Pili katika Sheria ya Kodi ya Mapato ambayo orodha ya makundi/taasisi tofauti 24 ambazo mapato yake yana msamaha wa kodi.

Kwa kutungwa kwa Sheria ya Kodi ya Mapato ya mwaka 2004, serikali imeweza kupunguza kiwango cha utoaji misamaha ya kodi. Katika kifungu cha 10(3), Sheria ya Kodi ya Mapato inahitaji kwamba mikataba yote iliyosainiwa baada ya tarehe 1 Julai, 2004 kutokupewa msamaha wa kodi.

Hata hiyo licha ya kuwepo kwa kifungu hicho, serikali imeendelea kusaini mikataba yenye kifungu kinachoonyesha misamaha ya kodi. Mfano ni mikataba wa MCC wa mwaka 2008.

(g) Kipimo cha udhibiti katika kubaini misamaha ya kodi isiyofaa

Mikataba yote yenye kifungu kinachoonyesha misamaha ya kodi inahitaji kupitiwa na Mwanasheria Mkuu wa Serikali kwa ushauri kabla ya kusainiwa na wahusika.

Kuanzishwa kwa kalenda ya matukio (mfano miaka mitatu) kwa wawekezaji kuelezea msamaha wa kodi walioupara ili kuiwezesha serikali kutathmini kama kuna faida katika kutoa misamahahiyo ya kodi.

(h) Misamaha ya kodi iliyotolewa kwa taasisi za kidini chini ya sheria ya Ushuru wa Forodha(Customs Duty Act) na TIC chini ya Sheria ya Mapato ya mwaka 2004

- Kuna wasiwasikama misamaha ya kodi iliyotolewa kwa baadhi ya taasisi za kidini ambazo zinaingiza zaidi magari inatumika vizuri.
- Misamaha ya kodi inakuwepo kwa sababu ya udhibiti mdogo katika misamaha ya kodi na hasa katika misamaha inayotolewa kwenye manunuzi ya vifaa kwa ajili ya shughuli za kidini na miradi ya uwekezaji ya TICmiongoni mwa wengine.Wasiwasi mkubwa ni katika utumiaji wa mwisho wa vifaa ambavyo vinaweza kuwa vimepelekwa katika matumizi ambayo hayakukusudiwa.Zaidi ya hayo,misamaha ya kodi iliyotolewa katika maduka yasiyo na ushuru, pia haina ufuatiliaji wa kutosha katika kuhakikisha kwamba misamaha iliyotolewa katika vifaa vilivyopata misamaha haviuzwi katika maduka mengine tofauti na yaliyopo katika viwanja vya ndege.

(i) Uzoefu wa msamaha wa kodi kutokaMauritius

Mauritius iliondoa karibia misamaha ya kodi zote kwa ajili ya makampuniukiondoa makampuni yote yaliyokuwa yameisha pewa misamaha hiyo ya kodi. Kivutio pekee kilichobaki kwa wawekezaji ni msamaha wa kodi wa miaka minne kwa kampuni ndogondogo pamoja na vikundi vya kazi za mikono chini ya sheria ya kulinda biashara ndogondogo ya Julai, 2005 iliyobuniwa ili kuvutia urasimishaji wa biashara ndogondogo zisizokuwa rasmi.

Pamoja na hatua hizo, kiwango cha kodi ya makampuni kilipunguzwa kutoka asilimia 25 mpaka asilimia 15 kuanzia Julai, 2007 ikiwa ni jitihada za kuoanisha na vivutio vya uwekezaji vilivyokuwepo kwa makampuni.Kiwango cha kodi ya mapato ya mshahara (PAYE), nacho kilibadilishwa na kuwa asilimia 15. Uwekezaji wa mojakwamoja kutoka nje uliongezeka kufuatia mabadiliko hayo na kusababisha ongezeko kuwa mara mbili ukilinganisha mwaka 2006 na ule wa 2005 ambalo lilikuwa asilimia 1.66 na likawa karibia

mara tatu kwa mwaka 2007 yaani kufikia asilimia 4.5 ya pato la taifa(GDP)

3.6.2 Utozaji kodi kwa sekta isiyokuwa rasmi

Katika kuchanganua ulipaji kodi wa sekta isiyokuwa rasmi, utafiti ulijikita katika ulipajikodi wachimbaji madini wadogowadogo, wakulima wadogowadogo na biashara ya utumaji wa pesa kwa njia ya simu za viganjani.

(a) Uzoefu kutoka kwenye jengo la machinga Dar es salaam
Jengo la machinga liko katikati ya Jiji la Dar es Salaam katika wilaya ya Ilala. Majengo yalijengwa na Halmashauri ya Jiji la Dar es Salaam (DCC) ambayo iliingia ubia na mfuko wa wafanyakazi (NSSF) kwa makubaliano kuwa DCC itakusanya mapato toka kwa wafanyabiashara wadogowadogo na kuilipa NSSF.

Lengo kuu la majengo hayo ilikuwa kuhakikisha kuwa kuna majengo ya kudumu kwa ajili ya wafanyabiashara wadogowadogo(machinga). Hata hivyo mradi ulipata changamoto nyingi ikiwemo ya uchache wa wateja wanaotembelea majengo hayo toka yalipoanza kutumika; Wateja wanaoingia kwenye majengo hayo ni wachache sana. Hali hiyo ilisababisha ugumu katika kufanya biashara na kusababisha wengi wa wafanyabiashara hao waondoke. Aidha, wafanyabiashara wadogo wadogo kuwa na mitaji midogo.

(b) Changamoto zinazojitokeza katika ukusanyaji wa kodi na mamlaka ya kodi

Wafanyabiashara(machinga) waliowengi hawana elimu rasmi ya ulipaji wa kodi. Kwa hiyo hakuna uwajibikaji wa hiari kwa sheria za kodi. Kukosekana kwa chanzo kinachoaminika cha taarifa za walipakodi kama vile machinga hawajajiandikisha na wala hawalazimiki kujandiandikisha au kuwa na namba ya mlipakodi pale wanapopewa sehemu ya kufanya biashara katika majengo hayo.

Kukosekana kwa miundombinu ya kibiashara inayoanisha kodi iliyolipwa. Hali hii imepelekea ulipaji wa kodi kwa hiari kuwa

chini sana. Kodi nyingi sana zinatozwa kwa mtu huyohuyo. Wafanyabiashara wadogowadogo wanatozwa kodi za aina nyingi kama vile; Kodi ya manispaa, kodi ya soko, kodi ya uwekaji bidhaa, kodi ya ulinzi n.k. ambazo kiukweli zinaondoa ari ya wafanyabiashara.

3.6.3 Wachimbaji wadogowadogo wa madini

Maombi ya leseni ya wachimbaji madini wadogowadogo zinapitishwa na maofisa wa Kanda - Wizara ya Nishati na Madini. Wakati wa maombi muombaji anatakiwa aainishe kwa maandishi sehemu na ukubwa wa eneo la uchimbaji lililoombwa:

(a) Aina ya leseni zinazotolewa:

- (i) Leseni za msingi za uchimbaji madini (hutolewa kwa wananchi wachimbaji madini pekee)
- (ii) Leseni ya mfanyabiashara (inatolewa kwa wananchi na wasio wananchi ambao wanunua madini na kuuza)
- (iii) Leseni ya madalali wa minada ya madini (hutolewa kwa wananchi pekee)

Wachimbaji madini wadogowadogo wanatakiwa kulipa mlahaba Serikalinikulingana na sheria ya madini ya mwaka 2010.

Hata hivyo, Wizara haiwezi kusimamia na kudhibiti uzalishaji na kuthaminisha vito/madini yaliyochimbwa na wachimbaji madini wadogowadogo kutokana na kutokuwa na uhakika wa muda wa uzalishaji. Mchimbaji anaweza kuchukua zaidi ya miaka miwili kabla ya kuanza kuzalisha. Hata wakati uzalishaji ukiwa tayari umeanza wachimbaji hawaweki wazi kiasi cha madini yaliyochimbwa. Zaidi ya hayo, Wachimbaji madini wadogowadogo hupewa Leseni za msingi za uchimbaji madini, hata hivyo hakuna udhibiti wa kujua vitaru vyenye uzalishaji mkubwa.

Wizara haina udhibiti wa kiasi cha madini kilichochimbwa yakiwa ni matokeo ya kutokuwa na udhibiti katika uzalishaji.

Wizara ya Nishati na Madini haina udhibiti juu ya ukubwa wa eneo la uzalishaji kwa vile inategemea taarifa zinazotolewa na wachimbaji.

Changamoto nyingine katika ukusanyaji wa mapato kutoka kwa wachimbaji madini wadogowadogo ni kama ifuatavyo:-

- (i) Wachimbaji,wafanyabiashara na wanadishaji wa madini hawalazimiki kuwa na TIN kwa mara ya kwanza wanapoomba leseni.
- (ii) Gharama kubwa za kudhibiti machimbo ya madini yaliyotawanyika maeneo mbalimbali.
- (iii) Wachimbaji hawatunzi hesabu kwahiyio inaleta changamoto katika kukadiria kiasi cha kutoza kodi kwani ni vigumu kuhakiki gharama za uzalishaji.
- (iv) Ugumu wa kudhibiti biashara ya magendo ya madini yanayofanyika kupitia barabara zinazokwenda nje jirani.
- (v) Kuna vitendo vya wenye vitalu vya uchimbaji wa madini kuhamisha haki zao kwa watu wengine.Utaratibu huo unahuusu uandikishaji wa uhamishohuo kwa Wizara ya Nishati na Madini.
- (vi) Wizara ya Nishati na Madini haina udhibiti wa viwanja vya ndege; hii inaleta changamoto katika kufanyika kwa biashara ya madini kwa magendo. Kazi hiyo ya udhibiti magendo hufanywa na mamlaka ya viwanja vya ndege.
- (vii) Ilibainika kuwa kwa sasa hakuna ushirikiano kati ya TRA na Wizara ya Nishati na Madini katika kukusanya mapato kutoka kwa wachimbaji.

3.6.4 Kumbi za Starehe (Harusi na mikutano)

Aina hizi za biashara zimekuwa zikiongezeka na kukua siku hadi siku katika maeneo ya mijini na kutoa mianya mingine ya kupata fedha. Aina hii ya biashara inategemea sanamaeneo na huduma zinazotolewa.Kumbi hizi zinazojitosheleza ni zile

zinazotoa huduma mbalimbali zikiwepo chakula, kumbi za mikutano na starehe kwa njia ya malipo. Malipo hutegemea eneo ukumbi ulipo, huduma zilizopo na kujitangaza.

Huduma za aina hii zinapatikana pia katika hoteli maarufu na za hali ya juu ambazo hutolewa kama mojawapo ya huduma za hoteli.

Hakuna kodi yoyote inayotozwa katika aina hizi za biashara. Kimsingi biashara hizi zinatakiwa zilipiwe kodi bila msamaha wowote.Hata hivyo kwa kuwa kumbi nyingine zipo katika maeneo yasiyofikika kuna angalizo kuwa kodi hii inaweza isiwe rahisi kukusanya.

3.6.5 Simu za viganjani na uhamishaji fedha kwa kutumia simu za viganjani (Mobile phone money transfer)

Simu za viganjani na uhamishaji wa fedha kwa kutumia simu hizo imekuwa ni biashara ya kawaida iliyanzishwa na makampuni mbalimbali kama vile Airtel, Tigo na Vodacom.Aina hizi za biashara zinajumuisha Airtel money,Tigo -pesa na M-pesa. Aina hii ya biashara imeenea maeneo mbalimbali ambayo ni maalum kwa shughuli za kiuchumi nchi nzima.

Mtoa huduma aliyesajiliwa kwa huduma zilizotajwa hapo juu anafaidika kwa kupata ujira kwa kutegemea idadi ya huduma alizotoa.

Pamoja na hayo,ujira unaolipwa ni kipato cha kawaida chini ya sheria ya kodi ya mwaka 2004 hivyo mapato hayo yanatakiwa kulipiwa kodi ya asilimia 30 kwa kampuni au kwa kiasi kinachotozwa kwa watu binafsi.

3.6.6 Aina nyinginezo za mapato yasiyotokana na Kodi

Mapato yasiyotokana na kodi inajumuisha mapato na matumizi kwa kutumia rasilimali za nchi au mali au fidia zinazotolewa na nchi kwa ajili ya watu waliopo kisheria.Hii inajumuisha matumizi ya rasilimali za nchi kama mapato yatokanayo na misitu, mapato yatokanayo na mauzo ya mali za serikali, mali zilizotaifishwa,zisizo na wenyewe,zilizorithiwa

kihalali, mauzo yatokanayo na mali zisizochukuliwa bandarini, na aina mbalimbali za tozo na usajili wa nembo za biashara.

3.6.7 Mapato yasiyona kodi kutoka kwenye Ardhi na Mali asili.

Uhamishaji wa hati za kumiliki viwanja na kodi ya ardhi ni eneo lingine linalochangia mapato yasiyo na kodi. Mapato haya yanakusanywa na Wizara ya Ardhi na Makazi na pia Mamlaka za Serikali za mitaa kwa niaba ya wizara.

3.6.8 Changamoto za ukusanyaji maduhuli kwenye maeneo haya;

- Kutokuwepo kwa kumbukumbu sahihi za viwanja vyenye majengo na visivyo na majengo nchi nzima.
- Kukosekana kwa uwajibikaji na utunzaji wa kodi za ardhi zinazokusanywa na serikali za mitaa.
- Wananchi kutoelewa vizuri tofauti kati ya kodi ya ardhi na kodi ya umiliki wa mali.
- Viwango vidogo vya kodi ya ardhi vinavyotumika vinachangia kupungua kwa makusanyo ya maduhuli.
- Miundombinu isiyotosheleza inasababisha taarifa za makusanyo ya maduhuli kutolewa kwa mwezi badala ya kila wiki.
- Maeneo mengi hayajafanyiwa tathmini hivyo kusababisha wamiliki kutokulipia kodi ya ardhi
- Kutokuwepo msukumo wa ukusanyaji wa maduhuli hivyo kusababisha ukusanyaji wa kodi kwa mafungu hasa wakati wa kuhamisha umiliki wa mali.
- Kutokuwepo hitajio la namba ya mlipa kodi wakati wa uhamishaji wa umiliki wa mali badala yake wizara inadai uthibitisho wa malipo ya kodi itokanayo na mtaji tu.
- Hivi sasa Wizara ya Ardhi na Maendeleo ya Makazi ina mpango wa kuuendeleza mfumo uitwao Integrated Land Management Information System (ILMIS) ambao utaboresha zaidi usajili wa viwanja ili kuwa na kumukumbu sahihi.

Uchunguzi umeonyesha kuwa kuna maeneo mengi yenye viwanja ambavyo havijapimwa na vitaweza kuingiza mapato mengi.

3.6.9 Mauzo yatokanayo na bidhaa za misitu.

Licha ya ukweli kwamba bidhaa za misitu zimekuwa kianzio kikubwa cha mapato kwa Wizara ya Maliasili na Utalii, wizara imekiri wazi kwamba hakuna udhibiti wa kutosha kwenye eneo la misitu, hivyo kusababisha makusanyo yamaduhuli sawana asilimia 40 kutokusanywa.

Zifuatazo ni changamoto zilizopo kwenye makusanyo ya maduhuli kutokana na rasilimali za misitu zinazokusanywa na Mamlaka za Serikali za Mitaa.

- Maofisa wenye dhamana ya kusimamia rasilimali za misitu kuingiliwa na wanasiasa kwenye maamuzi ya kazi zao.
- Mishahara midogo kwa wanaohusika na uangalizi wa rasilimali hizo, umbali mkubwa uliopo kati ya maeneo ya makazi na ofisi husababisha usumbufu wakati wa kufuata mishahara.
- Kukosekana vitendea kazi ikiwa ni pamoja na rasilimali watu, zana mbalimbali ili kudhibitibidhaa za misitu kutokana na mtawanyiko wa misitu.
- Usimamizi mbovu wa sheria zinazohusu rasilimali za misitu kwenye mamlaka ya serikali za mitaa.
- Utaratibu usioridhisha uliopo kati ya serikali kuu na serikali za mitaa pale inapoonekana ni muhimu kutoa adhabu kwa mtumishi wa serikali za mitaa.
- Kutokuwepo muingiliano mzuri wa kikazi kati ya serikali kuu na serikali za mitaa, mfano kituo cha uwekezaji kinatoa cheti cha kuhamasisha wawekezaji bila kutathmini maduhuli yanayotakiwa kukusanywa na wizara ya mali asili hivyo kusababisha mwekezaji kutolipa baadhi ya kodi.
- Mfano mwingine ni pale ambapo wawekezaji wanaposhindwa kulipa kodi ya hoteli inayotozwa na wizara

ikiwa ni matokeo ya kodi kidogo inayotozwa na serikali za mitaa, hivyo kuwa ni rahisi kufanya biashara na serikali za mitaa badala ya wizara.

- Pia sheria ya misitu ya 2002 inataka vibali vyote na lesenizitolewazo kwa ajili ya uchimbaji na utafutaji wa madini, kupata vibali vya mazingira kutoka wizarani,lakini haifuatwi.
- Urasimu uliokithiri serikalini unachangia pia ukusanyaji hafifu wa maduhuli.
- Wafanyabiashara kughushi nyaraka mbalimbali.
- Kutoeleweka vizuri kwa vianzio vya kodi na wakusanyaji mapato kama vilivyoainishwa kwenye kifungu 49 cha sheria ya misitu ya mwaka 2002 (Act No 14 of 2002).

3.6.10 Vitalu vya uwindaji- Ada ya uwindaji

Mapato yatokanayo na ukodishwaji wa vitalu vya uwindaji kwa mwaka 2010 yalifikia jumla ya Sh. 33 bilioni. Mpango mkakati ulioanzishwa mwaka 2011 umeiwezesha Wizara ya Maliasili na Utalii kukusanya kiasi cha Sh.79 bilioni kutokana na kianzio hiki cha mapato.

Changamoto walizonazo wakusanyaji wa maduhuli katika sekta hii

- i. Mlipa ushuru kulazimika kuwa na Namba ya Utambulisho wa Mlipa Kodi (TIN) kwani utoaji leseni za uwindaji na uvunaji wa mazao ya misitu unamlazimu mwombaji kuwa na TIN (Rejea Kiambatisho cha IV, Jedwali la Nne la Sheria ya Kodi ya Mapato ya mwaka 2004)
- ii. Watumishi wa Halmashauri wanaokusanya mapato pamoja na Maafisa Wanyamapori katika wilaya wanaofanya kazi hiyo kwa niaba ya Wizara kutowajibika kwa Wizara ya Maliasili na Utalii moja kwa moja.
- iii. Utoaji leseni na daraja za mahoteli haufanyiki kwa ufanisi kwa vile hakuna kanuni zinazosimamia eneo hili hadi wakati wa kuandika taarifa hii.

- iv. Ukosefu wa uaminifu kwa baadhi ya wakusanyaji wa mapato kwa kutokutoa nakala za stakabadhi zilizokiri mapokezi ya mapato kwa walipa ushuru wakati wa kutoa leseni za biashara na vibali vya uwindaji na uvunaji wa mazao ya misitu
- v. Kutokuwepo kwa watumishi wa kutosha na nyenzo za kazi za kudhibiti wanyamapori kutokana na ukubwa wa maeneo ya misitu, hifadhi na kuhamahama kwa wanyama
- vi. Uwindaji haramu wa wanyamapori

3.6.11 Mrahaba kutokana na uchimbaji madini

Wakala wa Uguzi wa Madini Tanzania (TMAA) ndiye mwenye dhamana katika kudhibiti uzalishaji wa madini na ukusanyaji maduhuli yatokanayo na mrahaba kwa kampuni za uchimbaji madini. Hata hivyo, TMAA haina udhibiti wowote katika uzalishaji na uthamanishaji wa madini kwa wachimbaji wadogo na wa kati ambao wameachwa kueleza wenyewe kiasi cha madini wanachozalisha.

Kulingana na taarifa ya Wakala wa Usuluhihi wa mapato yatokanayo na sekta ya madini kati ya serikali na makampuni ya uchimbaji (TEITI), udanganyifu umeonekana kukithiri katika sekta ya madini kwa upande wa ulipaji wa mrahaba serikalini. Taarifa ya TEITI inaonyesha kuwepo kwa tofauti katika malipo ya mrahaba yaliyolipwa katika Wizara ya Nishati na Madini na taarifa za Makampuni ya madini kuhusiana na malipo hayo hayo.

Kwa mujibu wa taarifa ya TEITI, malipo ya mrahaba yaliyoonyeshwa na makampuni ya uchimbaji madini yalikuwa juu kwa ujumla ikilinganishwa na mapato yaliyorekodiwa na Wizara ya Nishati na Madini. Malipo yaliyofanywa na Makampuni kwa Wizara yalikuwa na mchanganuo unaoonyesha tarehe malipo yalipofanyika na stakabadhi zilizotolewa na wizara kukiri mapaokezi za malipo hayo. Wizara inadai kuwa mtandao wake usiokuwa wa kielektroniki umesababisha kuwapo ugumu wa kupata taarifa zinazohusiana na kipindi ambacho usuluhisho wa mapato unafanyika.

Changamoto zinazokwaza ukusanyaji wa mapato ya mrahaba

- i. Upungufu wa watumishi katika eneo la ukusanyaji mapato na hivyo kulazimika kuwatumia wataalamu wa madini kukusanya mapato katika maeneo ya pembezoni.
- ii. Upungufu wa vitendea kazi na miundombinu ya ukusanyaji, hii imekwaza ufuatiliaji wa ukusanyaji mapato ya mrahaba kwa wachimbaji wadogo na wa kati.
- iii. Kucheleweshwa kwa malipo ya mwisho ya mrahaba na baadhi ya makampuni ya uchimbaji kutokana na kutofanya usuluuhisho kikamilifu wa malipo ya awali na ya mwisho ya mrahaba.
- iv. Ukosefu wa miundombinu umesababisha utoaji taarifa za makusanyo ya mrahaba kufanyika kwa mwezi badala ya kila juma.
- v. Kuchelewa kuwasilisha makusanyo ya maduhuli kutoka maeneo ya pembezoni na kutoaminika kwa taarifa za makusanyo zinazopokelewa.
- vi. Mlipa ushuru kulazimika kuwa na Namba ya Utambulisho wa Mlipa kodi (TIN) kabla ya kuomba leseni ya uchimbaji; utaratibu huu haufuatwi na wachimbaji wadogo na wa kati.
- vii. Lipo tatizo katika udhibiti wa leseni kwa wachimbaji wadogo na wa kati pale muda wake wa matumizi unapoisha. Orodha ya wachimbaji waliosajiliwa/wenye leseni katika Wizara sio ya kuaminika. Wizara ina programu ya kompyuta iitwayo ‘Flex Cadastre’. Programu hii haihuishwi mara kwa mara na Maafisa madini wa Kanda na wakati wa kutoa leseni mpya za uchimbaji na za kutafuta madini.

3.6.12 Wakala wa shughuli zisizo za Kiserikali

Sheria ya Fedha Na. 13 ya mwaka 2008 na Waraka wa Hazina Na. 8 wa mwaka 2008/09 zinayataka mshirika na Taasisi za

Umma zinazofanya biashara kuchangia katika Mfuko Mkoo wa Serikali. Aidha, Ibara ya 135 (2) ya Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania inakataza mapato yoyote yaliyotajwa kisheria kutumika kwa kusudio maalum yasiwasilishwe katika Mfuko Mkoo wa Serikali. Mapitio ya michango iliyofanywa naWakala wa shughuli zisizo za Kiserikali katika Mfuko Mkoo wa Serikali yamebaini kuwa hakuna hata wakala mmoja kati ya manne waliofanyiwa mapitio aliyezingatia matakwa ya sheria na Katiba kama ilivyoelezwa hapo juu. Wakala wa shughuli zisizo za Kiserikali waliofanyiwa mapitio ni: Hifadhi ya Mbuga za Taifa (TANAPA); Mamlaka ya Hifadhi ya Bonde la Ngorongoro; (NCAA) Mamlaka ya Udhibiti wa Nishati na Maji (EWURA); na Mamlaka ya Udhibiti wa Mawasiliano Tanzania (TCRA).

SURA YA 4

MATOKEO YA UKAGUZI WA AWALI WA MALIPO YA UZEENI

4.0 Utangulizi

Ukaguzi wa awali wa mafao ya wastaifu unafanywa kwa mujibu wa Ibara ya 143 ya Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania ya mwaka 1977 na Kifungu cha 29 cha Sheria ya Ukaguzi wa Umma Na.11 ya mwaka 2008. Kifungu cha 5 (a) cha Sheria hiyo ya Ukaguzi kinamtaka Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali kuhakikisha kwamba fedha zinazokusudiwa kutolewa kutoka Mfuko Mkuu wa Serikali, matumizi yake yawe yameidhinishwa na kwamba zitatolewa kwa mujibu wa masharti ya Ibara ya 136 ya Katiba, na iwapo ataridhika kwamba masharti hayo yatakelezwia ipasavyo, basi ataidhinisha fedha hizo zitolewe. Kutokana na ukweli kuwa malipo ya pensheni hulipwa bila makadirio yake kuidhinishwa na Bunge, ni vyema Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu akafanya ukaguzi wa awali kwa malipo hayo ya mafao ya wastaifu ambayo si rahisi kukadiriwa kwa uhakika na kutengewa fedha.

4.1 Madhumuni ya ukaguzi wa awali

Lengo la kufanya ukaguzi wa awali wa mafao ya wastaifu ni kuhakiki usahihi wa malipo hayo na kuzuia au kubaini makosa mapema na wakati huo huo, kuhakikisha kuwa wastaifu wanalipwa kile wanachostahili. Ukaguzi wa awali ni muhimu kwa kuwa malipo yasiyo sahihi yakifanywa kwa wastaifu inakuwa vigumu kuyarejesha kutoka kwa wastaifu hao. Kwa upande mwingine, ukaguzi wa awali unalenga kuhakikisha kuwa sheria za malipo ya uzeeni pamoja na kanuni na sera za utumishi wa umma, miuondo ya utumishi na mifumo ya mishahara vinafuatwa na kuzingatiwa wakati wa kutengeneza malipo ya wastaifu.

4.2 Mawanda ya ukaguzi wa awali

Matokeo ya ukaguzi na mapendekezo yaliyomo katika ripoti hii hayawahusu watumishi ambao mafao yao ya uzeeni yanashughulikiwa na Mfuko wa Pensheni kwa Watumishi wa Serikali (PSPF). Ukaguzi wa awali wa mafao ya uzeeni unahuishisha makundi yafuatayo:

- Maafisa wa Jeshi, Walimu na Maafisa Usalama.
- Malipo ya Mikataba kwa Viongozi wa Kisiasa, wasiokuwa raia na wastaafu walioko kwenye ajira ya mkataba.
- Watumishi wa Serikali wasio na stahili ya pensheni ambao hulipwa fidia ya kiinua mgongo.
- Mafao ya askari Polisi wa ngazi za chini.

4.3.0 Matokeo ya ukaguzi na mapendekezo

4.3.1 Matokeo

Katika mwaka 2011/2012, Ofisi yangu ilianza na majalada 47 ya pensheni ikiwa ni bakaa kutoka mwaka 2010/2011. Jumla ya majalada 4480 ya wastaafu yaliwasilishwa kwa ajili ya ukaguzi na kufanya idadi ya majalada yote katika kipindi husika kuwa 4,527. Kati ya majalada yote yaliyokuwepo, majalada 4,492 yalikaguliwa, 335 yalirudishwa kwa Maafisa Masuuli kwa marekebisho na hadi kufikia tarehe 30 Juni, 2012 majalada 35 yalikuwa yakiendelea kukaguliwa kama inavyoonyeshwa kwa ufupi hapa chini:

Mchanganuo	Majalada
Salio la nyuma 1 Julai, 2011	47
Majalada yaliyopokelewa katika mwaka	4,480
Majalada yaliyokuwepo kwa ajili ya ukaguzi	4,527
Majalada yaliyokaguliwa	4,492
Salio la majalada tarehe 30Juni, 2012	35

4.3.2 Ukokotoaji zaidi au pungufu wa mafao ya wastaafu

Majalada yaliyowasilishwa kwa ajili ya ukaguzi yameonyesha kuwepo kwa makosa katika ukokotoaji wa mafao ya baadhi ya

wastaafu. Makosa hayo yangesababisha mafao kulipwa zaidi au pungufu ya stahili ya mstaafu. Kwa mfano, kati ya majalada 4,492 ya pensheni yaliyokaguliwa, 184 yangelipwa zaidi kwa kiasi cha Sh.325,261,768.37 wakati majalada 151 yangelipwa pungufu kwa kiasi cha Sh.258,915,380.69 kama yalivyoonyeshwa hapa chini:-

(i) Fedha zilizozidishwa Sh. 325,261,768.37

Na.	Maelezo	Idadi ya kadhia	Kiasi (Sh)	Kiambatisho
1.	Muda uliozidishwa	88	198,445,478.40	III(a)
2.	Mishahara iliyozidishwa	50	100,368,723.78	III(b)
3.	Mishahara iliyozidishwa NSSF	18	<u>23,673,924.86</u>	III(c)
4.	Makosa katika ukokotoaji	28	2,773,641.33	III(d)
	Jumla	184	325,261,768.37	

(ii) Kiasi kilichopunjwa Sh.258,915,380.69

Na.	Maelezo	Idadi ya watumishi	Kiasi (Sh)	Kiambatisho
1.	Kipindi kilicho punjwa	73	138,465,623.44	III(e)
2.	Mishahara iliyopunjwa	47	<u>101,458,129.49</u>	III(f)
3.	Mishahara iliyopunjwa NSSF	14	<u>5,054,021.71</u>	III(g)
4.	Makosa katika ukokotoaji	17	13,940,606.05	III(h)
	Jumla Sh.	151	258,918,380.69	

Kutokana na mchanganuo huo hapo juu, endapo malipo ya uezni yasingekaguliwa kabla ya kulipwa, Serikali ingepata hasara ya Sh.325,261,768.37 wakati wastaaafu wangepata malipo pungufu ya jumla ya Sh.258,918,380.69.

4.3.3 Changamoto zilizojitokeza wakati wa ukaguzi

Wakati wa ukaguzi zilijitokeza changamoto ambazo zinaweza kuainishwa katika makundi matatu yafuatayo:

- (i) Matatizo ya utendaji,
- (ii) Tafsiri zisizo sahihi za Sheria za Penseni na Kanuni zake,
- (iii) Kasoro za kiutawala

Matokeo muhimu ya ukaguzi wa mafao ya uezni ni haya yafuatayo:

- Kuchanganya masharti ya ajira za kudumu na za mikataba
- Kuzidisha muda wa ajira ya pensheni kwa watumishi wa jeshi
- Uandaaji wa mishahara isiyostahili wakati wa kuandaa mafao
- Madai ya wastaaafu waliopitia ajira tofauti
- Kukinzana kwa maamuzi ya watumishi wengine wa umma kuhusu sheria ya pensheni
- Kutokuwa na stahili ya kulipwa pensheni
- Kuchelewa kuwasilisha majalada kwa ajili ya ukaguzi
- Majalada kuwa na nyaraka pungufu
- Mkanganyiko kuhusu sheria ipi itumike kulipa mafao

4.3.4 Kuzidisha muda wa ajira ya pensheni kwa watumishi wa jeshi

Sheria ya Jeshi la Wananchi inahitajimaofisa wa kijeshinawatuwanaotumikia chini yahuduma yapenshenikusitishahuduma zaomara baada yakufikia umri wa kustaafukwa lazimailakwamazingira maalum.

Hata hivyo, mapitio ya nyaraka zamaombiya penshenikwawanajeshiumebaini kuwabaadhi ya maafisanawatu wakijeshi walibakiakatikahudumanamamlaka husikabaada yakufikiaumri waowakustaafukwa lazima.

Ukaguzi ulibaini kuwa wanajeshe waliofikia umri wa kustaafu wanapandishwa vyeo vya juu na kulipwa mishahara mikubwa hali iyoingizia serikali hasara kubwa kwa njia ya malipo ya mafao ya kustaafu.

4.3.6 Mapitio ya masuala ambayo yalikuwa yenyé shaka yalionyesha kutotekelezwa kwa kiwango cha kuridhisha hali iliyofanya mambo hayo kuendelea kujitokeza

(i) Utumiaji wa mishahara isiyosahihi wakati wa kuandaa mafao ya mwisho

Sheria ya Pensheni inaelekeza kutumia mshahara wa mwisho wa mtumishi akiwa kwenye ajira ya Umma katika kuandaa mafao ya mstaaful. Hata hivyo, imeonekana kuwa baadhi ya watumishi waliokuwa Serikalini waliteuliwa katika nafasi mbalimbali katika Mashirika ya Umma au uongozi wa kisiasa na hivyo kupokea mishahara iliyoko katika vyeo hivyo. Sio sahihi kisheria mishahara hiyo ya uteuzi katika mashirika na siasa kutumika kukokotoa mafao ya pensheni kwa wastaaful badala ya ile ya mwisho katika utumishi wa Umma.

Baadhi ya wastaaful wamekuwa wakishinikiza waajiri wao kukokotoa mafao yao kwa kutumia mishahara ya mwisho kwenye taasisi walizokuwa wakifanya kazi kabla ya kustaafu. Hii ni kinyume na sheria ya pensheni ambayo inataka ukokotoaji na ulipaji wa pensheni uzingatie mishahara inayokubalika kulingana na sheria husika.

(ii) Madai mara mbili ya mafao ya kustaafu (pensheni na ajira ya mikataba)

- Wakati wa ukaguzi, ilibainika kuwa baadhi ya maafisa waliteuliwa katika nyadhifa mbalimbali kwa mkataba wakati huo wakiendelea kuwa na haki ya malipo ya mafao ya

pensheni. Wakati wa kustaafu kuna uwezekano wa watumishi hao kulipwa mara mbili katika kipindi kimoja cha utumishi (yaani malipo ya mkataba na malipo ya mafao ya pensheni)

- Baadhi ya watumishi walioajiriwa kwa masharti ya mikataba wamebainika kusajiliwa na kuchangia kwenye Mfuko wa Pensheni kwa Watumishi wa Umma (PSPF). Kulingana na sheria na kanuni za pensheni, watumishi wanaofanya kazi kwa mikataba hawastahili kuchangia na kulipwa mafao ya mfuko wa PSPF.
- Wakati wa ukaguzi, ilibainika kuwa maafisa wa jeshi waliokuwa wameteuliwa katika nyadhifa za uongozi wa kisiasa waliendelea kuwa na nyadhifa zao za kijeshi kinyume na maagizo yaliyotolewa na Jeshi la Ulinzi la Wananchi wa Tanzania na Katibu Mkuu Kiongozi yaliyowataka kujiuzulu vyeo vyao vya kijeshi mara tu baada ya uteuzi katika nyadhifa za kisiasa. Suala muhimu hapa ni kuhakikisha kuwa muda wa utumishi katika jeshi unalipwa pensheni na muda ambao mstaafu ametumikia uongozi wa kisiasa unalipwa tuzo ya mkataba. Hata hivyo, uzoefu umeonyesha kuwa utaratibu huo haufuatwi na hivyo kusababisha malipo mara mbili kwa maafisa wahusika; kwa mfano:

Maafisa wa jeshi wanaopata ajira za kisiasa hawaachi utumishi wao jeshini hadi wanapofikia umri wa kustaafu katika jeshi na hivyo kusababisha ukokotoaji wa mafao yao ya kustaafu kujumuisha muda ambao wametumikia vyeo katika siasa kinyume na sheria za pensheni hawastahili kuchangia wala kulipwa mafao yao kupitia mfuko huu.

(iii) Kutokuwa na stahili ya kulipwa pensheni

Watumishi wa ngazi ya chini Serikalini waliokuwa wameajiriwa chini ya masharti ya muda na baadae wakaingizwa katika masharti ya kudumu na pensheni, mafao yao ya izeeni yalikokotolewa kama vile bado walikuwa chini ya masharti ya muda kinyume na sheria za pensheni ambazo zinataka kipindi alichotumikia mstaafu chini ya masharti ya

muda kupata kibali cha Katibu Mkuu Hazina ili kihesabiwe katika masharti ya kudumu kwa madhumuni ya kulipa pensheni

- (iv) **Kuchelewa kuwasilisha majalada kwa ajili ya ukaguzi**
Sheria ya Pensheni inataka mchakato wa kulipa mafao ya wastaifu kuanza miezi 6 kabla ya mtumishi kustaifu. Utaratibu huu unalenga kukamilisha maandalizi ya malipo mapema na kulipwa kwa wakati. Kinyume na hivyo, baadhi ya majalada yanaletwa ukaguzi baada ya miezi kadhaa au mwaka baada mtumishi kustaifu.

Zaidi ya hayo, majalada mengi ya wastaifu huletwala kwa ajili ya ukaguzi wa awali yakiwa na nyaraka pungufu na hivyo kulazimu kuitisha nyaraka hizo jambo ambalo huchangia kuchelewesha machakato mzima wa ulipaji wa mafao kwa wastaifu.

- (v) **Uwasilishaji wa nyaraka pungufu**
Pamoja na kuchelewa kwa majalada ya malipo ya pensheni kama tulivyoeleza hapo juu idadi kubwa ya majalada ya pensheni yaliwasilishwa kwa ajili ya ukaguzi yakiwa na nyaraka pungufu ambazo hazikukidhi zoezi la kukokotoa mahesabu, hivyo kusababisha kuhitaji kuwasilishwa tena kwa nyaraka zilizokosekana. Hatua hii imesababisha kuchelewa kukamilisha zoezi la uandaaji wa malipo ya pensheni.

- (vi) **Mkanganyiko kuhusu sheria ipi itumike kulipa mafao**
Imeonekana kuwa uongozi wa baadhi ya taasisi umekuwaukiomba idhini ya kulipa mafao ya uezini bila kuzingatiasheria za pensheni zifuatazo:
Mafaili ya pensheni yamekuwa yanaandaliwa kwakutumia mishahara walijolipwa watumishi katika Mashirika ya kimataifa na ya Umma. Ilbainika wakati wa ukaguzi kuwa watumishi hawa walijiriwa Serikalini kwamkataba katika nafasi yenye mshahara wa chiniikilinganishwa na waliokuwa wanalipwa katika mashirikahayo; idhini iliombwa ili wahusika walipwe mishaharawaliyokuwa wanalipwa wakati wakiwa katika ajira

zamashirika ya kimataifa na ya umma. Hii ni kinyume naAya ya 47(a), (b) na (c) ya Kanuni za Kudumu na Kifungucha 14 Sheria ya Pensheni kama ilivyorekebishwa tarehe20 Machi, 1978. Sheria tajwa zitatumika tu endapo ajiraya mtumishi ni ya masharti ya kudumu na pensheni.

Pia, imeonekana kuwa baadhi ya maafisa walioachakuwa viongozi wa kisiasa kwa namna ambayo sheria zapensheni zilizopo ziliruhusu wao kulipwa mafao lakini malipo yao hayakutayarishwa kwa wakati kwa madai kuwa maafisa wahusika hawakuomba kulipwa mafaohayo.

Aidha, waajiri wao hawakushughulikia stahili zao zamafao kwa vile maafisa hawa waliendelea kuteuliwakatika nafasi ambazo mafao yakeya pensheni yanatawaliwa na sheria nyingine. Wakatimaafisa hawa wanapostaafu katika ajira yao ya mwisho, huomba kibali cha kuunganisha muda wote wa ajira iliwalipwe pensheni kwa sheria inayowapa manufaa zaidikimapato. Kwa vyovypote vile, sheria haitoi mwanya kwamstaafu kunufaika kwa kutumia sheria inayosimamiaajira yake ya mwisho katika mashirika ya kimataifa au taasisi nyingine.

(vii) Kasoro katika kutayarisha malipo ya uzeeni

Kwa ujumla, matatizo yaliyoelezwa hapo juu yamechangiwa zaidi na udhaifu wa watayarishaji majalada kwani baadhi yao walishindwa kufuata sheria za pensheni na miongozo. Ijapokuwa kasoro hizo zimeelezwu pia katika ripoti ya mwaka ulipoita, hakuna hatua yoyote iliyochukuliwa.

SURA YA 5

MAMBO MUHIMU YALIYOJITOKEZA KATIKA UKAGUZI WA WIZARA, IDARA, WAKALA NA SEKRETARIETI ZA MIKOA

- 5.1 Kushindwa kuweka kumbukumbu za masurufu ya Shs.1,511,759,500**

Kanuni ya 98 (1) ya Kanuni za Fedha za Umma za mwaka 2001 (zilizorekebishwa 2004) zinaelekeza kwamba “masurufu yote, bila kujali ni ya namna gani, yatolewe kwa majina ya maafisa wanaohusika na masurufu hayo, na maafisa hao watawajibika nayo hadi hapo yatakapolipwa au kuondokana nayo kwa kuwasilisha hati ya malipo iliyokamilika au kukabidhi kwa afisa mwingine anaewajibika nayo. Mtu yeote mwenye masurufu asiondolewe sehemu yoyote ya wajibu wake kwa kukasimu utunzaji au usimamizi wa masurufu hayo kwa afisa mwingine”.

- 5.2 Mrahaba usiokusanywa Dola za Kimarekani 12,634,354 sawa na Sh.19,709,593,191**

Kifungu cha 87(1)(c) cha Sheria ya Madini ya mwaka 2010 kinataka mrahaba kulipwa katika kiwango cha asilimia 4 ya thamani ghafi, yaani thamani ya madini katika soko mahali inaposafishwa au kuuzwa ama kama inatumika ndani ya Tanzania, pale inapopatikana ndani ya Tanzania. Hata hivyo, ukaguzi uliofanyika katika Wizara ya Nishati na Madini umegundua kwamba makampuni ya madini yamekuwa yakilipa mrahaba katika kiwango cha asilimia 3 ya thamani halisi kama ilivyoainishwa katika Sheria ya Madini iliyokuwa ikitumika awali na ambayo kwa sasa haitumiki kama inavyoonyeshwa hapa chini:

Jedwali 15: Mrahaba usiokusanywa

Kituo	Kumb. Na. ya Taarifa ya Ukaguzi	Kiasi kinachopaswa kulipwa katika Dola za Kimarekani (4%)	Kiasi kilicholipwa Dola za Kimarekani (3%)	Tofauti katika Dola za Kimarekani (Pungufu ya Malipo)
Kahama	AB.233/366/01 ya tarehe 16/03/2012	31,956,749.34	21,611,428.29	10,345,321.05
Shinyanga	BE.366/466/01 ya tarehe 07/03/2012	9,405,981.36	7,116,947.80	2,289,033.56
Jumla		41,362,730.70	28,728,376.09	12,634,354.61

5.3 Ulipaji wa madeni ya miaka iliyopita kwa kutumia fedha zilizoidhinishwa kwa matumizi ya mwaka 2011/2012 Sh. 252,975,000,000

Mapitio ya hotuba ya bajeti ya Waziri wa Ujenzi kwa mwaka wa fedha 2011/2012, Toleo la IV (*Volume IV*) - Daftari la Udhibiti wa Makadirio ya Matumizi ya Fedha za Umma za Shughuli za Maendeleo (*Public Expenditure Estimates Development Vote book*), Taarifa ya Hazina ya Kutolewa kwa Fedha (*Treasury Exchequer Issues Notification*) na Idhini ya Kutolewa kwa Fedha (*Release Warrants*) yamedhihirisha kuwepo kwa mradi wa “Ujenzi Maalum wa Barabara” hewa katika hesabu za Wizara ya Ujenzi mradi ambao ulipewa namba ya utambulisho (*Code No.*) 4168 ambayo pia ni hewa kama kasma ya matumizi inayojitegemea ili kuingiza fedha kwa ajili ya kufanya matumizi yaliyofikia Sh. 252,975,000,000 kulipia madeni yaliyokuwepo miaka iliyopita ya miradi iliyoteklezwa na TANROADS. Orodha ya fedha zilizotoka Hazina kwenda Wizara ya Ujenzi ni kama ifuatavyo:

Jedwali 16: Madeni ya miaka iliyopita

Na.	Na. ya Kibali cha Hazina cha kutolea Fedha (Treasury Release Warrant No)	Maelezo	Kiasi (Sh)
1	34 ya mwaka 2011/2012	Ikiwa ni kibali cha kutoa pesa kwa ajili ya malipo ya madeni yaliyokuwepo miaka iliyopita katika miradi 46.	100,000,000,000
2	292 ya mwaka 2011/2012	Ikiwa ni kibali cha kutoa pesa kwa ajili ya malipo ya madeni yaliyokuwepo miaka iliyopita.	152,975,000,000
Jumla			252,975,000,000

Mapitio zaidi yalidhihirisha yafuatayo:-

- i. Fedha zilizotolewa zilitengwa kulpia madeni ya miaka ya nyuma katika miradi 45 ya barabara na mradi mmoja wa kujenga makao makuu ya TANROADS. Miradi yote 46 ilipewa majina na Namba za utambulisho.
- ii. Kiasi kilichotolewa cha Sh.152,975,000,000 hakikuambatanishwa na michanganuo husika pamoja na kwamba vilihitajika katika ukaguzi.
- iii. Kiasi cha Sh.252,975,000,000 kilicholipwa katika mwaka huu ambao hesabu zake zinapitiwa hakikuonyeshwa kama kimelipia madeni ya mwaka uliopita katika taarifa ya fedha ya Wizara ya Ujenzi.

5.4 Amana iliyokaa muda mrefu kwenye Shule za Sekondari Sh.1,551,005,412.38

Ukaguzi wa Akaunti ya Amana (*Deposit Account*) katika Idara ya Mhasibu Mkuu wa Serikali umeonyesha jumla ya Sh.1,551,005,412.38 zilizoripotiwa kuwepo kwenye Akaunti ya Amana. Hata hivyo, kuanzia mwaka 2009, usimamizi wa shule

za Sekondari ulihamishwa kutoka Wizara ya Elimu kwenda TAMISEMI na hapakuwa na maelekezo zaidi kuhusiana na pesa hizi za Amana ambazo zimekuwepo kwenye akaunti za Hazina Ndogo kabla ya mwaka 2009 kama inavyoainishwa hapa chini:

Jedwali 15: Amana zilizokaa muda mrefu

Kituo	Kiasi (Sh)
Lindi	61,371,586.02
Mara	59,576,454.22
Iringa	336,001,141.96
Mwanza	352,287,813.56
Kagera	89,601,331.37
Rukwa	167,322,489.80
Tabora	51,498,919.72
Mbeya	320,218,325.73
Shinyanga	113,127,350.00
Jumla	1,551,005,412.38

Aidha, fedha hizi zitumwe kwa shule za Sekondari husika au zirudishwe katika Mfuko Mkuu wa Serikali, ili ziweze kutumika kama inavyotakiwa.

- 5.5 Malipoyaliiyofanywa na Serikali kwenda Mfuko wa Pensheni ya Utumishi wa Umma (PSPF) kulipia deni la pensheni Shs. 20,000,000,000**
- Ukaguzi wa malipo yaliyofanywa katika Wizara ya Fedha (Fungu 50) umeonyesha kuwa katika mwaka 2011/2012 jumla ya Sh.20,000,000,000 zililipwa PSPF na mwaka uliotangulia (2010/2011) jumla ya Sh. 10,000,000,000 zililipwa PSPF toka Fungu 21 ikiwa ni malipo ya vipengele yenyе lengo la kumaliza deni lenye jumla ya Sh. 3.190 trillioni. Deni hili limetokana na malimbikizo ya stahili za mafao ya pensheni kwa kipindi cha kabla ya kuanzishwa kwa PSPF July 1999 (utumishi wa kabla ya 1999), kipindi ambacho wanachama walikuwa hawajaanza kuchangia Mfuko wa Pensheni.

Kutokana na barua iliyotoka PSPF kwenda Wizara ya Fedha yenye Kumb. Na. PSPF/PB 75/125/VOL.II/183 ya tarehe 16 Aprili 2009, deni hili lilifikiwa kama ifuatavyo:

Jedwali 18: Malipo yaliyofanywa na Serikali kwenda PSPF kulipia deni la pensheni.

Maelezo	Kiasi (Sh)
Kiasi ambacho kingelipwa na PSPF kwa wastaifu wenye stahili ya kulipwa pensheni hadi kufikia tarehe 30/06/2009.	509 bilioni
Kiasi ambacho PSPF inaidai Serikali kwa ajili ya watumishi wenye stahili ya kulipwa pensheni watastaafu kuanzia tarehe 01 Julai 2009 na zaidi.	2.681 trilioni
Jumla	3.190 trilioni

Kutokana na taarifa ya uthamini halisia uliofanywa na “Genesis Actuarial Solutions”, thamani ya deni hili ilikuwa Sh.4.039 trilioni hadi kufikia tarehe 30 Juni 2010.

Ukaguzi uliofanyika ulijumuisha malipo na viambatanisho vilivyowasilishwa kwangu kwa uhakiki ambapo niliona kuwa PSPF ilikuwa ikilipa mafao ya pensheni kwa watumishi waliostaafu kabla ya mwaka 1999 kwa kuelewa kuwa Serikali itarejesha kiasi kilichotumiwa na PSPF. Hadi kufikia tarehe 30/06/2010, jumla ya Sh.716.6 bilioni zilikwisha kutumiwa na PSPF kulipa wastaifu na kiasi hicho kilipaswa kurejeshwa na Serikali.

Kutokana na barua ya Wizara kwenda kwa Mkurugenzi Mkuu wa PSPF ya tarehe 25/03/2011, Wizara itairejeshea PSPF ndani ya miaka 10 kwa kutenga kwenye bajeti kiasi cha Sh.71 bilioni kila mwaka kuanzia mwaka wa fedha wa 2011/2012.

Kufuatia yaliyoelezwa hapo juu tumegundua yafuatayo:

- Wizara haikutenga kiasi cha Sh. 71 bilioni katika bajeti ya mwaka 2011/2012. Kiasi kilichorejeshwa PSPF cha Sh.20 bilioni ndani ya mwaka unaokaguliwa sasa kimelipwa kutoka Mfuko wa Tahadhari (*Contingency Fund*) badala ya kutoka kwenye mafungu yaliyotengwa kila mwaka kama ilivyokusudiwa hapo mwanzo.
- Kiasi kilichorejeshwa PSPF mwaka 2011/2012 cha Sh.20 bilioni kilikuwa kidogo kuliko kiasi kilichokusudiwa cha Sh.71 bilioni (asilimia 28 tu ya kiasi kilichokubaliwa kwa mwaka cha Sh.71 bilioni) hali ambayo itaathiri uwezo wa kifedha wa PSPF.

5.6 Masurufu yasiyorejeshwa kwa muda mrefu Sh. 706,701,016.36

Wakati wa kupitia udhibiti wa taratibu za kutoa na kurejesha masurufu, ilibainika kuwa masurufu yanayofikia Sh.706,701,016.36 yalikuwa bado kurejeshwa hadi kufikia mwezi Disemba 2012 katika Wizara ya Mambo ya Nchi za Nje na Ushirikiano wa Kimataifa kitendo ambacho ni kinyume na Kanuni ya 103(1) ya Kanuni za Fedha za Umma za mwaka 2001 (zilizorekebisha mwaka 2004).

**5.7 Ulipaji wa deni la ATCL Dola za Kimarekani
41,466,177.16**

Wakati wa ukaguzi wa mwaka huu katika Wizara ya Fedha, ilionekana kuwa kiasi cha Sh.2,502,945,000 kililipwa kwa Shirika hodhi (CHC) kwa kutumia Hati ya Malipo Na. PV. 1497/12 ya mwaka 2011 ikiwa ni sehemu ya malipo ya deni la ATCL lililotokana na kukodi ndege aina ya Airbus A320 kutoka Kampuni ya Wallis Trading ya Liberia. Mkataba ulitiwa sahihi mwezi Oktoba 2007.

Kutokana na matokeo ya ukaguzi kama yaliyvoonyeshwa katika taarifa ya ukaguzi ya mwaka 2009/2010, ndege iliyokodishwa ilikuwa mbovu kwa kuwa miezi sita baada ya kuwasili nchini ilifanyiwa matengenezo makubwa nchini

Mauritius mwezi Machi 2009 na baadae Ufaransa mwezi Julai 2009.

Zaidi ya hayo, taarifa ya ATCL ya tarehe 14 Disemba 2010 ilieleza kuwa ndege hiyo ilikutwa wakati wa ukaguzi uliofanyika mwezi Septemba 2010 ikiwa imepakwa rangi ya Shirika la ndege la Taifa la Guinea.

Wakati wa kuhakiki malipo na nyaraka nyingine zilizowasilishwa wakati wa ukaguzi wa mwaka huu, niligundua yafuatayo:

- Kikosi maalum cha majadiliano kilichoteuliwa na Serikali kilikutana na Kampuni ya Wallis Trading Inc tarehe 26/10/2011 kwa madhumuni ya kujadili deni linalodaiwa na Kampuni ya Wallis Trading Inc. Pia, barua ya tarehe 27/10/2011 iliyotoka Wizara ya Fedha kwenda kwa Kampuni ya Wallis Trading Inc ilieleza kuwa kufikia tarehe 26/10/2011, kiasi kinachostahili kulipwa na mkodishaji kama “bakaa ya deni lililohuishwa” ni Dola za Kimarekani 39,000,000.
- Katika barua tajwa hapo juu ya tarehe 27/10/2011, Wizara ya Fedha ilitoa ufanuzi kwa Kampuni ya Wallis kwamba, malipo ya deni la Dola za Kimarekani 39,000,000 yatafanyika katika vipengele 26 kuanzia tarehe 31/10/2011 hadi 26/11/2013.
- Mnamo tarehe 26/10/2012, Wizara ililipakiasi cha Sh.2,502,945,000 (Dola za Kimarekani.1,553,450.23) kwa Kampuni ya Wallis Trading Inc ikiwa ni sehemu ya kwanza ya malipo ya gharama za ukodishaji wakati kiasi kilichobaki (ikiwa ni deni la msingi na riba) kilijilimbikiza hadi kufikia Dola za Kimarekani 41,466,177.16.

Ni maoni yangu kuwa rasilimali haba za serikali zilizopo zinapotea kwa kulipa deni bila kupata manufaa yoyote, tukizingatia kwamba ndege hiyo haipo Tanzania na zaidi ya yote, kwa sasa inafanya kazi ikiwa na rangi ya utambulisho wa Taifa la Guinea.

**5.8 Malipo yasiyokuwa na nyaraka za matibabu nje ya nchi
Sh.448,144,343**

Uchunguzi uliofanywa kwenye hati za malipo za Wizara ya Afya na Maendeleo ya Jamii juu ya matibabu yaliyofanywa nje ya nchi yenye jumla ya Sh.448,144,343, katika kipindi cha mwaka ulioishia tarehe 30 Juni 2012, umeonyesha kuwa kiasi hiki cha pesa kimelipwa kwenye Balozi mbalimbali nje ya nchi kama tahadhari ya kukabiliana na dharura za kitiba. Kiasi hiki kimetolewa kwa utaratibu wa masurufu ambapo mtumiaji anapaswa kutoa mrejesho wa namna zilivyotumika kabla hajapewa nyingine. Fedha hizi ziliwekwa kwenye akaunti Na. 9099150006 iliyopo Twiga Bancorp Ltd (Mchanganuo unaoonekanakwenye Jedwali hapa chini). Uchunguzi wa kina uliofanywa kwenye malipo haya ulibaini mapungufu yafuatayo:

- (i) Hakuna kibali kilichotolewa na Wizara ya Fedha kabla ya kuhamisha kiasi cha Sh.448,144,343 ukizingatia kuwa fedha hizo zilihamishwa mwishoni mwa mwaka wa fedha.
- (ii) Majina ya wagonjwa na hospitali zilizokusudiwa kulipwa baada ya kutoa huduma hazikuwekwa wazi.
- (iii) Makubaliano na majalada ya mikataba ya mawasiliano kati ya Wizara na Balozi havikuwasilishwa kwa ukaguzi.
- (iv) Nyaraka fungamano kama vile ankara za matibabu, Stakabadhi za malipo na taarifa za matumizi hazikuwasilishwa kwa ukaguzi.

Jedwali 17: Malipo yasiyokuwa na nyaraka za matibabu nje ya nchi

Hati ya Malipo	Nambari ya Hundi	Kiasi (Sh)	Mlipwaji	Maelezo
00465	04320 13/9/2011	26,831,811	Government Obligation Settlement - DSM. (Ubalozi wa Tanzania Berlin)	Malipo kabla ya huduma kwa ajili ya ada ya matibabu
01975	05349 14/2/2012	32,636,307	Government Obligation Settlement - DSM. (Ubalozi wa Tanzania Berlin)	Malipo kabla ya huduma kwa ajili ya ada ya matibabu
03522	06317 25/5/2012	66,127,507	Twiga Bancorp Ltd-Dsm. (Ubalozi wa Tanzania Washington DC - USA)	Marejesho <i>(Refund costs).</i>
03500	06284 23/5/2012	4,922,618	Government Obligation Settlement -DSM. (Ubalozi wa Tanzania -London)	Tofauti ya kubalisha Pound 11,760 ambazo zililipwa katika Euro badala ya Pound.
0835	04551 20/10/2011	100,000,000	Government Obligation Settlement - DSM. (Ubalozi wa Tanzania -Nairobi)	Sehemu ya malipo ya Ankara za matibabu
71/3	52DI10005595	25,470,749	Government Obligation Settlement -Dsm. (Ubalozi wa Tanzania -London)	Malipo kabla ya huduma kwa ajili ya gharama za matibabu
27/6	52DI10006450	41,274,651	Twiga Bancorp Ltd-	Gharama za Matibabu na

			Dsm. (Ubalozi wa Tanzania - Washington DC USA)	madeni ya nyuma.
04919	07385	190,875,700	Twiga Bancorp	Matibabu ya dharura nje ya nchi
	Jumla	448,144,343		

**5.9 Mishahara iliyolipwa kwa maofisa waliostaafu kwa mujibu
wa sheria Sh.152,909,338**

Ukaguzi wa mishahara kwa mwaka ulibaini malipo ya jumla ya kiasi cha Sh.96,992,000 yaliyolipwa na Wizara ya Afya na Ustawi wa Jamii kwa maafisa mbalimbali kwa kufanya kazi muda wote. Hata hivyo, kumbukumbu zinaonyesha kwamba watumishi hao walikuwa katika ajira zaidi ya muda unaoruhusiwa kisheria.

Aidha, Wizara tatu zilizotajwa hapa chini ziliendelea kulipa mishahara kwa watumishi waliokwishastaafu, watoro na waliofariki wakati walikuwa hawajafutwa katika orodha ya malipo kinyume na kifungu cha 17 cha sheria ya mafao ya kustaafu Na. 2 ya mwaka 1999.

Jedwali 20: Malipo kwa watumishi ambao hawapo kazini

Fungu	Wizara/Idara na Wakala	Kiasi (Sh.)
49	Wizara ya Maji	28,066,800
51	Wizara ya Mambo ya Ndani	9,115,000
58	Wizara ya Nishati na Madini	18,735,538
	Jumla	55,917,338

5.10 Ada ya Utalii isiyokusanywa Dola za Kimarekani 158,000

Kanuni Na. 4 ya Kanuni za Utalii (ada na tozo) za mwaka 2009 inaeleza kuwa “ada ya leseni kwa kila daraja italipwa kila mwaka kwa kiasi ambacho kimeainishwa katika Jedwali la Pili la Kanuni hizo”.

Mapitio ya makusanyo ya mapato yatokanayo na Leseni za Uendeshaji wa Huduma za Utalii katika Wizara ya Maliasili na Utalii kwa mwaka wa fedha 2011/2012 yameonyesha kuwepo kwa Kampuni zilizojiingiza kwenye biashara ya kutoa huduma ya utalii lakini hawajalipa ada ya Leseni za Utalii yeye jumla ya Dola za Kimarekani 158,000.

5.11 Sehemu ya Bajeti ya Maendeleo iliyotolewa kwa Wizara ya Maji kufuatia Wajibu wa Tanzania kufikia Malengo ya Maendeleo ya Milenia na Dira 2025

Pamoja na jitihada zilizofanywa na wadau mbalimbali katika Sekta ya Maji, kama vile Wadau wa Maendeleo (kupitia Programu ya Maendeleo ya Sekta ya Maji), Serikali, (kupitia mafungu yanayotengwa kila mwaka katika Wizara ya Maji), TASAF n.k, bado upatikanaji wa maji ni hafifu katika maeneo mengi ya Tanzania na ugawaji wake haukidhi mahitaji ya watanzania hasa wanaoishi vijijini. Ama kwa hakika, miundombinu mingi ya maji iliyopo imechakaa. Baadhi ya vijiji bado vinapata maji machafu sana. Vikwazo hivi vipo katika sekta ya maji pamoja na malengo ya Tanzania ya kufuta umasikini na kuleta maisha bora kwa kila Mtanzania ifikapo mwaka 2025. Usimamizi wa Ugawaji Maji, Maji Taka na Vyanzo vya Maji imeelezwa kwa undani katika Dira ya Maendeleo 2025. Dira ya Maendeleo ya Tanzania 2025 ina lenga upatikanaji wa maji salama vijijini; inalenga kuongezeka kutoka asilimia 53 mpaka asilimia 90 kufikia mwaka 2025 na kwa mijini kuongezeka kutoka asilimia 73 mpaka asilimia 100 kufikia mwaka 2025.

Mkakati wa Serikali wa kuyafikia malengo haya muhimu hauna mwelekeo ulio thabiti kufuatia kupungua kwa fedha zinazopelekwa kwenye miradi ya maji ikilinganishwa na fedha zinazopitishwa na Bunge, ikimaanisha kuwa kufikia malengo haya itachukua muda mrefu kuliko ilivyokusudiwa katika Malengo ya Maendeleo ya Milenia 2015 na Dira 2025. Kwa kipindi cha miaka mitatu mfululizo, kiasi kikubwa cha fedha kilichopitishwa na Bunge katika Bajeti ya maendeleo hakikutolewa na Hazina kama ifuatavyo:

Jedwali 21: Muhtasari wa fedha za maendeleo

Akaunti	2009/10	2010/11	2011/12
Fedha za maendeleo zilizotolewa	160,891,677,501	129,151,686,344	105,686,909,691
Fedha za maendeleo zilizoidhinishwa	245,656,445,000	233,092,607,000	428,638,963,000
Asilimia ya fedha zilizotolewa na Hazina	65.5%	55.4%	24.6%

5.12 Ukaguzi wa Usimamizi wa Manunuzi

5.12.1 Utangulizi

Mamlaka ya Udhibiti wa Manunuzi ya Umma (PPRA) imeandaa na kuwasilisha kwangu taarifa ya mwenendo wa manunuzi katika Taasisi za Manunuzi kwa kipindi hiki cha ukaguzi ambayo pia imeonyesha mengi ya maeneo yenyeye mapungufu yaliyojitekeza zaidi katika taarifa zangu zilizotangulia. Nakubaliana na kazi iliyofanywa na Mamlaka ambapo nimeona ni muhimu na sahihi kuijumuisha kwenye taarifa yangu. Lengo la ukaguzi uliofanywa na PPRA ni kubaini kiwango cha uzingativu wa Sheria ya Manunuzi ya mwaka 2004; Kanuni zake za 2005 na Tangazo la Serikali Na. 177 la mwaka 2007 na kwamba manunuzi yaliyofanywa yanawakilisha thamani halisi ya fedha zilizotumiwa na Taasisi husika.

Muhtasari wa matokeo na mapungufu yaliyojitekeza ni kama ifuatavyo:

5.12.2 Matokeo ya Ukaguzi wa Manunuizi

Kama ilivyokuwa kwa ukaguzi wa mwaka wa fedha uliopita, mapungufu yaleyale yameonekana tena mwaka huu wa fedha ambayo ni: Uundwaji usio sahihi wa Vitengo vya Kusimamia Manunuizi; Uandaaji usio sahihi wa mipango ya mwaka ya manunuizi; Utunzaji mbovu wa kumbukumbu; udhaifu katika kusimamia mikataba, na; Kushindwa kutangaza utoaji wa mikataba.

(a) Uundwaji usio sahihi wa Vitengo vya Kusimamia Manunuizi (PMUs)

Hili bado ni tatizo linalozikabili Taasisi za Manunuizi zilizo nyingi. Ukaguzi umebaini kuwa wastani wa kiwango cha uzingativu katika kuunda Vitengo vya Manunuizi ulikuwa asilimia 78 (asilimia 56 mwaka 2010/2011) kwa Wizara, Idara na Wakala.

(b) Uandaaji usio sahihi wa mipango ya mwaka ya manunuizi

Taasisi za Manunuizi nyingi zilizokaguliwa bado hazizingatii matakwa ya uandaaji wa mipango ya mwaka ya manunuizi pamoja na kwamba ni muhimu katika kuzisaidia Taasisi za Manunuizi: kuepuka manunuizi ya dharura yasiyo ya lazima; kujumuisha manunuizi pale inapowezekana ili kupata thamani ya fedha na kupunguza gharama za manunuizi; pale inapowezekana, kuingia mikataba endelevu kwa manunuizi yanayohitajika mara kwa mara; kuepuka manunuizi yasiyo jumuifu na kufuata utaratibu wa manunuizi unaofaa; na kupanga vyema vikao vya bodi za zabuni ili kupunguza gharama za uendeshaji.

Mapitio ya utayarishaji wa mipango ya manunuizi ya mwaka unaonyesha kwa wastani uzingativu wa asilimia 58. Wastani wa uzingativu wa utayarishaji wa mipango ya mwaka ya manunuizi kwa Wizara, Idara na Wakala ilikuwa asilimia 68 mwaka 2011/2012 (asilimia 54 mwaka 2010/2011).

(c) Udhaifu katika kusimamia mikataba

Kama ilivyokuwa kwa kaguzi zilizopita, mapungufu yafuatayo yalionekana wakati wa mapitio ya usimamizi wa mikataba: Baadhi ya mikataba inakosa nyaraka muhimu na mingine ina nyaraka zisizo za mikataba; inapotokea kushindwa kutekeleza matakwa ya mkataba dhamana zilizowekwa hazitumiki; muda wa kupewa huduma bila malipo hautumiki pale zinapopokelewa mali zisizo na ubora; Kutotumia kifungu cha fidia kwa kuchelewa kutekeleza mikataba; Kutokuwa na vikao katika eneo la mradi kwa miradi mingi iliyopitiwa; Kutokuwepo mipango ya kudhibiti na kutoa hakikisho la ubora katika utekelezaji wa mikataba, kazi zilizokamilika hazikufanyiwa tathmini kuona kama zimekidhi matakwa ya utekelezaji aliyopewa mkandarasi katika mkataba; Taarifa za utekelezaji hazikuandaliwa; Taarifa za wasimamizi wa mikataba hazikutayarishwa; Muda wa utekelezaji mikataba kuongezwa bila kufuata taratibu; Malipo kufanywa kwa kazi ambayo haijafanyika kwa kuzidisha kiwango cha kazi iliyokamilika; na Kutokuteuliwa kwa Kamati za mapokezi na ukaguzi wa mali zilizonunuliwa kuthibitisha usahihi, ubora na idadi.

Matokeo ya ukaguzi yameonyesha wastani wa kiwango cha uzingativu wa asilimia 55 na 71 kwa udhibiti wa ubora na usimamizi wa mikataba. Wastani wa kiwango cha uzingativu kwa Wizara, Idara na Wakala ulikuwa asilimia 56 kwa udhibiti wa ubora na asilimia 72 kwa usimamizi wa mkataba (asilimia 64 na 41 mwaka 2010/2011).

(d) Kushindwa kutangaza utoaji wa mikataba

Kuonyesha taarifa za manunu ni mionganii mwa mambo yanayoonyesha uwazi katika misingi ya manunu ya umma. Hata hivyo, Taasisi za Manunu nyingi zilizokaguliwa bado hazizingatii matakwa ya kuwasilisha kwenye Mamlaka mikataba iliyotolewa kama ilivyoelezwa kwenye Kanuni za 21(1) na 67(4) za Matangazo ya Serikali Na. 97 na 98 ya mwaka 2005. Mamlaka, kuitia Kanuni Na. 21(3) na 67(3) za Matangazo ya Serikali Na. 97 na 98 ya mwaka 2005, inatakiwa

kutangaza kwenye Jarida na tovuti taarifa iliyowasilishwa juu ya utoaji wa mikataba.

Ukaguzi uliofanyika umebaini kwamba kiwango cha uzingativu katika matangazo ya utoaji wa mikataba kilikuwa asilimia 65. Wastani wa kiwango cha uzingativu kwa Wizara, Idara na Wakala ulikuwa asilimia 65.

(e) Utunzaji Mbovu wa Kumbukumbu

Katika kuchunguza kiashiria hiki, wakaguzi walibaini mapungufu ambayo ni pamoja na: Nyaraka zilizokosekana; kukosekana kwa orodha ya zabuni, nukuu za bei na mikataba; kusambaa kwa kumbukumbu za manunuzi katika Idara tofauti; kukosekana kwa kumbukumbu za usimamizi wa mikataba; upungufu wa sehemu za kutunzia nyaraka pamoja na ukosefu wa taratibu za kutunza majalada.

Maoni ya wakaguzi ni kwamba baadhi ya nyaraka zinachifwaa kwa makusudi ili kuficha mapungufu yaliyojitekeza kwenye manunuzi.

Ukaguzi ulibaini kwamba kiwango cha uzingativu katika utunzaji wa kumbukumbu kilikuwa asilimia 63. Wastani wa kiwango cha uzingativu katika Wizara, Idara na Wakala ulikuwa asilimia 68.

Ushauri

Kwa kuzingatia utendaji wa Wizara, Idara na Wakala Mamlaka ya Udhibiti wa Manunuzi ya Serikali ilishauri yafuatayo:

- i) Taasisi za manunuzi zenye utendaji mzuri zipongezwe kwa utendaji wao mzuri.
- ii) Afisa Masuuli, Wenyeviti wa Bodi za Zabuni na Wakuu wa Vitengo vya Manunuzi wa Taasisi za Manunuzi 22 zilizofanya vibaya waitwe mbele ya Bodi ya Wakurugenzi ya Mamlaka ya Udhibiti wa Ununuzi wa Umma ili watoe maelezo juu ya sababu za kufanya vibaya na kuweka mikakati ya kuboresha hali hiyo.

- iii) Taasisi za Manunuzi zilizofanya vibaya watakiwe kuendesha mafunzo kwa wafanyakazi juu ya utumiaji wa Sheria ya Manunuzi ya Umma na Kanuni zake.
- iv) Juu ya mapungufu katika usimamizi wa mikataba, Taasisi zote zenye utendaji mbovu katika viashiria vya usimamizi wa mikataba na udhibiti wa ubora lazima ziongezwe katika orodha ya Taasisi zitakazokaguliwa kwenye kaguzi zijazo za ukaguzi wa thamani ili kutathmini kwa undani kiwango, chanzo na sababu ya mapungufu yaliyoonekana na baada ya hapo kushauri njia za kurekebisha mapungufu hayo.

5.13 Usimamizi wa vifaa

Divisheni ya usimamizi wa vifaa iliandaa na kuwasilisha taarifa ihusuyo usimamizi wa vifaa kwa Taasisi mbalimbali katika mwaka husika. Taarifa hiyo ilionyesha mambo mengi ambayo pia yalijitokeza katika taarifa zangu za miaka iliyopita.

Naishukuru Divisheni ya usimamizi wa vifaa vya Serikali kwa mchango wao ambao nimeona ni muhimu kuujumuisha katika taarifa yangu. Masuala yaliyojitekeza katika taarifa hiyo yameonyeshwa kama kiambatanisho Na. IV cha ripoti hii.

SURA YA 6

UCHAMBUZI WA HESABU JUMUIFU NA DENI LA TAIFA

6.0 Utangulizi

Hesabu Jumuifu za Serikali ya Jamhuri ya Muungano zinaonyesha mapato na matumizi ya Serikali Kuu yanayolenga kulisaidia bunge na wananchi kushinikiza Serikali kuonyesha matumizi ya fedha na shughuli zinazofanywa na Serikali.

Hesabu hizi zinalengo la kuboresha uwazi,kuongeza uwajibikaji,kuipatia sekta ya umma taarifa zilizokamilika,kuhimiza taarifa zinazolinganishwa,kutoa taarifa zilizokamilika ili kusaidia uchambuzi wa fedha wa muda mrefu na kuzitolea maamuzi.Wizara ya fedha inawajibu wa kuzitoa kwa umma hesabu za mwaka ulioishia tarehe 30/6/2012.

Napenda kuonyesha kwamba pamoja na madhumuni ya ripoti hii,Hesabu Jumuifu za Serikali ya Muungano ya Tanzania zinamaanisha; Hesabu Jumuifu za Mapato na Malipo, Hesabu Jumuifu za taarifa ya ulinganisho wa makisio na kiasi halisi kilicholipwa, Hesabu Jumuifu za taarifa ya mtiririko wa fedha, Hesabu Jumuifu za taarifa ya malipo kwa aina ya kazi na vielekezi katika taarifa ya fedha.

Ukaguzi umebaini kwamba Serikali imeshindwa kutengeneza hesabu jumuifu za taasisi zake kama vile Serikali za Mitaa na Mashirika ya Umma kutokana na tofauti katika kutoa taarifa za hesabu kulingana na viwango ambapo ni kinyume na aya ya 6.5 ya Viwango vya Kimataifa vya kihasibu katika Sekta ya Umma kwa misingi ya fedha taslimu [(IPSAS) -cash basis of accounting], ambayo inahitaji chombo kinachodhibiti taasisi zake kutoa hesabu jumuifu za shughuli za taasisi zake nje na ndani ya nchi.

6.1. Tathimini ya Hesabu za Mwisho wa Mwaka

(i) Matumizi ya kawaida (matokeo ya hesabu)

Katika mwaka huu wa fedha utendaji na uchangiaji unaolenga kuonyesha uwazi na uwajibibikaji katika Serikali kuu kwa Matumizi ya Kawaida ni kama ifuatavyo:

Jedwali 22: Matumizi ya kawaida

A	B	C	A-B	B-C
Makisio yaliyo idhinishwa (Sh)	Fedha iliyopelekwa (Sh)	Matumizi yaliyofanyika (Sh)	Pungufu ya fedha iliyopelekwa (Sh)	Bakaa ya fedha ambayo haikutumika (Sh)
9,214,885, 955,263	8,687,230,788 ,550	8,685,275,162,09 4	529,610,793,169	1,955,626,456

Taarifa za fedha jumuifu katika matumizi ya kawaida kwa mwaka huu wa fedha kwa Wizara, Idara na Sekretarieti za Mikoa yalikuwa ni Sh. 8,685,275,162,094 ikilinganishwa na makisio yaliyoidhinishwa ya kiasi cha Sh. 9,214,885,955,263

Taarifa za fedha jumuifu zinaonesha kwamba, jumla ya fedha zilizotolewa na hazina ni Sh. 8,687,230,788,550 kwa ajili ya matumizi ya kawaida ikilinganishwa na matumizi halisi ya Sh.8,685,275,162,094, hii ikiwa na maana kwamba kiasi cha Sh. 529,610,793,169 hakikupelekwa kulingana na makisio yaliyoidhinishwa. Kiasi cha Sh. 1,955,626,456 kilibaki na kurudishwa katika akaunti ya Mlipaji Mkuu wa Serikali iliyopo Benki Kuu.

(ii) Matumizi ya Maendeleo (matokeo ya hesabu)

Katika mwaka huu wa fedha wa ukaguzi, matokeo ya hesabu kwa Matumizi ya maendeleo ilikuwa kama ifuatavyo:

Jedwali 23: Matumizi ya maendeleo.

A	B	C	A-B	B-C
Makisio yaliyo idhinishwa (Sh)	Fedha iliyopelekwa (Sh)	Matumizi yaliyofanyika (Sh)	Pungufu ya fedha iliyopelekwa (Sh)	Bakaa ya fedha ambayo haikutumika (Sh)
4,311,009,39 4,737	3,384,431,758,3 46	3,376,296,146,18 6	926,577,636,391	8,135,612,160

Taarifa za fedha jumuifu zinaonyesha kwamba, jumla ya fedha zilizotumika kwa shughuli za maendeleo ni Sh. 3,376,296,146,186 ikilinganishwa na makisio yaliyoidhinishwa ya Sh. 4,311,009,394,737.

Jumla ya fedha iliyotolewa na hazina ilikuwa Sh. 3,384,431,758,346 ikilinganishwa na kiasi cha Sh. 3,376,296,146,186 ambazo ni fedha zilizotolewa na kutumika ambapo kiasi cha Sh. 926,577,636,391 hakikutolewa kama ilivyoidhinishwa , hali kadharika fedha ambayo haikutumika ilikuwa Sh. 8,135,612,160 fedha ambazo zilirudishwa katika akaunti ya Mlipaji Mkuu wa Serikali iliyopo Benki Kuu.

**(iii) Jumla ya matumizi ya Serikali
Sh.12,061,571,308,295**

Jedwali hapa chini linaonyesha matumizi ya kawaida na ya maendeleo kwa Wizara, Idara zinazojitegemea, Wakala wa Serikali na Serikali za Mitaa kwa miaka 2010/2011 na 2011/2012.

Matumizi ya kawaida yameongezeka kutoka Sh. 7,581,154,383,404 mwaka wa fedha 2010/2011 hadi kufikia Sh. 8,685,275,162,093 mwaka 2011/2012 sawa na asilimia 15, na matumizi ya maendeleo yameongezeka kutoka Sh. Sh.2,218,032,826,357 mwaka wa fedha wa 2010/2011 hadi kufikia Sh. 3,376,296,146,186 kwa mwaka wa fedha 2011/2012 ikiwa ni sawa na asilimia 52 .

Jedwali 24: Jumla ya matumizi yote

Matumizi ya Serikali	2010/2011 (Sh)	2011/2012 (Sh)	mabadiliko ya asilimia (% change)
Matumizi ya kawaida	7,581,154,383,404	8,685,275,162,093	15
Matumizi ya maendeleo	2,218,032,826,357	3,376,296,146,186	52
Jumla	9,799,187,209,761	12,061,571,308,279	23

Kwa ujumla matumizi ya serikali yameongezeka kwa kiasi cha Sh.2,262,384,098,518 sawa na asilimia 23 kutoka Sh.9,799,187,209,209,761 mwaka wa fedha wa 2010/2011 hadi kufikia Sh.12,061,671,308,279 kwa mwaka wa fedha 2011/2012.

(iv) Makusanyo ya maduhuli

Taarifa Jumuifu ya mapato ilioishia tarehe 30 Juni, 2012 inaonyesha makusanyo halisi ya Sh. 12,150,498,773,424 ikilinganishwa na makadirio ya Sh. 13,525,895,350,000 hivyo kuleta upungufu wa makusanyo ya Sh. 1,375,396,576,576 sawa na asilimia 10 ya makisio ya bajeti yaliyoidhinishwa. Mtiririko wa makusanyo ya maduhuli kwa muda wa miaka mitatu ya nyuma ni kama inavyoonekana hapa chini:

Mwaka	2009/2010 (Sh)	2010/2011 (Sh)	2011/2012 (Sh)
makadirio	10,063,686,670,897	11,823,445,375,763	13,525,895,350,000
makusanyo halisi	7,928,122,248,611	11,425,587,436,564	12,150,498,773,424
upungufu wa makusanyo	2,135,564,422,286	397,857,939,199	1,375,396,576,576
Tofauti (%)	21	3	10

Makusanyo katika akaunti ya kawaida yanatokana na kodi mbalimbali, makusanyo yasiyo ya kodi na makusanyo kutokana na rasilimali za serikali ambapo makusanyo katika akaunti ya maduhuli ya maendeleo yanayotokana na misaada ya wafadhili, mikopo ya nje na ndani ya nchi.

6.2 Taarifa ya misaada ya nje

Taarifa jumuifu ya misaada ya nje hadi kufikia tarehe 30/6/2012 inaonyesha jumla ya makusanyo ya nje ya Sh.3,168,234,333,111.22 ikilinganishwa na makisio yaliyoidhinishwa ya Sh.5,195,184,967,780 na kusababisha upungufu wa makusanyo kwa kiasi cha Sh.2,026,950,634,699 sawa na asilimia 39 ya makisio ya bajeti yaliyoidhinishwa hii inamaanisha kwamba lengo la serikali katika kukusanya mapato halikufikiwa.

Ukaguzi unapendekeza kwamba Serikali ijitahidi kufikia makusanyo ya mapato ya mwaka kwa kutegemea vyanzo vya ndani badala ya kutegemea misaada kutoka nje ambayo kufikia mwisho wa mwaka inakuwa haitolewi kama ilivyokusudiwa.

6.3 Taarifa ya Madeni yasiyolipwa Sh.432,443,000,129

Taarifa jumuifu ya hesabu za taifa zinaonyesha madeni yasiyolipwa kiasi cha Sh. 432,443,000,129 kwa mwaka wa fedha ulioishia tarehe 30/6/2012 (2011: Sh.577.5 Bilioni). Kitendo cha kuweka matumizi tarajiwu ni kijume na taratibu za Viwango vya Kimataifa vya Kihasibu katika Sekta ya Umma kwa misingi ya fedha taslimu [(IPSAS) - cash basis of accounting] na kanuni namba 53(1),(3) - (5) ya Fedha za Umma ya mwaka 2001 (iliyorekebishwa 2004) ambayo inasema kwamba hesabu za fedha za Serikali ni lazima ziwe katika misingi ya fedha taslimu (cash basis of accounting) na hakuna Afisa Masuuli atakayeruhusiwa kuingiza katika vitabu vya hesabu za Serikali makusanyo ya mapato na malipo ya matumizi ya Serikali yaliyotarajiwu. Kanuni zinasisitiza kwamba, kitendo hicho cha kuingiza deni katika vitabu vya hesabu kabla halijalipwa linakingana na kanuni za bunge za kuitisha matumizi kabla ya kutumia. Aidha, kanuni ya 54 (4) ya Fedha za Umma ya mwaka 2001, inazuia Maafisa Masuuli kuhamisha fedha za matumizi ya mwaka mmoja kwenda mwaka mwingine, fedha za matumizi zilizohamishwa kwenda mwaka mwingine zinatakiwa kuchukuliwa kama fedha za matumizi yasiyo halali.

6.4 Taarifa ya Mihadi ambayo haijalipwa Sh.134,148,478,322

Taarifa jumuifu ya hesabu za serikali zinaonyesha kiasi cha Sh. 134,148,478,322 ambazo ni mihadi ambayo haijalipwa kufikia tarehe 30/6/2012. Hii inaonyesha kwamba, Maafisa Masuuli waliweka hizi mihadi kipindi cha kuelekea mwisho wa mwaka katika kujaribu kutumia kiasi cha fedha chote kilichokuwepo katika vifungu vyao ili kuzuia kurudisha fedha katika Mfuko Mkuu wa Serikali. Kukosekana kwa udhibiti wa wazi, kunasababisha fedha za serikali kutumika katika

matumizi ambayo yangeweza kuepukika,na hivyo kuokoa fedha ya umma kutokana na usimamizi mbovu kipindi cha mwisho wa mwaka wa fedha.Ukaguzi unapendekeza kuwa kwamba Serikali ichukue hatua madhubuti ambazo zitapunguza hali ya kuingia miyadi isiyo muhimu na kuingia gharama mwisho wa mwaka kwa wizara na Taasisi zake,ambazo zinahitajika kisheria kurudisha bakaa ya fedha ambayo haikutumika katika Mfuko wa Mlipaji Mkuu wa Serikali.

6.5 Taarifa ya malimbikizo ya Maduhuli

Taarifa jumuifu ya hesabu za serikali inaonyesha kuongezeka kwa malimbikizo ya maduhuli kutoka Sh. 26,697,463,538 mwaka 2010/2011 hadi kufikia Sh.98,774,320,855 mwaka 2011/2012, ikiwa ni ongezeko la asilimia 77. Udhibiti uliowekwa na Serikali mpaka sasa haujaweza kuinua ukusanyaji wa mapato, na kusababisha makusanyo ya mapato kuwa chini ya makisio na kuilazimisha Serikali kugharamia bajeti kwa kutumia mikopo ya ndani ya nchi.

Pamoja na hayo, hesabu zilizowasilishwa na Wizara ya Nishati na Madini hazikuonyesha malimbikizo ya maduhuli yanayofikia Sh.1,645,582,899 pamoja na ukweli kuwa na Sh.503,412,412 kati ya kiasi hicho ambacho hakikuonyeshwa, yalikuwa hayajakusanywa kutoka mwaka wa nyuma kama inavyoonyeshwa kwenye taafia ya mwaka 2010/2011 zaidi ya hayo, ukaguzi uliofanyika mikoani kwenye vituo 13 ulibaini kuwa kulikuwa na maduhuli yasiyo kusanywa kutoka miaka ya nyuma yanayofikia kiasi cha Sh.1,142,170,487.
Pia, hesabu za Wizara ya Ardhi, nyumba na Maendeleo ya Makazi kwa mwaka unaoishia tarehe 30 Juni, 2012 zilionyesha maduhuli yasiyokusanywa ya Sh.352,873,364.88.

6.6 Taarifa ya upotevu Sh.13,024,783,230

Taarifa ya hesabu jumuifu ilionyesha kwamba jumla ya hasara iliyoingiwa na Serikali katika maeneo ya fedha za umma na mali, ilikuwa Sh. 13,024,783,230 ikilinganishwa na Sh. 12,968,168,985 katika mwaka 2010/2011 hili likiwa ni

ongezeko la Sh. 56,614,245 sawa na asilimia 0.44. Serikali haijachukua juhudini madhubuti ili kupunguza matukio ya hasara au kuanzisha mchakato kwa ajili ya Bunge kufuta hasara hizi.Ukaguzi unahimiza serikali kuchukua hatua madhubuti katika kupunguza hasara.

6.7 Ufutiliaji wa mchakato wa malipo ya mirathi katika mahakama za mwanzo

Ukaguzi katika ofisi za Hazina ndogo ulionyesha kiasi kikubwa cha pesa kilicho katika akaunti ya amana ya mirathi kama mapato katika banki ambayo hayamo katika daftari la mapato na matumizi (cash book) na hundi zilizokwisha muda wake ambazo hazijachukuliwa na walengwa. Katika kukamilisha zoezi la ukaguzi na kupata ushahidi wa kutosha, iliamuliwa kuongeza mawanda ya ukaguzi kwa kutembelea mahakama za mwanzo wakati ambapo wilaya kumi (10) ambazo ni Ilala, Kinondoni, Temeke, Morogoro, Kilombero, Tanga, Muheza, Korogwe, Bagamoyo and Kibaha zilitembelewa ili kugundua chanzo cha tatizo na kulitolea mapendekezo kwa Serikali.Kutokana na ukaguzi huo tulibaini mapungufu yafuatayo:

- Kiasi kidogo cha pesa kulipwa kwa hundi**

Tuligundua kwamba walengwa hulipwa hundi ambazo zinawalazimu kufungua akaunti benki.Kutokana na kiasi kidogo cha pesa, kama sh. 10,000 na taratibu za kufungua akaunti benki, walengwa wanaamua kutopeleka hundi zao benki kwa ajiri ya malipo na hivyo basi hundi zinakwisha muda wake zikiwa mikononi mwao.

- Hundi kuchelewa kufika katika mahakama za mwanzo**

Tuligundua ucheleweshaji wa hundi katika mchakato wa kuzisambaza kutoka katika hazina ndogo mpaka kwa Hakimu wa Wilaya ambapo hundi huchukuliwa kwa kipindi cha kati ya wiki moja mpaka mbili. Pia tulibaini kuwa,Hakimu wa Wilaya ni lazima asubiri kwa mahakama husika ya mwanzo kuja kuchukua hizo hundi ambapo inachukua muda wa wiki nne mpaka sita.Muda wa wastani wa kuchelewa ni wiki nane hali

ambayo inaongeza hatari ya hundi kupita muda wake kabla ya kuchukuliwa.

- **Ucheleweshaji katika kukabidhi hundi kwa walengwa katika mahakama za mwanzo**

Katika mahojiano na wafanyakazi katika mahakama za mwanzo, ilionekana kwamba hakuna mawasiliano ya mara kwa mara na yaliyo rasmi ambayo yanafanywa na Mahakama za mwanzo kwenda kwa walengwa ili kuwataarifu juu ya hundi zilizopo.

- **Kutokuwepo na mwamko wa umma kuhusu taratibu za Mirathi**

Pia, ukaguzi ulibaini kuwa, hundi zilizokwisha muda wake zilikuwa mikononi mwa walengwa na walikuwa hawaelewi kama hundi hizo zimekwisha muda wake.

- **Kutokuwepo kwa utunzaji mzuri wa kumbukumbu katika Mahakama za mwanzo**

Hundi zimekuwa zikitolewa bila ya kunukuu namba ya kesi kitu ambacho kinasababisha ugumu katika kufuatilia uhamishwaji na ulipaji katika daftari la kumbukumbu.

- **Ukosefu wa wafanyakazi wenye sifa katika Mahakama za mwanzo**

Mahakama za Mwanzo hazina wafanyakazi wakutosha wenye sifa zinazotakiwa katika utendaji wa kazi wa kila siku, hali inayosababisha kazi za karani kama vile utunzaji wa kumbukumbu za hesabu kufanywa na mhudumu wa ofisi na mlinzi. Tuligundua hundi kadhaa zilizokwisha muda wake zikiwa katika uangalizi wao bila ya kufahamu kwamba zimekwisha muda wake.

- **Kukosekana kwa ufuatiliaji na kazi zinazohusiana na ukaguzi wa ndani**

Wizara ya Fedha haijaanzisha taratibu za ufuatiliaji wa hundi za Mirathi.Aidha, ukaguzi wa ndani haujawahi kufanya mapitio na ufuatiliaji wa mchakato wa malipo ya mirathi.

- **Utunzaji mbovu wa taarifa katika Mahakama za Mwanzo na za wilaya**

Tuligundua Utunzaji mbovu wa taarifa katika Mahakama za wilaya.Daftali za kumbukumbu mbalimbali na daftali la kutuma nyaraka hazikuwa na taarifa zinazoendana na wakati na pia wakati mwingine,daftali hizo zinakuwa zimepotea na kuisababishia mahakama usumbuwa wa kufuatilia mafaili. Hali hii wakati mwingine inasababisha upotevu wa hati za malipo na mafaili.

Ukaguzi unapendakuishauri serikali kama ifuatavyo:

- (a) Ofisi ya Mkaguzi Mkuu wa ndani inatakiwa kupewa taarifa juu ya udhaifu ulioonekana katika Mahakama za Mwanzo ili iweze kufanya tathimini ya kina ya mchakato wa malipo ya mirathi kwa Mahakama zote za Mwanzo na kutambua hundi zote zilizopita muda wake kwa ajiri ya kurekebisha hesabu katika vitabu vya hesabu za serikali.
- (b) Serikali kuongeza ufanisi katika mawasiliano na usafirishaji katika Mahakama za Mwanzo na za Wilaya kwa kuwapatia kompyuta,simu na magari kwa ajiri ya usimamizi mzuri wa mirathi.
- (c) Kuanzisha kamati ya uratibu kwa ajiri ya ufuatiliaji mzuri wa shughuli za mirathi
- (d) Kuanzisha utaratibu maalum wa kusimamia malipo ya mirathi
- (e) Kuboresha utunzaji wa nyaraka na kumbukumbu za Mahakama kwa ajiri ya kurahisisha ufuatiliaji wa taarifa za mirathi.
- (f) Kuwapatia wafanyakazi wa mahakama semina zinazohusiana na shughuli zao ili kuboresha ujuzi na uwezo wao.

- (g) Kufanya mawasiliano ya mara kwa mara kati ya Msimamizi wa Mirathi na karani wa Mahakama ili kufuutilia malipo yao.
- (h) Kufanya mawasiliano ya simu ya mara kwa mara kati ya mwajiri, Hazina Ndogo na Hazina Makao makuu ili kuweza kufanya ufuutiliaji wa malipo.
- (i) Karani wa Mahakama awe na orodha ya hundi zilizolipwa kutoka Hazina ndogo katika mbao za matangazo ili kuwawezesha watu kusoma na kufahamu hali halisi ya malipo yao.

6.8 Bakaa ya fedha taslimu za Serikali na zilizoko benki

Ukaguzi wa hesabu jumuifu za Jamhuri ya Muungano wa Tanzania ulibaini kuwepo kwa kiasi cha Sh. 1,137,662,034,854.85 katika akaunti Na. 1900170001 kama bakaa ya mwanzo wa mwaka. Hata hivyo, bakaa hii haikuonyeshwa kama bakaa ya mwisho wa mwaka uliopita, kwa hali hiyo usahihi wa hali halisi ya fedha katika akaunti hiyo haukuweza kuthibitishwa.

6.9 Mwenendo wa Deni la Taifa

Napenda kutaarifukuwa, katika kipindi cha mwaka wa fedha ulioishia tarehe 30 Juni, 2012, jumla ya deni la Taifa lilikuwa Sh. 16,975.9 bilioni ukilinganisha na Sh.14,441.6 bilioni iliyoripotiwa mwaka 2011 hivyo kuwa na ongezeko la Sh. 2,534 bilioni sawa na asilimia 17.6 ikilinganishwa na mwaka jana. Katika deni la Sh.16,975.9 billioni, deni la nje ni Sh.12,430.068 billioni sawa na asilimia 73 na deni la ndani ni Sh.4,545.9 billioni sawa na asilimia 27 ya deni lote.

Hadi kufunga mwaka wa fedha deni la nje ni sh.12,430.068 bilioni ikilinganishwa na Sh.10,734.32 bilioni kwa mwaka uliopita hivyo kuwa na ongezeko la Sh.1,695,75 bilioni lililo sababishwa na ukopaji mpya, malimbikizo ya riba, na kushuka kwa thamani ya Shillingi ukizilinganisha na fedha za nje. Sehemu kubwa ya deni ilitumika katika urari wa malipo na kusaidia bajeti, ustawi wa jamii na elimu, usafiri na mawasiliano.

Kwa upande wa deni la ndani liliongezeka kwa sh. 838.6 billioni kutoka Sh.3,707.3 bilioni mwaka 2011 hadi Sh.4,545.9 bilioni kufikia tarehe 30 Juni, 2012, fedha hizo zilitumika katika uendeshaji wa bajeti ya Serikali.

kuongezeka kwa deni la ndani kulitokana na uamuzi wa Serikali wa kubadilisha deni katika akaunti ya benki yake iliyoko Benki Kuu kwa kiasi cha Sh. 469.48 bilioni kuwa dhamana maalumu ya miaka 10 ili kuijengea Serekali uwezo wa kifedha kwa ajili kupata amana ya muda mfupi kutoka Benki Kuu ya Tanzania kwa ajili ya utekelezaji wa bajeti yake. Aidha, Serikali imekuwa na mwelekeo wa malipo ya riba kuongezeka ukisababishwa na madeni ya ndani na nje kama ilivyoainishwa kwenye jedwali hapa chini.

Jedwali 27: Malipo ya riba kwa miaka mitano iliyopita:

Wadeni	2007/08	2008/09	2009/10	2010/11	2011/12
Multilateral	20.29	26.75	26.32	51.41	62.58
Bilateral	8.07	4.06	1.47	11.07	2.61
Commercial/Exp.	-	5.09	0.81	2.58	20.42
Jumla Ndogo	28.36	35.90	28.60	65.06	85.61
Domestic	241.64	208.35	229.39	271.64	328.75
Jumla Kuu	270.0	244.25	257.99	336.70	414.36

Chanzo: Wizara ya fedha

Pamoja na hali ya deni iliyonyeshwa hapo juu, Serikali ina madeni ambayo hayakujumuishwa kwenye deni la Taifa kama ilivyoonyeshwa kwenye aya zifuatazo hapa chini na kupelekea taarifa za deni la taifa kuwa na shaka.

- Kuna madai ya PSPF ya shilingi 716,600,000,000, kati ya madai ya jumla ya shilingi trilioni 3.2 ikiwa ni kwa ajili yakiwa ni michango ya pensioni kwa wafanyakazi wa Serikali ambayo Serikali imekubali kulipa kwa awamu kumi kwa kiasi cha Sh.71,660,000,000 kila mwaka wa fedha. Deni hili la Serikali halijajumuishwa kwenye deni la Taifa.

- Kuna madai ya Shirika la Ndege la Afrika Kusini na Citi Bank kiasi cha Dola 4,129,298.38 na Dola 1,460,000 sawa na Sh.6.5bilioni na Sh.2.3 bilioni sawia dhidi ya kampuni ya Ndege ya Tanzania. Madeni haya yatakayolipwa na Serikali kupitia Wizara ya Fedha (fungu 50). Deni hili linajumuishwa kwenye deni la Taifa.
- Serikali ilitoa dhamana kwa Wizara, Idara, Serikali za Mitaa na Mashirika ya Umma kwa ajili ya mikopo iliyotolewa kutoka mifuko ya pensheni ambayo Serikali inalipa kupitia kwenye bajeti kama ilivyoripotiwa katika rasimu ya Taarifa ya uhimilifu wa deni la Taifa. Madeni hayo yanafikia Sh.1,250,013,500,000. Fedha hizo zilitumika katika miradi ya ujenzi wa chuo Kikuu Dodoma, Ofisi za TAKUKURU, na nyumba za polisi. Hata hivyo madeni hayo hayajumuishwa kwenye Deni la Taifa.

6.10 Dhamana za Serikali zilizopita muda wake Sh. 799,596,351,405.64

6.10.1 Dhamana kwa Makampuni yanayouza bidhaa nje ya nchi Sh. 300,100,925,004

Kufikia mwishoni mwa mwaka wa fedha (30/06/2012) kulikuwa kuna dhamana yenye jumla ya Sh.300,100,925,004. Kati ya kiasi hicho, dhamana za jumla ya Sh. 78,921,135,217.03 zilikuwa zimeisha muda wake hadi ninapoandika taarifa hii (Februari, 2013) ikimaanisha kuwa jukumu la kulipa mikopo hiyo linakuwa ni la mdhamini (Serikali). Kwa mwelekeo, dhamana za Serikali chini ya utaratibu wa mauzo ya bidhaa nje ya nchi ziliongezeka kutoka Sh.251,211,629,902.92 mwaka 2010/2011 hadi Sh.300,100,925,004.53 mwaka 2011/2012 ikiwa ni ongezeko la Sh.48,889,295,101.61 sawa na asilimia 19%.

6.10.2 Dhamana kwa wafanyabiashara wadogo na wakati Shs.824,959,876

Katika kundi hili, kulikuwa na dhamana tano ambazo muda wake ulikuwa umepita. Kimwelekeo hapakuwa na mabadiliko yoyote ya dhamana kati ya mwaka 2010/2011 na 2011/2012.

Kwa upande wa dhamana kwa mauzo ya bidhaa nchi za nje, athari za dhamana hizo kupita muda wake ni zile zile kwa waliopewa dhamana hiyo na Serikali.

6.10.3 Dhamana zilizotolewa kwa madeni ya Mashirika ya Umma Sh.498,670,466,525.11

Hali ya dhamana zilizotolewa na Msajili wa Hazina inaonyesha kuwa dhamana zilizotolewa kwa Mashirika mbalimbali zilifikia kiasi cha Sh.484,670,466,525.11 hadi kufikia mwisho wa mwaka wa fedha. Hata hivyo, hatua mbalimbali zilikuwa zikiendelea kuhusiana na dhamana hizo ambazo tayari muda wake ulikuwa umepita, mikopo ya muda mfupi iliyotolewa ambayo nayo muda wake ulikuwa umepita ambayo haiwezi kurejeshwa katika Taasisi za fedha. Jumla ya mikopo hii na dhamana ilifikia kiasi cha Sh.206,867,448,332 na Dola za Kimarekani 42 milioni hadi kufikia tarehe 30 Juni, 2012 kama inavyoonekana hapa chini:

- Bakaa ya Mikopo ya benki ya muda mfupi ya kiasi cha Sh. 1,648,936,493 kilikuwa hakijalipwa na Mamlaka ya Mkonge. Mamlaka hii iko chini ya mfilisi; kulingana na taarifa ya Msajili wa Hazina Shirika Hodhi la Mashirika ya Umma linategemewa kufidia deni hilo kutokana na fedha zinazotokana na mapato ya ufilisi.
- Bakaa ya mikopo ya benki ya muda mfupi ya Sh. 3,065,026,923 ilikuwa inadaiwa kutoka kwa Kampuni ya State Motor Corporation; mchakato wa ufilisi umeweza kupata kiasi cha Sh.194,156,393. Bodi iliamua kufuta kiasi kilichosalia.
- Chama cha Ushirika cha Mara kilikuwa na deni la 8,502,977,181 lililokuwa linadaiwa na NBC/CHC. Serikali kupitia maamuzi ya baraza la Mawaziri Na. 10/2005 iliamua kuchukua madeni ya Chama cha Ushirika cha Mara kutoka na Chama hicho kushindwa kulipa.
- SUKITA inadaiwa na NBC/CHC kiasi cha Sh. 10,139,494,512.90; inatarajiwa kufidia kiasi hicho kutokana na mchakato wa ufilisi unaoendelea.
- General Tyre (EA) ina bakaa ya mkopo wa kiasi cha 18,276,168,539 unaodaiwa na NSSF na sasa hivi Kampuni

- haiendelei na uzalishaji. Serikali iko katika mazungumzo na Continental AG kuhusu namna kufufua kiwanda hicho
- Bodi ya Mikopo ya Elimu ya Juu (HESLB) inadaiwa mikopo ya kiasi cha Sh. 121,607,477,900.06 ambayo ilipaswa kuwa imeshalipwa hadi kufikia tarehe 30 Juni, 2009. Kutokana na taarifa za Msajili wa Hazina, HESLB haina uwezo wa kulipa mkopo huo pamoja na riba.
 - Shirika la Ndege la Tanzania (ATCL) lilikuwa na mkataba wa kukodi ndege aina ya Airbus A.320 ambao muda wake ulikuwa umekwisha na ilikuwa inadaiwa gharama za kukodi ndege hiyo za jumla ya Sh.1,696,681,480.48. Aidha, ATCL ilikuwa na deni la Dola za kimarekani 42 milioni kutoka kampuni ya Kiliberia lililodhaminiwa na serikali. Serikali imekwishaanza kulipa mkopo huo.
 - Kampuni ya Mbolea Tanzania ilikuwa na deni la kiasi cha Sh.41,930,630,685,304 ambalo halilipiki kutoptana na matatizo ya kifedha yanayoikabili Kampuni.

Matatizo haya yamesababishwa na mambo yafuatayo:

- Kukosekana kwa dhamana iliyowekwa ili kufidia hasara hiyo.
- Kuahidi dhamana ambayo ufuatiliaji wake kisheria hautekelezezi.
- Kukosekana kwa uchambuzi yakinifu wa uwezo wa Kampuni kukopesheka.

SURA YA 7

UWASILISHAJI NA UCHAMBUZI WA MATOKEO YA UKAGUZI

7.0 Utangulizi

Sura hii, inachambua misingi ambayo imepelekea utoaji wa aina fulani ya maoni ya ukaguzi. Uchambuzi huu una lengo la kufafanua vigezo na msingi iliyotumika katika kutoa maoni ya ukaguzi kama iliyoyjadiliwa katika sura iliyotangulia.

Hati ya ukaguzi ni maoni rasmi au kukataa kutoa maoni kunakotolewa na mkaguzi huru kutokana na ukaguzi au tathmini iliyofanywa kwa Taasisi au Idara yake (mkaguliwa). Hati hii hutolewa ili kumwezesha mtumiaji wa taarifa za fedha kama hakikisho ili aweze kufikia maamuzi kutokana na matokeo ya ukaguzi uliofanywa.

Hati ya ukaguzi huchukuliwa kama nyenzo muhimu wakati wa kutoa taarifa za fedha kwa watumiaji. Inakusudia kulishauri Bunge na watumiaji wengine wa taarifa za Wizara/Idara na Sekretarieti za Mikoa kama taarifa za fedha zimetayarishwa kwa kuzingatia viwango kubalifu vya Kimataifa vya kutayarisha taarifa za fedha katika sekta ya Umma (IPSAS) na kwa namna inavyotakiwa chini ya Kifungu cha 25 (4) cha Sheria ya Fedha za Umma ya mwaka 2001 (zilizorekebishwa 2004) ikiwemo Wizara/Idara na Sekretarieti za Mikoa kuzingatia Sheria na Kanuni nyingine zilizowekwa.

Kwa lugha ya kawaida, hati ya ukaguzi ni hakikisho kwamba taarifa ya fedha iliyowasilishwa na mkaguliwa kwa kiwango kikubwa ni sahihi na ya kuaminika kwa ajili ya kufanya maamuzi ya Serikali kama vile Serikali kutathmini kama fedha zilizotengwa kwa ajili ya Wizara/Idara/Wakala na Sekretarieti za Mikoa zimetumika kwa manufaa ya Umma. Ni muhimu kutambua kwamba hati ya ukaguzi inayotolewa kwa taarifa za fedha siyo hakikisho la moja kwa moja kwamba hali ya kifedha ya Taasisi ni nzuri na sahihi kabisa kuweza kutegemewa katika kufanya maamuzi. Hati ya ukaguzi ni maoni tu kwamba taarifa iliyowasilishwa ni sahihi na haina

makosa makubwa ambapo maamuzi mengine huachiwa mtumiaji wa taarifa kuamua.

7.1 Aina ya hati za ukaguzi

Kuna aina tano (5) za hati za ukaguzi, kila moja ikieleza mazingira tofauti anayokutana nayo mkaguzi. Hati hizo ni kama ifuatavyo:

(i) Hati inayoridhisha

Wakati mwingine hati hii huchukuliwa na wengi kama “hati safi”. Aina hii ya hati hutolewa wakati taarifa za fedha zilizowasilishwa hazina makosa mengi na zimezingatia matakwa ya viwango vya Kimataifa vya Uhasibu katika Sekta ya Umma (IPSAS) na kwa mujibu wa Kifungu cha 25 (4) cha Sheria ya Fedha za Umma ya mwaka 2001 (iliyorekebishwa 2004) ikihusisha uzingatiaji wa Sheria na Kanuni.

- **Hati inayoridhisha yenye masuala ya msisitizo**

Katika mazingira fulani, hati ya ukaguzi inayoridhisha huweza kurekebishwa kwa kuongeza aya yenye masuala ya msisitizo yanayodokeza masuala muhimu ambayo yasiporekebishwa na mkaguliwa yanaweza kusababisha kutolewa kwa hati yenye shaka katika ukaguzi unaofuata. Kuongezwa kwa aya ya masuala ya msisitizo hakuathiri hati ya ukaguzi iliyotolewa.

Madhumuni ya masuala ya msisitizo ni kutoa uelewa zaidi kwa hali iliyotokea wakati wa ukaguzi licha ya kutolewa kwa hati ya ukaguzi inayoridhisha.

- **Hati yenye shaka**

Hali na mazingira inayosababisha kutolewa kwa hati hii, huwa katika kundi moja au mawili ambayo ni:

- **Kunapokuwa na mashaka ambayo husababisha mkaguzi ashindwe kutoa hati ya ukaguzi.**

Mambo yanayoweza kusababisha kutolewa kwa hati hii ni haya yafuatayo:

- Matumizi yasiyokuwa na hati za malipo
- Bidhaa na huduma zimenunuliwa bila kuwa na hati za kupokelea hivyo kukosekana uhakikisho kama zimepokelewa na kuingizwa katika vitabu
- Malipo mbalimbali kukosa viambatanisho
- Stakabadhi za maduhuli kutowasilishwa kwa ajili ya ukaguzi
- Mali zinazomilikiwa au kununuliwa kukosa majedwali. Hii inasababisha mashaka ya kuwepo kwa mali hizo
- Kutopatikana kwa ushahidi wa mapokezi ya fedha zilizolipwa. Kutokuwepo stakabadhi za kukiri mapokezi kutoka kwa walipwaji unawenza kusababisha upotevu wa fedha. Katika hali hii kunakuwa na ufinyu wa mawanda ya ukaguzi.

Pale ambapo mkaguzi anapotoa maoni yanayotofautiana na hali halisi ya taarifa ya fedha zilizotolewa (kutokubaliana na taratibu kubalifu za utunzaji na uzingatiaji wa sheria na kanuni).

Kutokubaliana na uongozi katika njia ilio bora ya utunzaji wa kumbukumbu na uzingatiaji wa sheria hutokea katika mazingira yafuatayo:

- Mali zinazomilikiwa na Wizara/Idara na Sekretarieti za Mikoa kutoingizwa katika rejista.
- Mali zilizonunuliwa kutoingizwa vitabuni na hivyo kutolewa na matumizi yake kutoweza kuthibitishwa.
- Kutobainishwa salio la benki katika vitabu vyta fedha
- Wakati kumbukumbu za hesabu zinapokosekana, kutokamilika au kutokuwa sahihi.
- Kutobainishwa kikamilifu kwa sera ya uhasibu iliyotumika
- Pale ambapo Wizara/Idara na Sekretarieti za Mikoa zinapotumia njia isiyo sahihi kama vile viwango vyta uchakavu visivyo sahihi.

Kwa hali hiyo, hati yenye shaka inaonyesha kuwa taarifa za fedha zilizowasilishwa ni sahihi isipokuwa kwa madhara yatokanayo na masuala halisi ya kiukaguzi yaliyogunduliwa.

(iii) Hati isiyoridhisha

Hati isiyoridhisha hutolewa inapogundulika kuwa taarifa za fedha za Wizara/Idara na Sekretarieti za Mikoa kwa kiasi kikubwa si sahihi zinapoangaliwa katika ujumla wake, hazikuandaliwa kwa kuzingatia Viwango vya Kimataifa vya Uhasibu katika Sekta ya Umma (IPSAS) na kwa namna inayotakiwa katika Kifungu cha 25(4) cha Sheria ya Fedha za Umma ya mwaka 2001 (iliyorekebishwa 2004) inayoelezea kuwa taarifa zilizopo siyo sahihi na haziaminiki katika kupima matokeo ya uendeshaji katika Wizara/Idara/Wakala na Sekretarieti za Mikoa.

Maelezo ya hati isiyoridhisha huwa wazi ambapo ninaeleza kwamba taarifa za fedha hazikuzingatia Viwango vya Kimataifa vya Uhasibu katika Sekta ya Umma (IPSAS) na kwa namna inayotakiwa katika Kifungu cha 25(4) cha Sheria ya Fedha za Umma ya mwaka 2001 (iliyorekebishwa 2004).

(iv) Hati mbaya

Hati mbaya ambayo hujulikana kama kukataa kutoa hati, hutolewa wakati ninaposhindwa na hivyo kukataa kutoa hati kwa taarifa za fedha. Aina hii ya hati hutolewa ninapajaribu kufanya ukaguzi kwa Taasisi na kushindwa kutokana na sababu mbalimbali na hivyo kusababisha kutotoa hati ya ukaguzi. Hali inayosababisha kutolewa kwa hati mbaya inaweza kusababishwa na kukosekana kwa uhuru au ufinyu mkubwa wa mawanda ya ukaguzi ama kwa makusudi au la, mkaguliwa kukataa kutoa ushahidi na taarifa zinazotakiwa katika maeneo muhimu kwenye taarifa za fedha na panapokuwa na mashaka makubwa katika uendeshaji wa shughuli za mkaguliwa.

Jedwali 27: Misingi ya kutoa hati ya ukaguzi

Hali na sababu zinazosababisha kutolewa kwa hati ya ukaguzi	Masuala yenyé athari lakini si mazito	Masuala yenyé athari na mazito
Taarifa za fedha ni za kupotosha	Hati yenyé shaka	Hati isiyoridhisha
Kushindwa kupata ushahidi wa kutosha na sahihi		Hati mbaya

Jedwali hilo hapo juu hutoa mwongozo wa namna hati za ukaguzi zinavyotolewa, tafsiri yake ni kama ifuatavyo:

Pale ninapogundua masuala yanayosababisha kutokubaliana na masuala hayo ni yenyé athari lakini si mazito, ninatoa hati yenyé shaka (isipokuwa pale ambapo masuala yana athari na ni mazito hati isiyoridhisha hutolewa)

- (b) Pale ambapo matokeo ya ukaguzi yanayosababisha kuwepo mashaka na:
 - (i) Mashaka hayo ni makubwa yana athari lakini si mazito, hati yenyé shaka hutolewa
 - (ii) Mashaka yana athari na ni mazito, hati mbaya hutolewa

Madhumuni ya Ofisi ya Taifa ya Ukaguzi ni kutoa ripoti ya ukaguzi ambayo inaonyesha uwiano ulio wazi, kuweka msisitizo kwa mambo muhimu yanayohitaji kushughulikiwa na uongozi wa wakaguliwa na kubainishwa fursa za kuboresha utendaji.

Jumla ya Wizara 93 na Sekretarieti za Mikoa 21 zilikaguliwa katika mwaka wa fedha 2011/2012 na matokeo yake ni kama ifuatavyo:

7.2 Hati inayoridhisha isiyokuwa na masuala ya msisitizo

Wizara/Idara na Sekretarieti za Mikoa 47 (41.2%) kati ya 114 zilizokaguliwa mwaka huu zilipewa hati inayoridhisha isiyo na masuala ya msisitizo kama inavyoonekana katika Kiambatisho VI

7.3 Hati inayoridhisha yenye masuala ya msisitizo

Matokeo ya ukaguzi ya mwaka huu yalionyesha kuwa kati ya Wizara/Idara na Sekretarieti za Mikoa 114 zilikaguliwa, 61 au asilimia 53.5% zilipewa hati zinazoridhisha zenye masuala ya msisitizo.

7.4 Hati yenye shaka

Kati ya Wizara/Idara na Sekretarieti za Mikoa 114 zilizokaguliwa, 6 au asilimia 5.3% zilipewa hati yenye shaka.

7.5 Hati isiyoridhisha

Hapakuwa na fungu lolote katika Wizara/Idara na Sekretarieti za Mikoa 114 zilizokaguliwa katika mwaka 2011/2012 lililopewa hati isiyoridhisha. Pia hakuna fungu lililopewa hati isiyoridhisha katika mwaka uliopita 2010/2011. Hali hii inaonyesha kukua kwa kiwango cha matumizi mazuri ya fedha za umma ukilinganisha na 2009/2010 ambapo hati kama hii ilitolewa kwenye wizara moja na Sekretarieti ya Mkoa moja.

7.6 Hati mbaya

Katika ukaguzi wa mwaka wa fedha 2011/2012 hapakuwa na hali iliyosababisha ufinyu wa wigo wa ukaguzi kiasi cha kulazimika kutoa hati mbaya

Jedwali lifuatalo linaonyesha aina ya hati zilizotolewa kwa Wizara/Idara na Sekretarieti za Mikoa katika taarifa za fedha kwa mwaka ulioishia tarehe 30 Juni, 2012.

Jedwali 28: Muhtasari wa hati za ukaguzi

Maelezo	Hati inayoridhish hisha	Hati inayoridhis ha yenye masuala ya msisitizo	Hati yenye shaka	Hati isiyoridh isha	Hati mbaya	Jumla
Wizara/Idara	40	47	6	0	0	93
Sekretarieti za Mikoa	7	14	0	0	0	21
Jumla	47	61	6	0	0	114

7.7 Wizara /Idara na Sekretarieti za Mikoa zilizopewa hati inayoridhisha.

Wizara /Idara na Sekretarieti za Mikoa 47 zimepewa hati inayoridhisha kama inavyoonyeshwa kwenye kiambatisho Na.Vi.

7.8 Wizara/Idara na Sekretarieti za Mikoa zilizopewa hati inayoridhisha yenye masuala ya msisitizo

Ufuatao ni mchanganuo wa sababu za kutoa hati inayoridhisha yenye masuala ya msisitizo kwa kila fungu:

1.	Fungu 16: Ofisi ya Mwanasheria Mkuu
	Taarifa za fedha za Ofisi ya Mwanasheria Mkuu zimeonyesha kuwepo kwa kiasi cha Shs.700,206,684.88. ikiwa ni mihadi mwishoni mwa mwaka wa fedha 2011/2012. Hii ni kinyume na Mfumo kubalifu wa kiuhasibu wa IPSAS unaotambua mapato na matumizi kwa fedha taslimu.
2.	Fungu 18: Mahakama Kuu
	Taarifa za fedha za Mahakama Kuu zimeonyesha kuwepo kwa kiasi cha Shs.1,370,887,399 fedha za matumizi ya kawaidaikiwa ni madeni yasiyolipwa mwishoni mwa mwaka wa fedha 2011/2012. Hii ni kinyume na Mfumo kubalifu wa kiuhasibu wa IPSAS unaotambua mapato na matumizi kwa fedha taslimu. Pia inaathiri utekelezaji wa shughuli zilizo kasimiwa katika mwaka husika wa fedha.

3	Fungu 19: Mahakama za Mwanzo
	<p>Taarifa za fedha za Mahakama za Mwanzo zimeonyesha kuwepo kwa kiasi cha Sh.868,507,866 fedha za matumizi ya kawaidaikiwa ni madeni yasiyolipwa mwishoni mwa mwaka wa fedha 2011/2012. Hii ni kinyume na Mfumo kubalifu wa kiuhasibu wa IPSAS unaotambua mapato na matumizi kwa fedha taslimu. Pia inaathiri utekelezaji wa shughuli zilizo kasimiwa katika mwaka husika wa fedha.</p>
4	Fungu 28: Idara ya Jeshi la Polisi
	<ul style="list-style-type: none"> Kutokuonyesha kikamilifu kwa Mapato na matumizi mengineyo katika taarifa za mtiririko wa fedha Sh. 6,183,867,693.23 na 6,041,328,650.66 Taarifa ya mtiririko wa fedha kwa mwaka unaoishia tarehe 30 Juni 2012 inaonyesha uainishaji wa mapato na matumizi mengineyo yenye thamani ya Sh. 6,183,867,693.23na Sh.6,041,328,650.66. Lakini maelezo ya ziada yaliyoonyeshwa kwenye viambatisho 23 na 24 ya taarifa ya mtiririko wa fedha hayakuwa na taarifa ya kunyambulisha kiasi kilichoonyeshwa. Kutokuonyeshwa kwa malipo ya bidhaa (manunuzi ya vifaa) Sh. 1,335,030,964 Menejimenti haikuandaa mchanganuo wa manunuzi ya vifaa mbalimbali yenye thamani ya Sh. 1,335,030,964 kwa hiyo haikuweza kuthibitika usahihi wa kiasi kilicholipwa kwa manunuzi haya kwenye mapato na matumizi. <p>Mengineyo Madeni na Mihadi yasiyolipwa Sh. 97,402,969,043 na 97,116,080,473.63</p> <ul style="list-style-type: none"> Menejimenti ya Idara ya Polisi na Uokozi ilikuwa na malimbikizo ya madeni na mihadi yenye thamani ya Sh. 97,402,969,043 na 97,116,080,473.63 kwa ajili ya vifaa na huduma ambayo inapingana na kanuni ya bajeti kwa mfumo wa uandishi wa hesabu wa IPSAS kwa fedha taslimu.

5	Fungu 29: Idara ya Huduma za Magereza
	Malipoya shilingi 564,691,711 sawa na Dola za Kimarekani 348,100 yalilifanywa kwa mkandarasi M/S Giva Tanzania LTD ambayeana mkataba naldaraya Magerezakutoa huduma na matengenezo kwa mwaka wa fedha 2011/2012. Malipo haya yalikuwa ni dola 348,100 sawa nashilingi 564,691,711 ikiwa ni pamoja na ushuru (VAT). Mkandarasi huyo alilipwa asilimia 100 ndani ya miezisitakablayamkataba wake kumalizika.
6	Fungu 32: Ofisi ya Raisi Menejimenti ya Utumishi Wa Umma
	Ofisi ya Raisi Menejimenti ya Utumishi wa Umma imeshindwa kujibu hoja za miaka ya nyuma zenyenye thamani ya Sh.332,143,247. Hali hii inaweza kusababishamasuala yanayofananana haya kujirudiakatikamiaka inayofuata.
7	Fungu 37: Ofisi ya Waziri Mkuu
	<p>i. Bakaa ya fedha ambayo haikuwa sahihi Ofisi ya Waziri Mkuu ilihamisha kiasi cha Sh.913,150,141 na Sh.2,482,366,765 sawia, kwenda Ofisi ya Waziri Mkuu Dodoma na Mpiga Chapa Mkuu wa Serikali kwa ajili ya matumizi ya kawaida ya ofisi. Hadi kufikia mwisho wa mwaka taarifa za fedha zilionyesha kutokuwepo bakaa yoyote ya fedha wakati Ofisi ya Waziri Mkuu Dodoma ilionyesha bakaa ya Sh.660,280,908 na Mpiga Chapa Mkuu wa Serikali ilionyesha bakaa ya Sh.844,698,285.</p> <p>ii. Gharama ya ziada kwa mkataba wa manunuza Sh. 11,802,182 Wakati wa ukaguzi wa 2011/12 Ofisi ya Waziri Mkuu ililipa jumla ya Sh. 11,802,182 kwa timu ya watu waliosafiri kwenda China kufuutilia kazi ya uchapishaji wa vitabu vya kumbukumbu ya miaka 50 ya uhuru. Hata hivyo mkataba uliosainiwa kati ya Ofisi na M/s Guangzhou Quiancai ya China, mzabuni alitakiwa kulipia mzigo na gharama za mzigo hadi kupakiwa tayari kwa kusafirishwa. Gharama zaidi za kuwatuma maafisa wa serikali kwenda China kwa</p>

	<p>usimamizi wa utekelezaji wa mkataba kiasi cha Sh. 11,802,182 hazikustahili.</p> <p>iii. Malipo yenyeye nyaraka pungufu Sh. 42,474,500 na manunuzi yaliyofanyika bila kufuata taratibu za kiahasibu Sh. 30,713,151 Wakati wa ukaguzi llibainika kuwa Ofisi ya Waziri Mkuu ililipa Sh. 42,474,500 bila kuwa na nyaraka kamilifu.</p> <p>iv. Madeni yasiyolipwa Hesabu za mwisho wa mwaka zilionyesha kuwa kulikuwa na madeni yasiyolipwa yanayofikia kiasi cha Sh.1,489,362,941.</p>
8	Fungu 38: Jeshi la Ulinzi la Wananchi wa Tanzania

- Uhamishaji wa fedha kwenda kwa waambata wa majeshi nchi za nje Sh.404,620,666 bila kuwa na nyaraka kamilifu kiasi cha sh 404,620,666 kilipelekwa katika ofisi za waambata wa kijeshi walioko nje ya nchi kwa ajili ya matumizi ya kawaida.
Kinyume na kanuni za fedha No.95 (4) ya mwaka 2004, malipo hayo hayakuwa na viambatisho vya kuonyesha matumizi halisi ya fedha hizo.
- **Malipo ya mishahara kwa watumishi walio acha kazi Shs.20,648,800**
Ukaguzi wa majalada ya watumishi na kumbukumbu nyingine za mishahara ya watumishi wa umma jeshini ulifanyika katika mwaka wa fedha husika ili kuangalia udhibiti wa mishahara katika JWTZ.
- Ukaguzi umebaini kuwa, wafanyakazi wanane ambao walikuwa wameachishwa kazi kati ya mwezi Septemba, 2011 na Aprili, 2012 walikuwa bado wanalipwa mishahara kinyume cha sheria. Hadi kufikia Juni 2012 jumla ya Sh 20,648,800 zilikuwa zimelipwa kwa watu hao.

9	Fungu 39: Jeshi la Kujenga Taifa
	<ul style="list-style-type: none"> Mapitio ya taarifa za fedha za Fungu 39 - Jeshi la Kujenga Taifa yalibaini maduhuli mengineyo ya kiasi cha Sh.17,083,568,860 yanayojumuisha kiasi cha Sh.12,475,547,000 ambazo ni madeni yasiyolipwa yaliyohamishwa na Hazina kutoka matumizi ya kawaida kwenda hesabu ya Amana na hivyo kusababisha tofauti ya kiasi cha Sh.4,608,021,860 ambacho ni kikubwa kinacholeta athari katika taarifa za fedha. Malipo ya Sh.58,357,500 yalifanywa bila kuwa na nyaraka kamilifu hivyo ukaguzi kushindwa kuthibitisha uhalali wa malipo hayo.
10	Fungu 40 - Idara ya Mahakama
	<p>Masurufu yasiyorejeshwa Sh.58,037,898 Masurufu ya kiasi cha Sh. 58,037,898 yalikuwa hayajarejeshwa hadi kufikia mwisho wa mwaka wa fedha. Aidha hakuna hatua yoyote iliyochukuliwa na Afisa Masuuli ikiwepo tozo la asilimia kumi (10%) kutoka katika mishahara ya wahusika.</p>
11	Fungu 41: Wizara ya Katiba na Sheria
	<p>Mali zenyе thamani ya Sh.98,893,958 hazikuandikwa nambari za utambulisho wala kuandikwa katika daftari la mali.</p>
12	Fungu 42: Ofisi ya Bunge
	<p>Matumizi katika ununuzi wa rasilimali za thamani ya Shs.132,511,915 yalitolewa taarifa kama matumizi ya kawaida kinyume na Kanuni No.95 (2) ya Kanuni za Fedha za Umma ya mwaka 2001 (iliyorekebishwa 2004) pia hati za malipo zenyе thamani ya Sh.17,145,000 hazikupatikana kwa ajili ya ukaguzi.</p>

13	Fungu 46: Wizara ya Elimu na Mafunzo ya Ufund <ul style="list-style-type: none"> • Madeni yasiyolipwa Sh.11,061,371,927 Taarifa ya madeni ilionyesha madeni yasiyolipwa ya kiasi cha Sh. 11,061,371,927 hadi kufikia tarehe 30 Juni, 2012. • Taarifa ya upotevu wa mali za Umma Sh.85,948,293 Mapitio ya taarifa za fedha yalibaini kuwa Wizara ilionyesha upotevu wa mali zenyenye thamani ya cha Sh.85,948,293. • Malipo zaidi ya mishahara na mafao ya wastaifu Sh.33,872,421 Mapitio ya majalada ya watumishi na orodha za mishahara yalifanywa ili kubaini udhibiti wa ndani katika eneo la mishahara. Hata hivyo mapungufu yafuatayo yalibainika: - Watumishi wanne waliokuwa wamestaifu tangu mwezi Februari na Septemba 2012 waliendelea kulipwa mishahara ya kila mwezi inayofikia Sh.5,811,251. Aidha, ilibainika kuwa mtumishi mmoja aliyekuwa chini ya Kurugenzi ya ukaguzi wa shule alipandishwa cheo kutoka TGTS E kwenda TGTS F. Hata hivyo tangu mwaka 2008 mtumishi huyo alilipwa mshahara wa TGTS H kwa mwezi badala ya TGTS F bila kuwepo barua ya kupandishwa cheo na hivyo kusababisha malipo zaidi ya kiasi cha Sh.27,520,770. • Tozo kwa kuchelewesha kuwasilisha makato katika mfuko wa Pensheni (PSPF) Sh.180,748,127 Ukaguzi wa hati za malipo na majalada ya watumishi katika mwaka husika ulibaini kuwa Wizara ililipa kiasi cha Sh.180,748,127 kwa PSPF ikiwa ni tozo kwa kuchelewesha kuwasilisha makato ya watumishi kwa kipindi cha Julai, 1999 hadi Mei, 2008.
----	---

14	Fungu 48: Wizara ya Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi
	<ul style="list-style-type: none"> • Taarifa ya Malimbikizo ya Mapato Sh 352,873,364.88 Katika mwaka wa fedha ulioishia Juni 30, 2012 uongozi wa Wizara ulitoa taarifa ya Fedha za malimikizo ya mapato ya Sh.352,873,364.88. Hata hivyo, majedwali na nyaraka zingine zilizoambatishwa hazikuonyesha malimbikizo ya kodi ya ardhi katika vituo vya mikoani. • Mapato yaliyokusanywa kutoka vituo vya mikoani lakini hayakuhamishiwa kwenye Akaunti ya Mapato ya marejesho Shs.59, 552,205 Imebainika kwamba jumla ya Sh.59,552,205.40 zilikusanywa kutoka vituo 18 vya mikoani, lakini mwisho wa mwaka yaan Juni 30, 2012 fedha hizo hazikuwa zimeingizwa kwenye akaunti kuu No.2011000025 ya mapato ya Wizara. • Viwanja 7,342 vyenye shaka ambavyo vilitengwa na kukaa kwenye mfumo wa hazina ya viwanja. Ukaguzi wa mfumo wa hazina ya viwanja wa wizara uliofanywa ili kufuutilia ugawaji wa viwanja na ukusanyaji kodi, ulibaini kwamba viwanja 7,342 vilifanyiwa utafiti. Hata hivyo wamiliki wa viwanja hivyo hawajatayarishiwa ankara zao ili waweze kulipa kodi ya ardhi. • Ukosefu wa Kumbukumbu kwa Mgao wa Viwanja 160 kinyume na sehemu No.I ibara ya 10 ya Kanuni za Ardhi za mwaka 2001 Ukaguzi wa Mradi wa Viwanja 20,000 umebaini kuwa viwanja 160 vyenye thamani ya Shs.555, 820,891 kama inavyoonekana katika mfumo wa hazina ya viwanja Wizarani, unaonyesha kwamba viwanja hivyo viligawiwa kwa waombaji waliofanikiwa kupata katika jiji la Dar es salaam katika kipindi cha mwaka husika.

	<p>Hata hivyo, maandishi yanayoonyesha mauzo ya viwanja hivyo hakuletwa kwa ajili ya ukaguzi</p> <ul style="list-style-type: none"> Wadaiwa wasiolipa mauzo ya viwanja vyenye thamani ya Sh. 424,343,715.00 Wizara ya Ardhi Nyumba na Maendeleo ya Makazi iliuza viwanja 210 vyenye thamani ya Sh. 633,984,493 vilivyotengwa kwa waombaji mbalimbali katika Jiji la Dar es Salaam kutoka kipindi cha mwaka 2005 hadi 2011. Ukaguzi wa kumbukumbu za uhasibu na nyaraka nyingine unaonyesha kwamba kufikia mwisho wa mwaka ni kiasi cha shs.209 640,778.00 tu kilikuwa kimekusanywa, na kuacha bakaa ya Sh.424,343,715.00 bila kukusanywa. Ukiukwaji wa sheria ya mipango miji kuhusu ujenzi kwenye fukwe za bahari Ukaguzi ulibaini kwamba jumla ya viwanja 46 vilivyokuwa ndani ya eneo la mita 60 kutoka ufukweni mwa bahari viliendelezwa kinyume na Kifungu cha 13 cha Sheria ya Mipango Miji (Public Beaches Planning Area Law, CAP378)
	<ul style="list-style-type: none"> Taarifa ya Malimbikizo ya Mapato Sh 352,873,364.88 Katika mwaka wa fedha ulioishia Juni 30, 2012 uongozi wa Wizara ulitoa taarifa ya Fedha za malimbikizo ya mapato ya Sh.352,873,364.88. Hata hivyo, majedwali na nyaraka zingine zilizoambatanishwa hazikuonyesha malimbikizo ya kodi ya ardhi katika vituo vya mikoani. Mapato yaliyokusanywa kutoka vituo vya mikoani lakini hayakuhamishiwa kwenye Akaunti ya Mapato ya marejesho Shs.59, 552,205 Imebainika kwamba jumla ya Sh.59,552,205.40 zilikusanywa kutoka vituo 18 vya mikoani.Lakini mwisho wa mwaka, Juni 30, 2012 fedha hizo hazikuingizwa kwenye akaunti kuu No.2011000025 ya mapato ya Wizara.

15	Fungu 51: Wizara ya Mambo ya Ndani
	<ul style="list-style-type: none"> • Malipo yasiyo na nyaraka kamili kiasi cha Sh. 7,215,500 Malipo ya kiasi cha Sh.7,215,500 yalifanyika bila ya kuwa na nyaraka kamili, hivyo hatukuweza kujiridhisha kama yalikuwa ni malipo halali. • Mishahara iliyolipwa kwa watumishi wasiokuwepo Sh. 9,115,000 Jumla ya Sh.9,115,000 zililipwa kwa watumishi ambao wamestaafu, kufukuzwa au kuacha kazi. <p style="text-align: center;">Masuala mengineyo</p> <ul style="list-style-type: none"> • Madeni yasiyolipwa Sh. 1,051,021,168.77 Taarifa za fedha za Wizara zinaonyesha kuwepo madeni ya jumla ya Sh. 1,051,021,168.77 hadi kufikia tarehe 30 Juni, 2012. Kuwepo kwa madeni haya ni kinyume na Mfumo kubalifu wa kiuhasibu wa IPSAS unaotambua mapato na matumizi kwa fedha taslimu na yanaweza kuathiri utekelezaji wa bajeti ya mwaka 2012/2013 kwani sehemu yake inaweza kutumika kulipia madeni ya nyuma. • Thamani ya majengo isiyoambatanishwa na jedwali kuthibitisha kuwepo kwake Sh. 999,999,614 Taarifa ya mtiririko wa fedha ilionyesha kuongezeka kwa raslimali za kudumu zenye thamani ya Sh. 1,020,968,614 ambazo kati yake ni majengo yenye thamani ya Sh. 999,999,614 ambayo yalikosa jedwali la kuthibitisha kuwepo kwake na mahali yalipo. • Kutosuluhishwa kwa tofauti kati ya Jedwali la ,majengo,mitambo na vifaa mbalimbali na Rejista ya mali za kudumu Sh. 1,954,575,708.40 Jedwali la majengo, mitambo na mali mbalimbali lilionyesha mali zenye thamani ya Shs. 17,053,703,291.60 wakati Rejista ya mali za kudumu ilionyesha mali zenye thamani ya Sh. 19,008,279,000 na hivyo kujitokeza tofauti ya Shs. 1,954,575,708.40 ambayo haikusuluhishwa

16	Fungu 52: Wizara ya Afya na Ustawi wa Jamii
	<ul style="list-style-type: none"> • Tozo kwa ucheleweshaji wakuwasilisha makato ya kisheria Sh.881,350,025 Katika mwaka wa fedha 2011/2012 uongozi wa wizara ulilipa jumla ya Sh.881,350,025kamaadhabukutokana na kuchelewa kuwasilishamichangokisheria kwa shirika la Mfuko wa Hifadhi ya Jamii (PSPF). Hata hivyo serikali haikupata faida kutokana na kiasikilicholipwakamaadhabukwa shirika hilo. • Mapokezi ya mali yasiyothibitishwa Sh.339,757,421 Kiasi cha Sh.339,757,421 kililipa kwa wazabuni kwa ajili ya kutoa huduma ya vifaa na mali. Hata hivyo hapakuwa na uthibitisho kama vifaa hivyo na mali hizo vilipokelewa Wizarani. • Malipoyenye nyaraka pungufu Sh.829,875,661 Wizara ililipa jumla ya Sh.829,875,661 kwa ajili ya huduma mbalimbali. Hata hivyo malipo haya yalikuwa na nyaraka pungufu. • Malipoyasiyokuwa na nyaraka Sh.94,670,544 Malipo ya kiasi cha Sh.94,670,544 yalifanywa bila nyaraka. • Malipoya matibabu nje ya nchi Sh.197,274,989 Wizara ilifanya malipo ya kiasi cha Sh. 197,274,989 kwenye ofisi zetu za balozi kwa ajili ya gharama za matibabu. Hata hivyo marejesho ya matumizi ya fedha hizo hayajafanyika. • Makatoya mishahara yasiyo naviambatanisho Sh.600,910,282 Katika mwaka huu wa ukaguzi Wizara ilifanya makato mbalimbali ya kisheria yenye kiasi cha Sh.600,910,282, ikiwa ni kodi na michango katika mifuko ya pensheni. Hata hivyo hakuna ushahidi wa kukiri mapokezi ya fedha hizo kutoka kwenye mfuko husika.

17	Fungu 53: Wizara ya Maendeleo ya Jamii ,Jinsia na Watoto
	Malimbikizoya madeniyash2,469,803,171.00
	<p>Wizara imetoa taarifa ya malimbikizo ya madeni ya kiasi cha Sh.2,469.803.171.00 hadi kufikia tarehe 30 Juni, 2012. Kuwepo kwa madeni haya ni kinyume na mfumo kubalifu wa Kiuhasibu wa IPSAS unaotambua mapato na matumizi kwa fedha taslimu na inaathiri umaana wa bajeti ya miaka inayofuata.Pia hii ni ishara kwamba mfumo wa IFMS-Epicor unaruhusukuundwa kwamadeni, haliambayohaipaswi kuwa hivyo.</p>
18	Fungu 55: Tume ya Haki za Binadamu na Utawala Bora
	<p>Mihadi na madeni Sh.244,844,018</p> <p>Katika mwaka wa fedha 2011/2012, taarifa ya fedha ya Tume ya Haki za Binadamu na Utawala Bora ilionyesha Mihadi na malimbikizo ya Madeni ya kiasi cha Sh. 244,844,018, hivyo basi, kuna hatari ya kutumia fedha kwa mwaka wa fedha 2012/2013 kulipia madeni ya miaka iliopita.</p> <p>Zaidi ya hayo, nikushindwa kwadhana yamfumowa serikali wa kufanya matumizi wakati inapesa ili kuondokana uendeshaji wa bajeti mbilisambamba.</p>
19	Fungu 56: Ofisi ya Waziri Mkuu Tawala za Mkoa na Serikali za Mitaa
	<ul style="list-style-type: none"> • Manunuzi bila ushindani wa zabuni ya Sh.53,721,998 Kinyume na kanuni Na.63 ya sheria ya manunuzi ya mwaka 2005 na makubaliano ya Wakala wa Manunuzi na Huduma wa Serikal (GPSA) Kumbukumbu Na..AE/005/HQ/DOM/G-07/008/2011/2012, Ofisi ya Waziri Mkuu Tawala za Mkoa na Serikali Mitaa ilifanya manunuzi ambayo yalifanywa kutoka chanzo moja. • Malipo ya ziada yaliyolipwa kwa ajili ya ununuzi ya gari aina ya (4WD Toyota Land Cruiser) Sh.56,520,305 Ukaguzi wa hati za malipo na nyaraka zingine zilizo ambatanishwa umebaini kwamba wizara ilifanya manunuzi ya

	<p>gari aina ya (4WD Toyota Land Cruiser) kutoka kwa M / S Toyota Tanzania Ltd.</p> <p>Malipo haya yalifanywa chini ya mpango wa dharura kupitia hati ya malipo Na.33/3, cheque Na.163,325 na Ankara kifani Na.PF/ COW / SD/12/174 ya tarehe 26/3/2012 yenye thamani ya Sh.1,036,634,019.</p> <p>Hata hivyo, ankara ya malipo inaonyesha jumla ya Sh 979,479,695.20 hivyo malipo ziada ya shilingi 56,520,305 hayakutolewa maelezo na uongozi.</p> <ul style="list-style-type: none"> • Magari ambayo hayafanyi kazi yenye thamani ya Sh. 196,757,891.88 Ukaguzi kuhusu utunzaji wa magari ulibaini kwamba magari tisa (9) yanayomilikiwa na Ofisi ya Waziri Mkuu TAMISEMI hayatumiki na kadri muda unavyokwenda thamani ya magari hayo inazidi kuporomoka na kuna uwezekano wa kuchomolewa vipuli. • Malimbikizo ya madeni ya jumla ya Sh. 1,579,086,048.92 Katika mwaka wa fedha wa ukaguzi Ofisi ya Waziri Mkuu TAMISEMI ilitoa taarifa ya malimbikizo ya madeni yasiyolipwa yenye thamani ya Sh.1,579,086,048.92 <p>Hata hivyo ukaguzi umebaini kwamba kiasi hicho cha fedha hakikuwa kwenye bajeti ya mwaka husika wa fedha na kuingiza malimbikizo hayo ya madeni kwenye hesabu ni kinyume na matakwa ya viwango vya kimataifa vya uandishi vitabu vya sekta ya Umma (IPSAS)</p> <p>Hii ina maana kwamba, fedha zilizotengwa kwa ajili ya mwaka wa fedha 2012/2013 zitatumika kulipia madeni ya mwaka 2011/2012. Wakati huo huo shughuli zilizoidhinishwa kwa mwaka husika zitakuwa zimetekelezwa nusu.</p>
20	Fungu 57: Wizara ya Ulinzi na Jeshi la Kujenga Taifa
	<ul style="list-style-type: none"> • Magariyalionunuliwa lakini hayajapokelewa Uongozi wa wizara ulimlipa mzabuni M/SSimbaMotorsLtdkiasi cha Sh.1,241,000,000 kwa hundiNa.971255yaDisemba 15, 2011

	<p>ikiwa ni gharama za bima na utawala kusafirisha magari 723 yakiwa yamebebwaa katikamizigotofauti tofauti. Magari 299 yamethibitishwa kuwa yameletwa, bado magari 424 yanashubiriwa kuletwaa kama mkataba unavyoeleza.</p> <ul style="list-style-type: none"> • Gharamaza kukomboa magari bandarini zilizolipwa kwa Shirika la Mzinga hazikutolewa maelezo Sh.292,315,317 • Kiasi cha Sh.1,124,503,902 zililipwa Shirika la Mzinga kwa hundiNa.971293ya tarehe 29/06/2012 ili kukomboa magari bandarini yakitokea nchini India-Ashock LeylandLtd. • Hati za kupokelea mizigo yenyeye thamani ya Sh.832,188,585 zilihakikiwa nakukubaliwa bado bakaa ya Sh.292,315,317 haijathibitishwa.
21	Fungu 58:Wizara ya Nishati na Madini
	<ul style="list-style-type: none"> • Mapato ya mrahaba yasiyokusanywa: Dola za Kimarekani 12,634,354.61 sawa na Shs.19,709,593,191 Wakati wa ukaguzi ilibainika kuwa makampuni ya uchimbaji madini yalilipa mrahaba kwa kiwango cha asilimia 3% baada ya makato ikiwa ni kiwango cha sheria ya zamani ya madini badala ya asilimia 4% kabla ya makato kama inavyotakiwa na kipengele cha 87(1) I cha sheria ya madini ya mwaka 2010 na hiviyokusababisha kutokukusanywa kwa kiasi cha Sh.19,709,593,191. • Malimbikizo ya maduhuli ambayo hayakuonyeshwa Sh. 1,645,582,899 Taarifa za fedha zilizowasilishwa na Wizara hazikuonyesha malimbikizo ya maduhuli yenyeye jumla ya Sh. 1,645,582,899.
22	Fungu 61 - Tume ya Taifa ya Uchaguzi
	<p>Taarifaya Tume ilionyesha mali, mitambo na vifaa vyenye thamani ya Sh.6,335,939,501.75 wakati daftari la mali lilionyesha mali yenyeye thamani ya Sh.5,702,523,735.88 na hivyo kusababisha tofauti ya Sh.636,415,765.87. Matumizi ya Tume yanajumuisha kiasi cha Sh.862,787,000 kilichohamishwa kwenda kwa</p>

	Wakurugenzi watendaji wa Halmashauri kwa ajili ya kugharamia chaguzi ndogo. Malipo hayo hayakuwa na taarifa za matumizi kinyume na kanuni ya 86 (1), 87 na 95 (4) ya Kanuni za Fedha za Umma 2001 (iliyorekebishwa 2004)
23	Fungu 66:Ofisi ya Rais Tume ya Mipango Posho maalum ya kujikimu iliyolipwa bila kibali Sh. 340, 334,565.
24	Fungu 69: Wizara ya Maliasili na Utalii
	<ul style="list-style-type: none"> KampuniSaba zauwindajyaani M/S Malagarasi Hunting Safaris, Mwanahuta & Company Ltd, Usangu Safaris Ltd, Rana Tours & Safaris Ltd, Coastal Wilderness (T) Ltd, Kilimanjaro Game Trails Ltd na Said Kawawa Hunting Company Ltdwana malimbikizo ya madeni USD 973, 493. <p>Hadi natoa taarifa hii ya ukaguzi kampuni hizo bado zilikuwa zinaendeleakufanya kazi/shughuli za uwindaji.</p> <p>Wizara inatakiwa kuwa na utaratibu au mikakati madhubuti ya ufuatiliaji na ukusanyaji wa maduhuli ya serikali.</p> <p>Pia AfisaMasuulianatakiwakuchukua hatuaza kisheria nakinidhamu dhidi yakampuni zote zilizotajwa hapo juu.</p> <ul style="list-style-type: none"> Maduhuliya jumla yadola 216,000 yanayohusiana na leseni za uwindaji kufikia mwisho wa mwaka hayakukusanywa nakampuni za utalii zimeendelea kufanya biashara ya utalii bila leseni halali za kufanya biashara. Kifungu Na.116(2) (a) cha Sheria Na.5 ya Uhifadhi wa Wanyamaporiya 2009 kinasema kuwa, faini itakuwasi chini yashilingi Elfu mia mbililakiniisiyozidi shilingimilioni kumi. Mara nyingifaini inayotozwa niya kiwango chachini yashilingi 200,000. Pamoja na kwamba iko ndani ya kiwango kilicho tajwa kisheria, ni dhahiri kwamba haiwezi kuondoa vitendo vya ujangili vinavyofanywa na wawindaji haramu wawanyama pori.

25	Fungu 81: Sekretarieti ya Mkoa wa Mwanza
	<ul style="list-style-type: none"> • Malipo yaliyofanyika bila viambatanisho Sh. 20,250,000 Hati za malipo za Sh.20,250,000 zilikosa viambatanisho vyakutolewa kwa ukaguzi licha ya kuombwa kwa ajili ya ukaguzi. Hii ni kinyume cha Kanuni ya 86(1) ya Kanuni za Sheria ya Fedha za Umma ya mwaka 2001 (iliyorekebishwa 2004). • Hati za malipo ambazo hazikutolewa kwa ukaguzi Sh. 5,432,000 Hati za malipo pamoja na viambatanisho vyake zenye jumla ya Sh.5,432,000 hazikutolewa kwa ukaguzi licha ya kuombwa kwa ajili ya ukaguzi. Hii ni kinyume cha Kanuni ya 86(1) ya Kanuni za Sheria ya Fedha za Umma ya mwaka 2001 (iliyorekebishwa 2004). • Malipo ambayo hayakustahili kulipwa Shs 27,680,000 Ukaguzi wa nyaraka za malipo uliofanyika katika ofisi ya Mganga Mkuu wa Mkoa uligundua kuwepo kwa malipo ya Sh.27,680,000 yaliyofanywa kwa ajili ya vibarua kinyume cha waraka Na.2 wa 2007 uliotolewa na Wizara ya Afya na Ustawi wa Jamii ulioagiza fedha za kuchangia huduma ya matibabu kutumika kwa ununuzi wa madawa, vifaa vya hospitali na gharama ndogondogo za ukarabati. Hali hii inadhihirisha kuwepo kwa matumizi kwa shughuli ambazo haziko katika makadirio ya matumizi yaliyoidhinishwa. • Mali za kudumu hazikuwa na kielelezo cha utambulisho Sh. 126,370,000 Mali za kudumu zilizonunuliwa katika mwaka huu wa fedha zenye jumla ya Sh.126,370,000 hazikuwa na kielelezo cha utambulisho jambo linaloweza kusababisha upotevu wa mali hizi. • Ucheleweshaji wa kupeleka fedha benki Sh.67,559,524 Fedha jumla ya Sh.67,559,524 zilizopokelewa na Sekretarieti ya mkoa kutoka vyanzo mbalimbali zilicheleweshwa kupelekwa

	benki kwa siku kati ya 2 hadi 79 Kinyume cha Kanuni ya 78(1) ya Kanuni za Sheria ya Fedha ya Umma ya mwaka 2001 (iliyorekebishwa 2004).
26	Fungu 85: Sekretarieti ya Mkoa wa Tabora
	<ul style="list-style-type: none"> • Malipo yanye nyaraka pungufu Sh.81,199,950 Secretarieti ilifanya malipo ya Sh.81,199,950 ambayo yalikuwa na nyaraka pungufu. • Masurufu yaliyolipwa kutoka katika vifungu vya matumizi Sh.26,406,400. Masurufu ya Sh.26,406,400 yalilipwa moja kwa moja kutoka katika vifungu vya matumizi na Sekretarieti kinyume na kanuni ya 98 (2) ya Kanuni ya Fedha za Umma ya mwaka 2001. • Malipo ya Sh.3,000,000 yalilipwa kwa njia ya masurufu lakini yakaonyeshwa moja kwa moja katika vifungu vya matumizi.
27	Fungu 91: Tume ya Udhibiti wa Madawa
	<ul style="list-style-type: none"> • Manunuzi bila kufuata taratibu za manunuzi Sh.209,686,039.55 Tume ya udhibiti wa madawa ililipa jumla ya Sh. 209,686,039.55 kwa watoa huduma mbalimbali bila kufuata taratibu za manunuzi. • Masurufu yasiyorejeshwa Sh.6,415,800 Masurufu ya jumla ya Sh.6,415,800 hayakuwa yamerejeshwa hadi tarehe 30 June,2012 na mpaka mwezi Februari, 2013 bado yalikuwa hayajarejeshwa ikiwa ni kinyume cha Kanuni 103 (1) ya Sheria ya Fedha za Umma Na.6 ya mwaka 2001(iliyorekebishwa 2004).
28	Fungu 96: Wizara ya Habari Utamaduni na Michezo
	Wizara inamalimbikizo yamadeniShs.965,652,404 yaliyotokana nawauza bidhaa, huduma,namadaiya wafanyakazi.

29	Fungu 99: Wizara ya Mifugo na maendeleo ya Uvuvi
	<ul style="list-style-type: none"> ▪ Kifaa ambacho hakikupokelewa Sh.29,953,000 Kituo cha utafiti wa mifugo (LRC)- Tanga kilitumia kiasi cha Sh.29,953,000 kwaajili ya kununua “Autokjedah Analyzer - Model: JK-KA-60” kwa matumizi ya utafiti kutoka VJB General Supplies, Dar Es Salaam. Hata hivyo, hadi tarehe ya ukaguzi (25/01/ 2013) kifaa hiki kilikuwa hakijapokelewa ▪ Kutokuwepo kwa mzani wa kupimia Ng’ombe wenyе thamani ya Sh.5,500,000 Mzani wa kupimia Ng’ombe wenyе thamani ya Sh.5,500,000 ambaо ungekuwa na uwezo wa kupima hadi kilo 1000 katika kituo cha utafiti wa mifugo (LRC)-Tanga haukuwepo licha ya kuwepo kwa kumbukumbu za manunuzi ya mzani huo. ▪ Kutokufanya kazi kwa chumba cha baridi (cold room) Sh. 15,114,000 Kituo cha utafiti(LRC) -Tanga kilijenga na kununua vifaa vya chumba cha baridi kwa gharama ya Sh.15,114,000, lakini chumba hiki hakikutumika kama ilivyobainika wakati wa ziara katika kituo hiki iliyofanyika tarehe 25 Januari, 2013.
30	Ubalozi wa Tanzania - Abuja
	<ul style="list-style-type: none"> • Ubalozi ulitumia fedha kiasi cha Sh.56,808,969 zikiwa ni makusanyo ya ada za viza. Fedha hizo zilikuwa ni zaidi ya zile zilizokuwa zimeabajetiwa na zilitumikabila ridhaa yaKatibu Mkuu wa Wizara ya Mambo ya Nje na Ushirikiano wa Kimataifa au Hazina. • Kiasi cha Sh.58,428,572.00 kilipokelewa ubalozinikutoka Wizarani ikiwa ni gharama ya kuwarudisha nyumbani watanzania ambaо walitoroka na kuingia nchini humo bila vibali maalaum. • Fedha halisi zilizokuwa zimetumika katika shughuli hiyo ni Sh.32,209,572 na bakaa ya Sh.26,219,000ilitakiwa kurudishwa

	Wizarani. Hata hivyo, hadi naandika taarifa hii kiasi hicho cha fedha kilikuwa bado hakijarejeshwa Wizarani.
31	<p>Ubalozi wa Tanzania - Bujumbura</p> <ul style="list-style-type: none"> • Malimbikizo ya Madeni Sh.130,666,076 Mwishoni mwa mwakajuni 30, 2012, ubalozi ulikuwa na malimbikizo ya madeni yenye jumla ya Sh.130,666,076 ambayo yalihusu wafanyakazina wazabuni. Madeniya jumla yashilingi 78,884,257 yanahusiana namwaka wa fedha 2010/11 na kiasi cha Sh.51,781,819 kinahusiana namwaka wa fedha 2011/12. Hii inaweza kuathiriuaminifuna ukarimuwa ubalozi kwa wateja wake. • Ukosefu wafedhakwaajili yakuimarishadiplomasia na kukuza uchumi kwa kutangaza vivutio vya Utalii. Miongoni mwamajukumu ya ubalozinikuimarishadiplomasianakutangaza vivutio mbalimbali vyautalii ambavyo vipo katika nchi ya Tanzania. Katika mwaka wa fedha 2010/11 na 2011/12, hakuna fedhazilizotengwahasakwa ajili ya kuimarishadiplomasiana kukuza uchumi kwakutangaza vivutio vyautalii.
32	<p>Ubalozi wa Tanzania - Cairo</p>
	Matumizi zaidi ya bajeti iliyoidhinishwa Sh.96,094,195 Wakati wa ukaguzi imebainika kwamba, Ubalozi ulilipa Sh.96,094,195 kwa ajili yamanunuzimbalimbalinamishahara ya watumishi. Hata hivyo, matumizi hayohayakuwa katikabajeti iliyoidhinishwa walampango kaziwa manunuzi wa mwaka.
33	<p>Ubalozi wa Tanzania - Kampala</p> <ul style="list-style-type: none"> • Hasara itokanayo na kubadilisha fedha za kigeni isiyokuwa na viambatanisho Sh.24,598,822 Ukaguziwatarifa za fedha umebaini kwamba mwisho wa mwaka Juni 30, 2012 ubalozi wa Kampala ulitoa taarifa yahasaraya Sh.24,598,822 itokanayo na kubadilisha fedha za

	<p>kigeni, Hata hivyo mchanganuo na viambatanisho vyake havikutolewa kwa ajili ya uhakiki.</p> <ul style="list-style-type: none"> Bakaa ya Sh.28,047,843 ya mfuko wa amana haijatumika muda mrefu. Ukaguziwa taarifa za fedha kuishia Juni 30, 2012 umegundua kwamba kiasi cha Sh.28,047,843 kilikuwa kwenye mfuko wa amana na kilikuwa hakijatumika kwa muda wa mwaka mzymawa fedha 2011/2012.
34	Ubalozi wa Tanzania - Kigali
	<p>Malimbikizo ya madeni Sh. 123,225,677 Ukaguzi wa taarifa za fedha za mwisho wa mwaka Juni 30, 2012 inaonyeshakuwa ubalozi ulikuwa na malimbikizo ya madeni ya Shs.123,225,677 ambayo yalikuwa yanahusiana na kodi ya nyumba, wazabuni, wastaa fu na mishahara ya wafanyakazi. Kuwepo kwa malimbikizo ya madeni mwisho wa mwaka ni kinyume na matakwa ya mfumo wa bajeti unaozingatia malipo kwa fedha taslimu.</p>
35	Ubalozi wa Tanzania - Kinshasa
	<p>Ubalozi ulihamisha Dola za Kimarekani 1,000 ambazo ni sawana Sh.1,575,690 za Tanzania, kutoka kwenye mfuko wa mapato yatokanayo na viza. Uhamisho huo hauku fuata taratibu kwasababu haukupata kibali kutoka kwa Katibu Mkuu wa Wizara za Fedha.</p>
36	Ubalozi wa Tanzania - Brussels
	<ul style="list-style-type: none"> Matumizi zaidi ya Sh. 150,805,390 Katika mwaka wa fedha 2011/2012 Ubalozi wa Brussels ulipokea jumla ya Sh.1,799,963,305 lakini ukatumia Sh. 1,950,768,695 na hivyo kufunga hesabu zake za mwaka ukiwa na matumizi zaidi ya Sh. 150,805,390. Kiasi hiki cha fedha

	<p>zaidi hakikuwa na kibali kutoka kwa Mlipaji Mkuu wa Serikali.</p> <ul style="list-style-type: none"> Deni kwa mwaka wa fedha 2011/2012 Sh. 530,202,631.34 Hesabu za mwisho wa mwaka unaoishia tarehe 30 Juni, 2012 za Ubalozi wa Brussels zilionyesha deni la Sh. 530,202,631.34 ambalo linatokana na huduma mbalimbali zilizotolewa katika Ubalozi huo. Deni hili ni kubwa na hivyo litasababisha sehemu kubwa ya bajeti ya mwaka 2012/2013 itumike kulipa deni hilo.
37	Ubalozi wa Umoja wa Mataifa - Geneva
	<p>Shughuli iliyogharimiwa wakati haikuwa katika bajeti Sh. 200,350,359 Ubalozi wa Geneva kwa mwaka wa fedha tunaoukagua uligharamia shughuli iliyotumia Sh. 200,350,359 ambayo haikuwa katika bajeti.</p>
38	Ubalozi wa Tanzania - London
	<p>Matumizi zaidi Sh.276,863,395 Hesabu za mwisho wa mwaka za Ubalozi wa London hadi kufikia tarehe 30, Juni, 2012 zilikuwa na matumizi zaidi ya Sh.276,863,395 dhidi ya makisio ya Sh.3,105,274,260 ukilinganisha na matumizi ya Sh. 3,382,137,655.</p>
39	Ubalozi wa Tanzania - Rome
	<ul style="list-style-type: none"> Majengo ya Ubalozi hayana hati milikiSh.4, 410,049,413.28 Ubalozi unamiliki majengo mawili, moja linaitwa Nyerere na linatumika kama makazi ya Mheshimiwa Balozi lipo eneo la Largo Olgita 15 Isola 90C Strada D,00123 lenye thamani ya Euro 1,200,000 sawa na Sh.2,370,024,000. Jengo lingine linatumika kama ofisi ya Ubalozi lililopo eneo la Viale Cortina d' Ampezzo 185,00135 lenye thamani ya Euro 1,032,913.80 sawa na Sh.2,040,025,413.28 majengo haya yalijengwa mwaka 1982 na 1984 lakini hadi sasa mwaka 2013 hayana hati miliki.

	<ul style="list-style-type: none"> Deni la Ubalozi hadi kufikia tarehe 30 Juni, 2012 Sh.764, 269,954.11 Hesabu za mwisho wa mwaka unaoishia tarehe 30 Juni, 2012 za Ubalozi wa Roma zilionyesha deni la Sh. 764,269,954.11 ambalo linatokana na huduma mbalimbali zilizotolewa katika Ubalozi huo. Deni hili ni kubwa na hivyo, litasababisha sehemu kubwa ya bajeti ya mwaka 2012/2013 itumike kulipa deni hilo.
40	Ubalozi wa Tanzania -Stockholm
	<ul style="list-style-type: none"> Matumizi zaidi dhidi ya makisio kwenye Akaunti ya Makusanyo Sh.139,953,446 Ubalozi ulitumia zaidi Sh. 139,953,446 kutoka kwenye akaunti ya makusanyo dhidi ya makisio yaliyoidhinishwa bila kupata idhini ya Katibu Mkuu Hazina. Deni la Ubalozi hadi tarehe 30 Juni, 2012 Sh. 770,352,370 Hesabu za mwisho wa mwaka unaoishia tarehe 30 Juni, 2012 za Ubalozi wa Stockholm zilionyesha deni la Sh. 764,269,954.11 ambalo linatokana na huduma mbalimbali zilizotolewa katika Ubalozi huo. Deni hili ni kubwa na hivyo, litasababisha sehemu kubwa ya bajeti ya mwaka 2012/2013 itumike kulipa deni hilo.
41	Ubalozi wa Tanzania -Pretoria
	Fedha ya Makusanyo haikuidhinishwa kuhamishwa Ubalozi uliruhusiwa na Katibu Mkuu, Wizara ya Mambo ya Nje na Ushirkiano wa Kimataifa kuhamisha kiasi cha ‘SAR’ 3,780,000 tu kutoka katika kiasi kilichobakishwa ‘retained’ cha ‘SAR 5,250,000’ na hivyo kiasi kilichobaki cha ‘SAR’ 1,470,000 hakikuruhusiwa kuhamishwa.
42	Ubalozi wa Tanzania - Berlin
	<ul style="list-style-type: none"> Umiliki wenye mashaka wa Jengo la Ubalozi Sh.2,449,037,200 Ubalozi wa Tanzania Berlin unamiliki jingo lenye thamani ya

	<p>Sh. 2,499,037,200 lililonunuliwa Disemba, 2002 ambalo lipo eneo la 11 Eschenallee, 14050 Berlin. Hata hivyo, jengo hilo halikua na hati miliki.</p> <ul style="list-style-type: none"> Madeni ya muda mrefu Sh. 391,953,136.88 Hesabu za mwisho wa mwaka zinazoishia tarehe 30 Juni, 2012 zinaonyesha madeni ya Sh. 391,953,136.88 ya muda mrefu ambayo hayajalipwa.
43	Ubalozi wa Tanzania - Tokyo
	<p>Matumizi zaidi ya bajeti Sh. 950,283,999.85 Kanuni ya 46 (3) ya Kanuni ya Fedha za Serikali Kuu inamtaka Afisa Masuuli kuomba kibali cha kutumia zaidi kuliko bajeti kabla kufanya matumizi. Kinyume na kanuni tajwa hapo ubalozi ultumia zaidi Sh. 950,283,999.85 bila idhini yoyote.</p>
44	Ubalozi wa Tanzania -New Delhi
	<p>Matumizi yasiyoidhinishwa katika bajeti Sh.180,647,729.56 Ubalozi ultumia kiasi cha Sh. 180,647,729.56 ambazo hazikuwa zimeidhinishwa katika bajeti kwa mwaka huu tunaoukagua.</p>
45	Ubalozi wa Tanzania -Kuala Lumpur
	<p>Matumizi yasiyoidhinishwa katika bajeti Sh.183,964,223.51 Ubalozi ultumia kiasi cha Sh. 183,964,223.51 ambazo hazikuwa zimeidhinishwa katika bajeti kwa mwaka huu tunaoukagua.</p>
46	Ubalozi wa Tanzania -Beijing
	<ul style="list-style-type: none"> Matumizi zaidi yasiyoidhinishwa katika bajeti Sh. 131,747,908 Hesabu za Ubalozi zinaonyesha kuwa zilitumika fedha zaidi Sh. 131,747,908 ambazo hazikuwa zimeidhinishwa katika bajeti kwa mwaka huu tunaoukagua.

	<ul style="list-style-type: none"> Deni la Ubalozi hadi tarehe 30 Juni, 2012 Sh. 352,734,824 Hesabu za mwisho wa mwaka unaoishia tarehe 30 Juni, 2012 za Ubalozi wa Beijing zilionyesha deni la Sh. 352,734,824 ambalo linatokana na huduma mbalimbali zilizotolewa katika Ubalozi huo. Deni hili ni kubwa na hivyo, litasababisha sehemu kubwa ya bajeti ya mwaka 2012/2013 itumike kulipa deni hilo Matumizi zaidi yasiyoidhinishwa katika bajeti Sh.234,916,555 Hesabu za Ubalozi zinaonyesha kuwa zilitumika fedha zaidi Sh. 234,916,555ambazo hazikuwa zimeidhinishwa katika bajeti kwa mwaka huu tunaoukagua.
47	Ubalozi wa Tanzania -Harare
	<p>Miadi na madeni kwa mwaka unaoishia tarehe 30 Juni, 2012 Sh. 78,837,727.40 Hesabu za ubalozi zilifungwa zikiwa na deni pamoja na miadi ya Shs.78,837,727.40 tarehe 30 Juni, 2012. Hali hii si nzuri ya kubakiza fedha kwa ajili ya shughuli ambazo hazikukamilika kutekelezwa wakati mfumo wetu wa malipo ni kutumia taslimu kulingana na kiasi kilichopo. Kubakiza fedha kunaonyesha mwaka wa fedha unaofuata kutakuwa na mifumo miwili ya malipo ambayo ni taslimu na mkopo.</p>
48	Ubalozi wa Tanzania Lusaka
	<p>a) Fedha ambazo hazikuonyeshwa kwenye taarifa za Hesabu Sh.1,762,638.10 Fedha jumla ya Sh.1,762,638.10 zilizopokelewa mwezi Julai, 2012 kama mshahara wa mwezi wa Juni, 2012 hazikuonyeshwa kwenye taarifa ya hesabu za Ubalozi zilizoishia tarehe 30 Juni,2012.</p> <p>b) Tofauti katika bakaa ya fedha ambayo haikutolewa maelezo Sh.18,488,320 Taarifa ya mapato na matumizi kwa mwaka wa fedha</p>

	<p>unaoishia tarehe 30 Juni, 2012 ilionyesha bakaa ya fedha mwisho wa mwaka ya Sh.29,413,172. Hata hivyo, fedha taslimu katika taarifa ya hesabu za Ubalozi ilionyeshwa kuwa Sh. 10,924,852 na hivyo kujitokeza fofauti ya Sh.18,488,320 ambayo haikutolewa maelezo.</p> <p>Mambo ya msisitizo:</p> <p>Matumizi ya ziada kwa kasma Sh. Sh.76,081,845 Katika kulinganisha makadirio ya matumizi yaliyoidhinishwa na matumizi halisi kwa kila kasma kwa mwaka wa fedha 2011/2012 ilionekana kuwepo matumizi zaidi ya Sh.76,081,845 kinyume na kanuni ya 46 ya Kanuni za Sheria ya Fedha ya mwaka 2001 (marekebisho ya 2004).</p>
49	Fungu 70: Sekretarieti ya Mkoa wa Arusha
	<ul style="list-style-type: none"> • Dawa zilizoisha muda wa matumiziSh.8,310,700 Dawa za hospitali zenyne thamani ya Sh.8,310,700 ambazo zimeisha muda wa matumizi na hazifai kwa ajili ya matumizi ya binadamu hazijaharibiwa. • Malipo yenyne nyaraka pungufuSh.9,350,021 Malipo ya jumla ya Sh.9,350,021 yalikuwa na nyaraka pungufu na hivyo kushindwa kuthibitisha uhalali wake kama Kanuni ya 95 (4) Fedha ya Serikali Kuu ya mwaka 2004 inavyoelekeza. • Fedha taslimu zilizolipwa kutoka akaunti ya maendeleo kutotumika11,135,000 Sekretariati ya Mkoa wa Arusha ililipa malipo toka akaunti ya maendeleo na kutoa benki taslimu ili kugharimia shughuli ya kimaendeleo lakini hadi Septemba, 2012 fedha hizo zilikuwa bado hazijatumika.
50	Fungu 71: Sekretarieti ya Mkoa wa Pwani
	<ul style="list-style-type: none"> • Makato ya pensheni katika watumishi waliostaafu katika Mfuko wa Pensheni wa watumishi wa Serikali Kuu Sh.

	<p>2,113,186 Makato ya Shs. 2,113,186 yalilipwa kwenye mfuko wa mafao ya watumishi wa Serikali Kuu kwa makosa.</p> <ul style="list-style-type: none"> • Mtumishi kulipwa mshahara wote wakati akiwa katika matazamio 11,014,200 Sekretarieti ilimpa mtumishi mshahara wote Sh. 11,014,200 wakati akiwa katika matazamio kinyume na masharti ya kazi yake.
51	Fungu 73: Sekretarieti ya Mkoa wa Iringa
	<ul style="list-style-type: none"> • Deni la Bima ya Afya kwa Hospitali ya mkoa wa Iringa Shs. 100,686,563 Hospitali ya mkoa wa Iringa inaidai Bima ya Afya kiasi cha Sh. 100,686,563 ambazo zinatokana na kutibu wagonjwa wa mfuko wa Bima ya Afya. • Madeniyalijolipwa hayakuwepo kwenye orodha ya wadai wa mwaka uliopita Sh. 20,659,937 Sekretarieti ya Mkoa ililipa jumla ya Sh. 20,659,937 kwa wadai ambao hawakuwepo katika orodha ya wadai wa mwaka uliopita. Hii ina athari kwenye bajeti ya mwaka husika.
52	Fungu 74: Sekretarieti ya Mkoa wa Kigoma
	<ul style="list-style-type: none"> • Udhaifu katika malipo ya masurufu Sh. 35,282,750 Mkoa ulilipa Sh. 35,282,750 kwa watumishi wake wawili pasipokuonyesha kuwa yalikuwa masurufu wakati kati yao mmoja alikuwa anadaiwa masurufu mengine kwa zaidi ya miezi saba Sh. 33,000,000. Hii ni kinyume na Kanuni ya 91 (2), 103 (1) and (2) ya Kanuni ya Fedha za Serikali Kuu ya mwaka 2004. • Fedha ya mishahara kutumika kwa matumizi ya shughuli za kawaida Sh. 15,945,000 Mkoa ultumia kiasi cha Sh. 15,945,000 kwa shughuli za

	<p>matumizi ya kawaida kinyume na taratibu za fedha.</p> <ul style="list-style-type: none"> Deni halikuthibitishwa Sh. 6,603,500 Mkoa katika hesabu zake ulionyesha deni la Sh.6,603,500 ambalo halikuwa na vielelezo kuthibitisha uhalali wake.
53	Fungu 75: Sekretarieti ya Mkoa wa Kilimanjaro
	<p>Malipo ya nyongeza ya mkataba hayakuidhinishwa na zabuni ya Sekretarieti ya mkoa Sh. 107,171,592 Malipo ya nyongeza ya mkataba ya Sh. 107,171,592 wa ujenzi wa Wodi ya akina mama wajawazito hayakuidhinishwa na zabuni ya Sekretarieti ya Mkoa wa Kilimanjaro. Ujenzi ulikuwa ukitekelezwa na kampuni iitwayo Elera Construction Co. Ltd.</p>
54	Fungu 76: Sekretarieti ya Mkoa wa Lindi
	<p>Dhamana kwa ajili ya utekelezaji wa miradi haikutolewa Sh. 98,087,533 Sekretarieti ya mkoa wa Lindi iliingia mikataba na kampuni mbalimbali kwa ajili ya utekelezaji wa miradi ambapo kisheria walitakiwa watoe dhamana ya benki kabla ya kuanza kazi. Utaratibu huu haukuftuwa na mkoa.</p>
55	Fungu 77: Sekretarieti ya Mkoa wa Mara
	<ul style="list-style-type: none"> Malipo ya tahadhari kwa ajili ya kesi zilizopo mahakamani Sh. 292,132,434 Mkoa una kesi katika mahakama na taratibu za kihasibu zinaelekeza kuonyesha katika taarifa za hesabu kiasi cha fedha unazoweza kutozwa kama fidia au faini iwapo mkoa utashindwa kesi hizo. Kuchelewa kukamilishwa kwa ukarabati wa nyumba ya makazi ya Mkuu wa wilaya ya Serengeti Sh. 17,447,020.80 Ukarabati wa nyumba ya makazi ya Mkuu wa wilaya ya Serengeti unaotekelizwa na kampuni ya PEK Brothers (T) Ltd kwa gharama ya Sh.116,313,742 umechelewa kukamilika Mkandarasi tayari amelipwa Sh.17,447,020 na ujenzi

	ulitarajiwa kukamilika Agosti 2012 lakini hadi Disemba, 2012 ulikuwa bado.
56	Fungu 79: Sekretarieti ya Mkoa wa Morogoro
	Deni inalodaiwa Sekretarieti ya mkoa Sh. 755,005,898 Hesabu za mwisho wa mwaka unaoishia tarehe 30 Juni, 2012 zilionyesha deni la Sh. 755,005,898 ambalo linatokana na huduma mbalimbali zilizotolewa katika Sekretarieti. Deni hili ni kubwa na hivyo, litasababisha sehemu kubwa ya bajeti ya mwaka 2012/2013 itumike kulipa deni hilo.
57	Fungu 80: Sekretarieti ya Mkoa wa Mtwara
	<ul style="list-style-type: none"> • Deni inalodaiwa Sekretarieti ya Mkoa Sh.182,309,061 Hesabu za mwisho wa mwaka unaoishia tarehe 30 Juni, 2012 zilionyesha deni la Sh.182,359,061 ambalo linatokana na huduma mbalimbali zilizotolewa katika Sekretarieti. Deni hili litasababisha sehemu kubwa ya bajeti ya mwaka 2012/2013 itumike kulipa deni hilo. • Utendaji dhaifu wa kampuni ya ‘Kadolo Contractor’ Sh. 203,091,511 Kampuni ya ‘Kadolo Contractors’ ilipewa kazi za zabuni na mkoa. Moja ilianza tarehe 20 Juni, 2011 na ilitakiwa kukamilika 30 Septemba, 2011 na nyingine ilianza tarehe 15 Septemba, 2010 na ilitakiwa ikamilike 15 Februari, 2011. Kazi zote hizi hadi tarehe 13 Oktoba, 2012 tulipotembelea eneo la miradi ilikuwa haijakamilika na mkoa haujachukua hatua yoyote ile.
58	Fungu 84: Sekretarieti ya Mkoa wa Singida
	<p>Mihadi na madeni yasiyolipwa Sekretarieti ya Mkoa ilikuwa na mihadi ya kiasi cha Sh.24,587,487.50 na madeni ya kiasi cha Sh.352,594,228.37 yaliyotokana na wazabuni wa mali na huduma pamoja na madai ya watumishi. Kuwepo kwa madeni haya na mihadi kuna kinzana na dhana ya bajeti inayozingatia malipo ya fedha taslimu.</p>

59	<p>Fungu 86: Sekretarieti ya Mkoa wa Tanga</p> <p>Ucheleweshaji wa ujenzi wa uzio wa nyumba ya Mkuu wa Wilaya Muheza Sh.87,330,030 Ujenzi wa uzio wa makazi ya Mkuu wa Wilaya ultakiwa kukamilika katika kipindi cha majuma 11 kuanzia tarehe 5 Aprili, 2012 hadi tarehe 4 Agosti, 2012. Hata hivyo ukaguzi umebaini kuwa ujenzi huo ulikuwa haujakamilika hadi ilipofika Novemba, 2012 pamoja na kwamba mkandarasi aliongezewa muda hadi tarehe 12 Septemba, 2012. Hakuna tozo iliyotolewa kwa ucheleweshwaji huo.</p> <ul style="list-style-type: none"> • Kutokuwa na mkakati wa kulipa madeni la Sh. 784,305,818 Mkoa hauna mkakati wa kulipa madeni kwani mwaka 2010/2011 madeni yalikuwa Sh.596,703,206 na kuongezeka Sh. 187,602,612 na hivyo madeni kufikia Sh.784,305,818. • Kuchelewa kupeleka fedha benki Sh.138,279,457 Fedha za makusanyo hospitali ya mkoa zimekuwa zikichelewa kupelekwa benki kinyume na Kanuni ya 60 ya Kanuni ya Fedha za Umma za mwaka 2001.
60	<p>Fungu 88: Sekretarieti ya Mkoa wa Dar Es Salaam</p> <p>Nyaraka zisizokamilika kwenye Mihadi isiyolipwa Sh. 200,000,000 Salio katika akaunti ya amana lililoonyeshwa tarehe 30 Juni 2012 linachanganya na Sh.200,000,000 zilizohamishwa kutoka fungu la Maendeleo ikiwa ni mihadi mbalimbali. Hata hivyo hakukuwa na taarifa ya mihadi isiyolipwa.</p>
61	<p>Fungu 89: Sekretarieti ya Mkoa wa Rukwa</p> <p>Miradi isiyokamilika Sh.218,591,493 Ukaguzi wa miradi mbalimbali ulibaini kwamba, miradi yenye thamani Sh.218,591,493 iliyotolewa kwa wakandarasi mbalimbali haijakamilika pamoja na kwamba kipindi cha mikataba kilikuwa</p>

	kimeshapita.
--	--------------

7.9 Wizara, Idara, Wakala na Tawala za Mikoa zilizopata Hati yenyé Shaka

Zifuatazo ni Wizara, Idara, Wakala na Tawala za Mikoa zilizopata Hati yenyé Shaka pamoja na sababu zilizofanya kupata hati hii.

1.	Hesabu Jumuifu za Taifa
	<ul style="list-style-type: none"> • Baadhi ya shughuli za Serikali hazikujumuishwa katika Hesabu Jumuifu za Taifa Katika kuitia taarifa za fedha kwa mwaka wa fedha ulioishia Juni 2012, iligundulika kuwa Taarifa za Hesabu Jumuifu za Taifa hazikujumuisha mapato, matumizi na fedha taslim za Serikali za mitaa kutokana na kutumia mifumo tofauti ya kiuhasibu ya utoaji taarifa. Aidha, hesabu za mashirika ya umma hazikujumuishwa katika Hesabu Jumuifu za Taifa kinyume na Aya 1.6.5 ya IPSAS • Kushindwakutoa maelezo ya ufanuzi kwa mujibu wa matakwa ya IPSAS IPSAS No. 1 Aya ya 1.4.9 inataka hesabu zionyeshe maoni na ufanuzi wa vitu vya muhimu ikiwa ni pamoja na fursa za mikopo zilizotolewa ambazo Serikali haijazitumia kwa ajili ya shughuli zake za baadaye za maendeleo pamoja na masharti yanayoambatana na fursa hizo. Hata hivyo matakwa hayo ya IPSAS hayakuzingatiwa. • Kushindwa kuandaa taarifa kulingana na mahitaji ya “IPSAS Cash basis” • IPSAS 1 aya ya 1.4.9 inahitaji kuonyesha kwenye taarifa ya fedha kiasi cha fedha za mkopo zilizopo ambazo zinaweza

	<p>kutumika baadae kulipia mahitaji ya mitaji. Hata hivyo, hitaji hili halikuzingatiwa.</p> <ul style="list-style-type: none"> IPSAS aya 1.6.16 inahitaji fedha taslim na miamala inayofanywa kwa fedha taslim kati ya taasisi chini ya chombo kimoja cha kiuchumi kuziondoa kabisa. Katika taarifa ya mapato na matumizi, kiasi cha Sh.4,828,689,668,358 kilionyeshwa kwenye taarifa kuwa miamala iliyofanywa kwa fedha taslimu.
2	Fungu 22: Deni la Taifa na huduma za ujumla
	<p>Kuonyeshwa pungufu kwa deni la Taifa Sh.2,874,190,267,938</p> <ul style="list-style-type: none"> Deni la PSPF kutojumuishwa katika deni la Taifa Sh.716.6 bilioni PSPF ilileta madai ya Sh.3.2 trilioni yakiwa ni madai ya malimbikizo ya makato ya mishahara ya wafanyakazi ambayo hayakulipwa na Serikali. Kati ya kiasi hicho kilichodaiwa Serikali ilikubali kwamba italipa kiasi cha Sh.716.6 bilioni kwa awamu. Hata hivyo Serikali haijaonyesha kiasi hiki cha Sh.716.6 bilioni kama ni sehemu ya deni la Taifa. Denila ATCL ambalo halikujumuishwa kwenye hesabu Sh.8.8 bilioni Deni la Kampuni ya Ndege Tanzania (ATCL) linalodaiwa na Shirika la Ndege la Afrika Kusini na Citi Bank lenye kiasi cha Sh.6.5 bilioni (USD 4,129,298.38) na Sh.2.3 bilioni (USD 1,460,000) zinazopelekea jumla ya pamoja ya Sh.8.8 bilioni ambazo Serikali kuitia Wizara ya Fedha (Fungu 50) ndiyo yenye jukumu la kulipa. Aidha deni hilo halikuonyeshwa kwenye deni la Taifa lilokuwepo tarehe 30 Juni, 2012. Mikopo iliyotolewa na Mifuko ya Pensheni kwa Taasisi za Umma Sh.1,250.013 bilioni. Dhamana ya Serikali kwa Taasisi za Umma kwa fedha zilizokopwa toka mifuko ya pensheni zinazotegemea bajeti ya Serikali pekee kama ilivyoainishwa kwenye rasimu ya

	<p>uchambuzi wa uhimilifu wa deni la Taifa ilifikia kiasi cha Sh.1,250,013,500,000. Walionufaika na mikopo hiyo ni Bunge, Chuo Kikuu cha Dodoma, PCCB, Jeshi la Polisi na Wizara ya Ulinzi, hata hivyo madeni hayo hayakuandikwa na kujumuishwa kwenye deni la Taifa.</p> <ul style="list-style-type: none"> • Deni la Saudi Arabia ambalo halikutolewa taarifa Sh.43,169,676 Serikali ya Tanzania inadaiwa na Serikali ya Saudi Arabia kiasi cha Sh.43,169,676. Uongozi ulikubali madai hayo na ukaahidi kulipa deni hilo kwenye mwaka wa fedha unaokuja baada ya kuhakiki taarifa za miaka ya nyuma. Deni lilifikia muda wa kulipwa bila kutengewa fedha na kuingizwa kwenye bajeti ya mwaka huu hali ambayo ilisababishwa na kutokuwapo na utunzaji mzuri wa nyaraka za madeni ya nje ili ulipwaji ufanyike mara muda wa kulipa unapowadia. • Dhamana ambazo Taasisi husika zimeshindwa kulipa Sh.53,994,267,965 Taarifa ya dhamana ilionyesha udhamini uliotolewa kwenye Mashirika ya Umma na Sekta binafsi kama SUKITA, HESLB, MCU nk. ambayo yako chini ya mfilisi au hayana uwezo wa kulipa madeni hayo; hali iliyopelekea madeni hayo kuwa ni ya Serikali lakini hayakuingizwa kwenye vitabu vya hesabu. Pia kiasi cha 1.6 bilioni kilidaiwa na mfilisi wa SUKITA kama fidia kwa Serikali kuchelewa kulipia mbolea iliyotolewa mwaka 1992. Hatukubaini uhalali wa madai hayo kwani SUKITA inadaiwa na Serikali kiasi kinachozidi Sh.10 bilioni. • Kutotambuliwa kwa deni la Kampuni ya mbolea Tanzania Sh.44,730 bilioni Kikao cha baraza la Mawaziri kilichokaa tarehe 19 Disemba, 2011 kilikubali ombi la kuitaka Serikali ilipe deni la TFC kwa benki za ABC na CRDB la jumla ya Sh.44,730,685,274. Serikali ilikubali kulipa deni hilo kwa mikupuo minne kwa kila mwaka miaka mitano kuanzia
--	--

	<p>tarehe 1 Aprili, 2012. Kila mkupuo Serikali ilikubali kulipa Sh.2,831,824,054 (CRDB Sh.1,445,540,472 na ABC Sh.1,386,283,582). Deni hili lilikuwa bado halijaingizwa katika orodha ya madeni kufikia tarehe 30 Juni, 2012.</p> <ul style="list-style-type: none"> • Deni laNIDA MOI ambalo halikuungizwa vitabuni Sh.78 bilioni. Serikali iliidhamini NIDA kwa Sh.55 bilioni kutoka kwa umoja wa Mashirika ya Pensheni na kiasi cha Sh.20 bilioni kutoka NSSF. Pia iliidhamini MOI kwa kiasi cha Sh.3 bilioni kutoka NHIF. Madeni hayo yatalipwa kupitia Wizara mama ya Mashirika hayo kwa hiyo ni sehemu ya deni kamili la Taifa ambalo lilikuwa bado halijahesabiwa kama sehemu ya deni la Taifa ilipofika mwisho wa mwaka. • Marekebishoya deni la Taifa yasiyodhibitishwa Sh.619.804 bilioni Uhakiki wa mchanganuo wa madeni ya Taifa kama ulivyokuwa tarehe 30 Juni, 2012 ulibaini kuwepo kwa marekebishi ya deni ya Sh.619,803,554,183.91 ambayo uongozi haukuweza kutoa maelezo ya kuridhisha. • Kutotambuariba ya benki itokanayo na kuchukua fedha zaidi ya amana iliyoko benki Sh.40.013 bilioni Katika mwaka huu, ukaguzi umebaini kuwa deni la Serikali liliongezeka kwa kiasi cha Sh.283.005 bilioni ambacho kulingana na sheria ya Benki Kuu ya mwaka 2006 kilisababisha riba ya Sh.40.013 bilioni kiasi ambacho mpaka mwisho wa mwaka kilikuwa hakijalipwa na hakujumuishwa kama sehemu ya deni la Taifa mwishoni mwa mwaka. • Malipobila nyaraka/maelezo yanayojitosheleza Sh.62,192,330,297 Katika mwaka huu wa fedha, Serikali ililipa PSPF Sh.62,192,330,297 kama mchango wa nyongeza kwa watumishi wastaifu. Hata hivyo hakukuwepo na vigezo vilivyo bayana katika ukokotoaji wa nyongeza hiyo. Pia
--	--

	<p>uongozi haukuwa na taarifa za wastaa fu hao badala yake walitegemea taarifa za PSPF pekee katika uidhinishaji wa malipo na hivyo kupelekea kushindwa kuhakiki uhalali wa usahihi wa malipo hayo. Pia kiasi kilicholipwa hakikuwa sehemu ya deni la Taifa lililokuwepo mwishoni wa mwaka tarehe 30 Juni, 2011. Hii ina maana kuwa kiasi cha deni la Taifa mwanzoni kwa mwaka huu wa fedha halikuwa sahihi pia.</p> <ul style="list-style-type: none"> • Mambomengineyo Kulikuwa na ongezeko kubwa la deni la Taifa mwishoni mwa mwaka. Wakati tarehe 30 Juni, 2011 deni la Taifa lilikuwa Sh.14,441,617,937,770.20 kiasi hiki kiliongezeka mpaka Sh.16,975,962,626,745.20 ilipofika tarehe 30 Juni, 2012 likiwa na ongezeko la Sh.2,534,344,688,975 sawa na asilimia (17.5%) ya deni la mwaka wa nyuma. Zaidi ya hivyo kulikuwa na deni la kimkataba la Serikali la kiasi cha Sh.577,537,084,848 kwa mwaka 2011 ambalo halikujumuishwa na deni la Taifa. <p>Ongezeko la deni la Taifa lilisababishwa na mikopo mipyä, malimbikizo ya riba na kubadilika kwa thamani ya kubadilishia fedha za kigeni. Hata hivyo kiasi kikubwa cha deni hilo la Taifa kilitumika kulipia malipo nje ya nchi na kuchangia kwenye bajeti ikifuatiwa na kuboresha maisha ya wananchi na elimu na usafirishaji na mawasiliano. Ilithibitika pia kuwa deni la ndani kiliongezeka kutokana na Serikali kubadilisha deni la benki (Bank overdraft) la Sh.469.48 bilioni kuwa dhamana maalum ya Serikali (Government Bond) ya miaka 10 ili kuiwezesha Serikali iendelee kupata mikopo ya muda mfupi kutoka Benki Kuu kwa ajili ya kuendesha bajeti yake.</p> <p>Kwa upande mwingine, ongezeko la deni la nje limesababishwa na ongezeko la ukopaji wa Serikali kwa ajili ya kusaidia bajeti ya Serikali. Kati ya kiasi chote cha deni la ndani la Serikali Sh.192.1 bilioni zilikopwa kwa njia</p>
--	---

	ya “Treasury bills” na Sh.185.2 kutoka “Treasury bonds” kwa ajili ya kusaidia bajeti.
3	Fungu 34: Wizara ya Mambo ya Nje na Ushirikiano wa Kimataifa
	<ul style="list-style-type: none"> Hati zamalipo za kiasi cha Sh.917,542,796.83 hazikutolewa wakati wa ukaguzi. Aidha malipo ya jumla ya Sh.115,000,000 hayakuwa na nyaraka za kutosha; kwa hali hiyo uhalali wa malipo hayo haukuweza kuthibitishwa. Masurufuya jumla ya Sh.706,701,016.36 yaliyolipwa katika mwaka ulioishia 30 Juni, 2012 yalikuwa bado kurejeshwa kinyume na Kanuni ya 103 (1) ya Kanuni za Fedha za Umma za mwaka 2001 (zilizorekebishwa 2004). Kutokana na hali hiyo matumizi yaliyoonyeshwa katika taarifa za fedha hayakuwa sahihi kwa kiasi sawa na masurufu yasiyorejeshwa.
4	Fungu 98: Wizara ya Ujenzi
	<ul style="list-style-type: none"> Malipo ya madeni ya mwaka wa nyuma yaliyolipwa kwa fedha za 2011/2012 kwa kutumia jina la mradi usiohalisi Shs. 252,975,000,000 Miradi katika Wizara ilipewa Namba 4168 kwa ajili kuitishia malipo ya madeni ya miaka ya nyuma kwa miradi inayotekelawa na TANROADS. Namba hii siyo halisi na hivyo kusababisha kutolewa kwa taarifa za hesabu zinazoonyesha matumizi zaidi kwenye hesabu za maendeleo. Fedha za usimamizi zilizotumika kwa shughuli nyingine zisizoidhinishwa Sh.802,000,000 Fedha za maendeleo zilizotolewa na Hazina (Kifungu kidogo 2005) na taarifa ya utekelezaji katika hesabu za wizara ilionyesha kuwa Sh. 802,000,000 ziliidhinishwa na Bunge kutumika na TANROADS katika usimamizi wa miradi 35 ya barabara. Hata hivyo licha ya fedha hizo kutolewa na Hazina kwenda Wizara ya Ujenzi fedha hizi hazikupokelewa na TANROADS na badala yake zilitumika kwa shughuli isiyoidhinishwa kibajeti ya kulipa madeni ya

	<p>miaka ya nyuma ambayo hayakuwa yamelipwa hadi kufikia mwisho wa mwaka wa fedha 2010/2011. Kwa hali hii jukumu la msingi la kusimamia utekelezaji wa miradi ya barabara halikufanyika ipasavyo.</p> <ul style="list-style-type: none"> • Fedha za ufuatiliaji kubadilishwa matumizi na kutumika kwa matumizi yasiyoidhinishwa Sh.576,053,081 Bunge liliidhinisha Sh.666,600,000 katika mwaka huu wa fedha kwa ajili ya kufuatilia utekelezaji wa miradi 33 ya barabara katika makubaliano ya mwaka ya utekelezaji kati ya Wizara ya Ujenzi na TANROADS. Hata hivyo Wizara ilitumia kiasi cha Sh.90,546,919 chini ya kifungu kidogo 2005 kwa ajili ya ufuatiliaji na bakaa ya Sh.576,053,081 ilibadilishwa matumizi kwa matumizi ambayo hayakuidhinishwa na Bunge. • Kuonyeshwa matumizi zaidi katika Hesabu za maendeleo Sh.252,975,000,000 Mhutasari wa Hesabu za maendeleo ulionyesha matumizi zaidi kwa Sh. 252,975,000,000 kutohana na sababu kuwa kiasi hiki kilitumika kulipia madeni ya miaka ya nyuma ambayo hayakulipwa hadi kufikia mwisho wa mwaka wa fedha 2010/2011. Matumizi halisi yanatakiwa yasijumuise Sh.252,975,000,000 na hivyo matumizi sahihi yalitakiwa kuwa Sh.615,486,241,504. Wizara kupitia Kurugenzi yake ya Huduma za Ufundis ilibadilisha matumizi ya skimu katika fedha zilizotolewa kwa TBA. Wizara ilitoa maelekezo kwa TBA jinsi ya kutumia fedha hizo Sh.395,075,722. Matumizi haya hayakuainishwa katika bajeti ya Wizara kama ilivyopitishwa na Bunge. <p>Masuala mengine</p> <ol style="list-style-type: none"> a) Kutokuwepo kwa kadi za kuonyesha kumbukumbu za mapokezi , utoaji na bakaa ya vifaa katika ghal ya vifaa vyenye thamani ya Sh.122,865,647 b) Rasilimali za kudumu zisizokuwa na kumbukumbu za
--	---

	<p>utambulisho zenyetamani ya Sh.210,090,658</p> <p>c) Makadirio halisi yaliyoidhinishwa katika Hesabu ya maendeleo yalionyesha upungufu kwa Sh.59,735,946,904. Makadirio halisi yalionyesha kimakosa kuwa ni Sh.869,354,067,451 badala Sh.929,090,014,356.</p> <p>d) Makosa katika taarifa ya Mtiririko wa Fedha -Akaunti ya Maendeleo Sh.830,464,381,143 Gharama za Ununuzi/Ujenzi wa rasilimali za kudumu zilionyesha kwamakosa kuwa Sh.830,630,573,072 badala ya Sh.577,489,381,143.</p>
5.	Ubalozi wa Tanzania - Muscat
	<p>Fedha za makusanyo ya mapato zilizopelekwa pungufu benki (OMR.20,965) sawa na Sh.83,771,821.75</p> <p>Mapato ya jumla ya OMR.20,905 sawa na Sh.83,771,821.75 zilizokusanywa kutoka vyanzo mbalimbali vya mapato ikijumuisha visa hazikupelekwa benki kinyume cha kanuni ya 78(1) ya Kanuni za Sheria ya Fedha ya Umma ya mwaka 2001 (iliyorekebishwa 2004).</p>
6.	Ubalozi wa Tanzania Abu Dhabi
	<ul style="list-style-type: none"> • Mapato yaliyokusanywa hayakupelekwa benki (Dhs.77,560)sawa na Sh.33,360,614 Tuligundua kuwepo kwa mapato ya jumla ya Dhs.77,560 sawa na Sh.33,360,614 zilizokusanywa kutoka vyanzo mbalimbali ikijumuisha visa ambazo hazikupelekwa benki kinyume na Kanuni ya 78(1) ya Kanuni za Sheria ya Fedha ya Umma ya mwaka 2001 (iliyorekebishwa2004).

Masuala mengine

- **Ucheleweshwaji wa kupeleka fedha za makusanyo ya mapato fedha benki kwa wastani wa siku 30 hadi 90**
Kinyume naKanuni ya 78(1) ya Kanuni za Sheria ya Fedha ya Umma ya mwaka 2001 (iliyorekebishwa2004) ubalozi ulikusanya Dhs.394,310 sawa na Sh.146,051,066 kutoka vyanzo vyake vya ndani lakini fedha hizo zilibaki bila kupelekwa benki kwa wastani wa siku 30 hadi 90.
- **Karadha ya mshahara ambayo haijalipwa (Dhs.35,000) sawa na Sh. 15,047,900**
Kiasi cha (Dhs.35,000) sawa na Shs.15,047,900 kilichotolewa kwa mtumishi wa ubalozi tokea mwaka 2007 hakijarejeshwa na hakuna juhud zozote zinazofanyika kurejesha fedha hizi toka kwa mhusika.

SURA YA 8

MAJUMUISHO NA MAPENDEKEZO

8.0 Majumuisho

Matokeo ya ukaguzi katika taarifa hii yaliwasilishwa kwa Maafisa Masuuli wote kwa ajili ya utekelezaji. Maafisa Masuuli wanatakiwa kuandaa taarifa ya utekelezaji wa mapendekezo na kuyawasilisha kwa Mlipaji Mkuu wa Serikali-Wizara ya Fedha.

Katika taarifa hii nimebainisha dosari na mapungufu mengi katika mifumo ya udhibiti wa ndani yaliyosababisha na kuwepo mianya na usimamizi dhaifu wa fedha. Masuala haya yanatakiwa kushughulikiwa na Maafisa Masuuli kwa kuweka mifumo thabiti ya udhibiti wa ndani na itakayolenga kuzuia kabisa kutokea tena kwa mapungufu haya.

Ili kueleza kikamilifu mapungufu niliyoyataja katika taarifa hii, nimewajibika kutoa tena mapendekezo yangu kuhusu dosari nilizobaini katika ukaguzi, ambayo kama yatakelezwa, yataweka usimamizi bora wa masuala ya fedha ndani ya Serikali.

8.1 Mapendekezo

8.1.1 Kutotekeleza mapendekezo ya miaka ya nyuma

Serikali imeonyesha jitihada katika kutekeleza mapendekezo yaliyotolewa katika kaguzi za miaka ya nyuma (2008/09, 2009/10 na 2010/11). Hata hivyo, kwa baadhi ya mapendekezo yaliyoko katika taarifa hizo, hakuna ushahidi ulio wazi katika maelezo ya Serikali unaoonyesha kuwa hatua zinazoelezwa kweli zimechukuliwa. Serikali iongeze jitihada na kuhakikisha kuwa mapendekezo ninayotoa yanatekelezwa kwa wakati ili kuzuia kutokea tena mapungufu au dosari za aina hii, kwani itasaidia kuimarisha uwajibikaji serikalini na kuongeza ufanisi katika utoaji huduma kwa umma wa Tanzania

8.1.2 Stadi ya jinsi ya kuongeza mapato ya serikali

8.1.2.1 Misamaha ya Kodi

Mambo yafuatayo yanapendekezwa kwa serikali kama njia ya kuongeza mapato yake:

- Kwa manufaa ya Taifa na wananchi kwa ujumla, ni vyema mikataba ya kuchimba madini ikajadiliwa na Kamati ya Bunge inayosughulikia masuala ya madini na ushauri kutolewa kwa waziri mhusika kabla ya kusainiwa.
- Hati za misamaha ya kodi ziwekwe bayana kuwa msamaha wa kodi ni wa muda gani, unaanza lini na kumalizika lini.
- Misamaha ya kodi iainishwe ikionyesha malengo ya kiuchumi, kijamii na kisiasa yanayokusudiwa kufikiwa ambayo yanajumuisha mambo yafuatayo:
 - Kuanzisha ajira
 - Upatikanaji wa bidhaa na huduma
 - Ongezeko la mapato yatokanayo na kodi za ajira, Kodi ya Ongezeko la Thamani, kodi za ndani n.k.
 - Kupata ujuzi, utaalam, uwezo wa usimamizi kwa waajiriwa wazalendo
 - Kuongeza thamani ya bidhaa zinazozalishwa nchini.
 - Kupanuka kwa shughuli za uchumi wa ndani ya nchi
 - Manufaa ya teknolojia kwa uchumi wa nchi
 - Mikataba yote yenye vipengele vya misamaha ya kodi ipitiwe na Mwanasheria Mkuu wa Serikali kwa ajili ya ushauri kabla ya kusainiwa na pande husika.
- Uwekwe muda ambao mwekezaji atatakiwa kueleza manufaa yatokanayo na misamaha waliyopewa na kiasi cha mapato yaliyopatikana, vyote hivyo vikilinganishwa na mipango kazi aliyojipangia mwekezaji na makubaliano ya malengo yatakayofikiwa ndani ya muda kama itakavyokubaliwa na Serikali. Hii itaisaidia Serikali kufanya tathmini ya kama kuna manufaa kuendelea kutoa misamaha kwa wawekezaji husika. Uhakiki wa mara kwa mara unatakiwa kufanya na TRA pamoja na NAO kupitia kaguzi maalum ili kujiridhisha kuwa misamaha ya kodi iliyotolewa inatumika vizuri.

- Wizara ya Fedha ichukue jukumu la kuipatia Ofisi ya Taifa ya Ukaguzi, orodha ya misamaha yote iliyotolewa kwa kila mwezi
- Ufutiliaji wa misamaha ya kodi uanzishwe ili kufutilia misamaha iliyotolewa na Wizara ya Fedha kuitia Tangazo la Serikali (G.N.); uanzishwe mfumo wa kutunza kumbukumbu utakaoziunganisha TRA na Wizara ya Fedha.
- Mfumo wa Ufutiliaji wa Misamaha ya Kodi uanzishwe katika Idara ya Kodi za Ndani.

8.1.2.2 Utozaji kodi kwa mapato yatokanayo na sekta isiyo rasmi

Kodi kutoka kwa wafanyabiashara na wachimbaji wadogo wa madini Serikali inashauriwa kufanya yafuatayo:

- Kuwepo kwa vitambulisho vya Taifa kutasaidia ufutiliaji wa walipa kodi na kuongeza idadi ya usajili wao. Kwa hali hiyo, utozaji wa vitambulisho vya Taifa uende sambamba na usajili wa walipa kodi wapya. TRA itakiwe kufutilia jambo hili kwa karibu.
- Juhudi zaidi ziongezwe kutoa makadirio ya kodi kwa wenyewe biashara ndogo ndogo.
- TRA iwalusishe kikamilifu Katibu Kata katika kuwatambua walipa kodi kama vile wamiliki wa kumbi za harusi, mikutano n.k.
- TRA iendeshe kampeni ya Elimu kwa Mlipa Kodi kwa sekta isiyo rasmi kwa njia ya kufanya mashauriano na viongozi wa vikundi, taasisi zisizo za kiserikali n.k.

8.1.2.3 Kodi za pango

- Watu wenyewe utajiri mkubwa waangaliwe upya kwa lengo la kukusanya mapato yatokanayo na mali wanazomiliki kama vile majengo
- Serikali itafiti ili kujua thamani ya majengo kwa ajili ya utozaji kodi.

8.1.2.4 Kodi kutokana na wakulima wadogo

- TRA iwalusishe kikamilifu Katibu Kata katika kuwatambua wakulima wadogo wanaolima kibiashara katika Kata zao

- Kutoa vitambulisho kwa ajili ya kuwatambua, kuwasajili na kuwafuatilia walipa kodi.

8.1.2.5 Kodi kutokana na biashara ya kuhamisha fedha kwa njia ya simu za kiganjani maarufu kama M- Pesa, Tigo Pesa n.k.

Kampuni za simu za kiganjani zinazofanya biashara ya kuhamisha fedha zitakiwe kukata kodi ya zuio kama vile asilimia tano (5%) ya malipo ghafi ya kamisheni inayolipwa kwa wanaofanya biashara hiyo ya kuhamisha fedha kwa niaba ya kampuni. Kodi hiyo ya zuio ipunguzwe kutoka kodi ya mwisho itakayotakiwa kulipwa na kampuni hizo za simu.

8.1.2.6 Maduhuli yasiyotokana na kodi

8.1.2.6.1 Kubadili haki ya kumiliki ardhi na kodi ya ardhi

- Mfumo Funganifu wa Taarifa za ardhi uanzishwe haraka ili urahisishe uwekaji kumbukumbu sahihi za viwanja kwa nchi nzima. Utaratibu huu utasaidia kuondokana na utaratibu wa kutunza kumbukumbu usiokuwa wa kielektroniki.
- Wizara ya Ardhi itakiwe kufungua akaunti katika Wilaya ili Halmashauri ziweze kuweka moja kwa moja makusanyo yatokanayo na kubadili hati za kumiliki ardhi na kodi za viwanja.
- Wizara ya Ardhi itakiwe kuajiri wahasibu ambao watasaidia kukusanya mapato na kuwajibika moja kwa moja kwa Wizara ya Ardhi tofauti na utaratibu wa sasa ambapo watumishi wa Halmashauri wanaokusanya mapato ya aina hiyo wanawajibika kwa Mkurugenzi Mtendaji wa Halmashauri.
- Kutoa elimu kwa umma kuhusu tofauti kati ya kodi ya ardhi na kodi ya majengo ili kuongeza uzingatiaji wa sheria.
- Kufanya mapitio ya viwango vya kodi ya ardhi vilivyopo kwa lengo la kuviboresha kwani vinachangia upungufu wa mapato
- Serikali kupitia Wizara ya Ardhi iwekeze katika miundombinu ya utoaji taarifa za ukusanyaji wa mapato kwa siku, wiki na mwezi.

- Tozo pamoja na riba inayoongezeka kila mwezi ianzishwe ili wale wasiolipa ada ya viwanja kwa wakati walazimike kufuata sheria na kulipa ada ya mwaka kama inavyotakiwa. Stadi ya kuongeza mapato imebaini pamoja na mambo mengine kuwa wanaomiliki ardhi/viwanja huacha kulipa ada kwa vile wanao uwezo wa kulipa riba kutokana na viwango vinavyotozwa kuwa vidogo.
- Wizara ya Ardhi ije na utaratibu kwamba wakati wa kusajili hati miliki ya ardhi au kubadili umiliki wa ardhi, iwe ni lazima kwa anayesajili hati/kupewa kiwanja au kubadili umiliki kuwa na namba ya utambulisho wa mlipa kodi (TIN). Hii itasaidia kuongeza mapato ya serikali.

8.1.2.7 Mauzo ya mazao ya misitu

- Wizara ya Maliasili na Utalii ifikirie kutoa motisha kwa watumishi wake. Aidha, Wizara iongeze kiwango cha maduhuli yanayobaki katika Halmashauri (asilimia 20 kwa sasa) kwa lengo la kutoa motisha kwa Halmashauri zinazokusanya maduhuli hayo kwa niaba ya Wizara.
- Watumishi wasiokuwa waaminifu walioteuliwa na Mkurugenzi wa Misitu wachukuliwe hatua za kisheria kwa vitendo vyao vya kuinyima serikali mapato kwa makusudi.
- Kuzileta pamoja wizara za serikali wakati wa kutoa leseni au vibali vya kisekta.
- Tozo itolewe kwa wafanyabiashara watakaobainika kughushi nyaraka kwa lengo la kunufaika na ukiukwaji huo wa sheria.
- Watumishi wenye sifa waajiriwe ili kusaidia ukusanyaji wa mapato
- Ofisi za Kanda zianzishwe katika mikoa na zipewe jukumu la kusaidia ukusanyaji wa mapato yasiyotokana na kodi.

8.1.2.8 Vitalu vya uwindaji - Ada ya uwindaji

- Wizara ya Maliasili ifikirie kuanzisha ofisi za kanda mikoani zitakazokuwa na jukumu la kusaidia ukusanyaji wa mapato yasiyotokana na kodi; watumishi wenye sifa wapelekwe katika ofisi hizo kusaidia kazi ya ukusanyaji mapato.

- Kuboreka kwa ukusanyaji mapato kutategemea pia kutolewa mafunzo kwa wakusanyaji mapato katika ngazi ya halmashauri
- Wafanyabiashara wasajiliwe na kupewa namba ya utambulisho wa mlipa kodi kwa lengo la kuwatambua wasiolipa ada za uwindaji na kuboresha ulipaji ada hizo kwa hiari.

8.1.2.9 Mrahaba kutokana na uchimbaji madini

- Inapendekezwa kuwa utaratibu wa Exit Vouchers System (EVS) uanzishwe katika ofisi za kanda ili kuongeza mapato yatokanayo na utozaji mrahaba kwa wachimbaji wa kokoto
- Shughuli za TRA na Wizara ya Nishati na Madini zifungamanishwe na taasisi hizi mbili zishirikiane ili kuhakikisha kuwa mapato yote halaliyanakusanywa. Hii ni pamoja na kushirikiana katika upande wa rasilmali watu katika masuala ya usimamizi wa mapato ili kupunguza gharama.
- Sheria ya Kodi ya Mapato ya mwaka 2004 inayowataka wafanyabiashara kuwa na TIN ifuatiliwe kwa karibu wakati wa utoaji leseni kwa wachimbaji wadogo na wa kati.
- Kutokana na tofauti iliyopo kati ya taarifa za malipo ya mrahaba baina ya serikali na kampuni za uchimbaji madini, ni muhimu kwa serikali kufanya usuluhisho wa mara kwa mara wa taarifa hizo ili kujua kiasi sahihi cha mrahaba kinachopaswa kulipwa serikalini.

8.1.2.10 Hifadhi ya mbuga za wanyama za Taifa (TANAPA)

Mambo yafuatayo yanapendekezwa kwa serikali:

- Ushuru wa hoteli za kitalii ulipwe kwa kiwango maalum badala ya viwango vinavyobadilika.
- Serikali iboreshe namna mapato yanavyokusanywa na kuweka utaratibu wa kisasa zaidi.
- Serikali ihakikishe kuwa Sheria ya Fedha Na. 13 ya Mwaka 2008 na Waraka wa Hazina No.8 of 2008/09 unaoyaagiza mashirika na makampuni binafsi kuchangia katika Mfuko Mkuu wa Serikali inazingatiwa

